# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

## VERBATIM REPORT OF

## CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, VOI CONSTITUENCY AT ACK TAUSA CHURCH

## ON

## APRIL 30, 2002

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARING ,VOI CONSTITUENCY HELD AT ACK CHURCH TAUSA ON APRIL 30, 2002**

**Present:**

1. Com. Abubakar Zein
2. Com. Keriako Tobiko
3. Com. Prof. Wanjiku Kabira

**Secretariat Staff in Attendance:**

1. Fatuma Jama - Programme Officer
2. Onesmus Kipchumba - Assistant Programme Officer
3. Alice Thuo - Verbatim Recorder
4. Nancy Odipo - Sign Language Interpreter

**Mkutano ulianza saa tatu 9.30 a.m na Com. Abubakar Zein.**

**Com. Zein:** Ningependa kukitambua kikao hiki kama kikao rasmi cha Tume ya kurekebisha Katiba minajili ya kukusanya maoni ya wakenya ili kuirekebisha Katiba yetu.

I would like to formally declare this as a sitting, formal sitting of the Commission, the Constitution of Kenya Review Commission for the purpose of collection of views to amend our Constitution. Ningemwachia Madam aendelee baada ya kusema hivyo.

**Fridah Mwadime:** Ningeomba Mwakeshi, kwa hisani yako tafadhali waandikishe hawa ndugu zetu haraka nataka tuanze. Ningetaka tuombe sote pamoja. Nafikiri tukisubiri wale wakiandikishwa labda ningeanza na kujijulisha kwenyu badhi yenyu mnanifahamu, wale ambao hawanifahamu, natajifahamisha kwenu halafu mtanifahamu. Kwa majina ni Fridah Mwadime, mimi ndiye mshirikishi wa mambo ya Katiba katika wilaya ya Taita Taveta, na niko hapa kwa sababu ya shughuli hii kama mshirikishi. Pia na kama mmoja wenu, maana ni mwana kamati wa sehemu ya uakilishi bunge ya Voi. Ningependa tena kuwajulisha wanakamati ambao wanawakilisha sehemu mbali mbali za sehemu ya taarafa hii ili mkaweze kuwajua hadi tunavyongojea watu wakijiandikisha pale. Labda ningeanza na mwenye kiti wa mambo ya katiba sehemu ya uakilishi bunge ya Voi Bwana Joseph Mwawasi, labda ungesimama usalimie wananchi.

**Mr. Joseph Mwawasi:** Hamjambo wananchi?

**Mwadime:** Ahsante. Ambaye anayeshikila wadhifa wa mwandishi wakati huu maana mwandishi wetu yule ambaye alichaguliwa na kamati amesafiri ni bwana John Mayanga nafikiri nyote mwamfahamu.

**John:** Hamjambo?

**Mwadime:** Wengine ni wale wameketi pale. Kuna yule ambaye ni mwenyeji wa hapa ni Bwana Rokins Mate. Rokins nafikiri yuko nje. Halafu mmoja wa wandishi pale ni Bwana Stanley Mwakeshi ambaye anawakilisha sehemu ya Location ya Ngolia. Halafu tuna mama pale kutoka sehemu ya Marungu anaitwa Irene Maranga anaandikisha pale. Halafu tuna mmoja wetu kutoka Sirau ambaye ni Rev. Silvanus Mwakoma na kati ya hawa wanakamati pia kuna Mstahiki Meya wa Voi Municipal, ni mwanakamati. Halafu kuna mwanakamati mmoja wetu ambaye ni Mjumbe wa mahali hapa anajiandikisha pale akimaliza atawasalimia. Tutampatia nafasi awasalimu, ni mwana kamati kwa hivyo kuna kamati ya watu kumi. Na Mheshimiwa Mwakiringo, karibu na pengine ukikaa kidogo tu, usalimie wananchi kwa maana wewe ni mmoja wapo wa kamati yetu ijapo wewe ni Mbunge wa mahali hapa. Karibu Mheshimiwa. Pengine ungesalimia wananchi. Ooh .. badaye (**laughter**) Ahsante, watu bado wangali wanajiandikisha. Labda pengine ningempatia (**interjection prayers**). Nafikiri tungeanza kwa maombi na ningeomba mmoja wa wanakamati Rev. Silvanus Mwakoma aje atuanzia na maombi tafadhali. Na hapa ni Kanisani japo tumepachukua kama mahali pa kuchukulia maoni. Ningeomba ndugu zetu ambao wana vichepeo kwa hisani zenu mnaweza kuziondoa kwanza kupeana heshima mahali hapa. Na pia nimekumbushwa na mmoja wetu kwamba pia sigara tusivute hapa. Asanteni.

**Rev. Silvanus Mwakoma**: Basi wapendwa wananchi, ni wakati mzuri tujiweke kwa bwana ili tukaendelee na shughuli hii ya kutoa maoni kwa ajili ya Kenya yetu, kwa ajili ya Katiba yetu. Mimi kama mlivyosikia ni member lakini kuna mchungaji mwenzangu wa kanisa hili, na kwa sababu ameingia, naomba tafadhali, Ndugu karibu, Rev. karibu utufungulie kwa maombi.

**Host Rev. Captain Alphonse:** Bwana asifiwe sana,basi mini ni Captain Alphonse Karingo, mchunganji wa kanisa hili la A.C.K. Tausa. Nafurahi kwa kuwa mmefika na kwa kuwa wakati umeenda sana basi tufunge macho tuombe.

Baba mwenyezi Mungu uishie milele, tumekuja mbele zako Bwana tukijua kabisa wewe ni Mungu Mkuu. Vyumbe vyote vyakutegemea wewe, kila hali tuliyo nayo humu nchini ni wewe unayetuongoza. Leo hii Bwana, twajiweka mikononi mwako, hasa wenzetu waliokuja kutoka sehemu mbali-mbali. Tunapokaa hapa Bwana kuendelea kujadiliana na kuzungumza maneno mengine, mengineyo ambayo yanatufaa sisi wenyewe, endelea kutupa nguvu ya kuzungumzia hayo mambo na hata kufikia mwisho, tuwe tumepatana kwa kila hali Mungu wetu. Wale walio mbali ambao hawajafika, endelea kuwaongoza vyema na wakifika Bwana tuendelee kushirikiana pamoja na hata tunapomaliza shughuli hii Bwana, mkono wako wa baraka tuuone katika maisha yetu na tuendelee kuishi vyema dunia hii. Na tufikapo mbinguni Bwana, tupate kuuridhi ufalme wa mbinguni kupitia kwa

Mwanao Yesu Kristo tumeomba. Amen.

**Com. Abubakar Zein**: Kwa heshima na taadhima kubwa, ningependa kuwaamkua tena, habari ya asubuhi? Mimi naitwa Abubakar Zein, mimi ni mmoja wa makamishna, na ningependa kuchukua fursa hii, kuwaomba makamishna wenzangu, wajitambulishe kwenu, halafu niwaelezee mambo kadha kabla hatujaanza, basi kupokea maoni yenu. Nitaanza na aliyeko kwangu kabisa mkono wa kushoto kule, halafu nirudi hapa karibu na mimi.

**Com. Wanjiku Kabira**: Hamjamboni, mimi naitwa Wanjiku Kabira. Ahsanteni.

**Com. Tobiko**: Hamjambo ndugu? Naitwa Keriako Tobiko na mimi ni komishna.

**Com. Zein**: Kama nilivyosema mimi naitwa Abubakar Zein na tumekuja hapa kwa minajli ya kupokea maoni yenu kuhusu ubadilishaji na urekebishaji wa Katiba yetu. Ningependa kuwagusia tu utaratibu tutakaotumia ili tuwe na nidhamu na kazi yetu iwe rahisi, wote tufanye kazi hii kwa wepesi. Ukiingia pale mlangoni, unakuta wenzetu wamekaa pale wanaandikisha watu majina, majina hayo yanaandikishwa kwenye fomu kama hii. Ikishajaa majina, tunaletewa sisi halafu sisi tutaanza kutumia majina hayo kwa kuita mtu aliye wa kwanza, wa pili, kufuatia utaratibu huo. Ukishaitwa jina lako kutoa maoni, kuna njia tofauti za kutoa maoni.

Ikiwa umeandika maoni yako katika maandishi, kwa mswaada, yaani memorandum una fursa ya kuja hapa na kutuzungumzia tu mambo muhimu yaliyo katika maandishi hayo.Hutakikani kuja kutusomea ule mswaada. Tunaomba sana uchambue yaliyo muhimu, peke yake, uyagusie, halafu utatupa mswaada huo sisi tutaenda kuusoma. Mtu ambaye ana maandishi atapewa dakika tano, kugusia yale mambo muhimu. Akimaliza kuzungumzia yale mambo muhimu, kamishena mmoja au makamishna hapo watakuwa na haki ikiwa kuna jambo ambalo wanataka ulifafanue, wanaweza kukuuliza swali. Na ikiwa kuna mmoja wetu ambaye pengine atakereka sana, na awe anataka kuuliza swali, anaweza kutuomba kwa kutuandikia kikaratasi kwamba anaomba kuuliza swali. Halafu ukimaliza kutoa maoni yako namna hiyo, utaenda hapo karibu na yule binti anayeandika. Utaandiaka jina lako Kwenye register kwamba umetoa maoni halafu utupe yale maandishi. Hiyo ni kwa kutoa maandishi . Ikiwa pia unataka kutoa maandishi bila kuzungumza, unaruhusiwa kufanya hivyo. Wakati wowote ukiwa na maandishi yako unaweza kwenda pale ukayatoa, ukajaza register. Ukimaliza hapo unaweza kukaa kusikiliza wenzako wanasema nini au pia unaweza kupata ruhusa ukaenda zako kushughulikia mambo mengine ya kujenga taifa.

Ukiwa hauna maandishi yeyote, unataka kuzungumza tu, maoni yako kuyatao kwa mazungumzo, tutakupa dakika kumi. Dakika kumi hizo tunakuomba sana ukiwa unazungumzia shida ni vizuri lakini pia uzungumzie mapendekezo yako ya kuitatua shida hizo, unataka zitatuliwe namna gani? Sijui kama tunaelewana?

Ukimaliza pia baada ya kutoa maaoni yako, kwa kauli pia utajaza jina lako pale. Tutakaa kwenye kikao hiki nafikiria kutoka

sasa, ni saa nne, mpaka saa kumi na mbili jioni.

Ikiwa imefika wakati huo na bado kutakuwa kuna watu wengine hapa pengine hatujawafikia, tutashauriana mnataka tufanye vipi, kwa sababu pengine kutakuwa kuna giza. Tutashauriana . Kwetu nyumbani kule Mombasa waswahili wanasema penye wengi hapaharibiki jambo. Au panaharibika jambo? Kwa hivyo tutashauriana ikifika wakati huo kama hatujapata kuwafikia wengine. Nyingine ambalo ni muhimu kufahamu ni kwamba unaweza kuzungumza kwa kiswahili, kwa kiingereza au pia ukitaka kutumia lugha yoyote ya Kenya, tuseme mfano kitaita, unaruhusiwa kuzungumza kwa kitaita. Tutakuwa na fursa ya kumchagua mmoja wetu atafsiri ikiwa utachagua kuzungumza kwa kitaita atafsili ili sisi sote tuwe tunaelewana.

Jambo lingine ambalo ni muhimu kufahamu ni kwamba, sisi tunarekodi mambo haya kwa kutumia rekoda. Huyu binti yuko hapa atakuwa akirekodi kwa tepu rekoda maneno yote. Sisi tutakuwa tukiandika kwa maandishi baadhi ya mambo unatuambia, lakini tutarekodi kila neno unalosema ndiyo hata neno moja lisipotee. Tukifika Nairobi, yale maneno yataandikwa yote katika mswaada. Kwa hivyo, usiwe na wasiwasi ukiona pengine nimesitata kidogo na kalamu uniambie “mbona wewe huandiki?” Tunarekodi kila neno.

Jambo lingine la muhimu wewe kufahamu ni kwamba hakuna mtu yeyote au taasisi yoyote inaweza kukuchukulia wewe hatua kwa maoni unayotoa hapa. Maoni haya ukitoa ni yako, unaruhusiwa na sheria kusema unavyopenda wewe. Hakuna mtu yeyote ambaye atafanyiwa matatizo yeyote kwa maoni anayotoa. Na pengine kwa jambo la mwisho kuomba, kwa vile mimi ni mpwani kama ninyi, tuseme yote yaliyo moyoni mwetu, lakini tutumie maneno murua. Siyo tu kwamba, kwa vile tuko kanisani kama alivyosema yule bibi kwamba watu wavue kofia na kuheshimu taadhima ya mahali hapa lakini kwamba ni vizuri tuwe tunabadilishana mawazo, tutumie lugha ambayo inaweza kusikika na wazee na kina mama na watoto pia. Sijui kama tunakubaliana kwa mambo haya?

Jambo la mwisho ambalo ningependa kuwaarifu na kukubaliana na nyinyi ni kwamba, nimewaambia tutatumia utaratibu huu; mtu aliyefika kwanza ndiye atakaye pewa fursa ya kuzungumza mbele, kutafika wakati pengine tutawaomba ninyi mturuhusu sisi kubadilisha utaratibu huo kidogo. Kwa mfano, akatokea bibi mja mzito hapa, tungewaomba mtupe ruhusa sisi tumpe nafasi ya mbele azungumze halafu aruhusie kwenda kupumzika akitaka kufanya hivyo. Kukatokea mtu mzee ambaye hawezi kuhimili au kustahamili kuchoka kwa kukaa kwa muda mrefu, tutawaomba pia mtupe fursa hiyo. Au akija mtu mgonjwa, sijui kama mnakubalia mambo hayo?

**Audience:** Ndiyo

**Com. Zein**: Tukifanya hivyo halafu tunarudi kwenye utaratibu wetu, tunaendelea na list vile vile ilivyoandikwa. Ahsanteni sana. Sasa ningependa kutoa kipaaza sauti hiki kwa ndugu yangu Tobiko ambaye ni Kamishna mwenzangu atakaye tuanzishia

mkutano wetu. Kuna swali lolote? Ndugu Tobiko.

**Com. Tobiko**: Ahsante sana Commissioner Zein. Tuanze na Naftali Mwanjele.

**Interjection:** Yeye ametoa.

**Com. Tobiko**: Yeye amaetoa akaenda. Pauline Mbachu. Nenda pale.

**Pauline**: Nimewasalimu kwa jina la Bwana. Mimi natoa maoni ya kuhusiana na kina mama, tuliketi kina mama wa Ndome Sub-location.

**Com. Tobiko**: Mama tafadhali, taja jina lako tena, liwe recorded.

**Pauline**: Naitwa Pauline Kishaga Mbachu. Tuligusia ulipaji kuhusu mtu akiuliwa na mnyama wa pori, alipwe milioni mbili badala ya malipo ya elfu thelathini. Chakula kikiharibiwa, tulipwe kwa afisi za Division badaya ya kwenda kuchukua shiling mia mbili kwa ofisi ya District. Haki za urithi wa ardhi, tuligusia kuwa mbuga za wanyama wa pori, National Park, zirudishwe kwa waakaji wa hapo zilipo ili wananchi wa hapo karibu wapate malisho na mashamba. Kuwe na tume ya ardhi ikirudishwa wilayani ama kwa Division.

Mamlaka ya Rais, tulisema hivi vipengele vitatu, serikali iwe peke yake, mahakama yawe peke yake, bunge liwe peke yake. Rais asiwe Amri Jeshi, na Rais asiwe Mbunge, achaguliwe moja kwa moja.Rais asiwe akifanya mkataba na serikali za nje bila kuhusisha bunge.

Tukagusia serikali za mkoa, Meya na ma-Chairmen wawe wakichaguliwa moja kwa moja na wananchi badala ya ma-councilors.

Kuhusu pombe, tuligusia tukiwa kina mama, vilabu vya pombe virudishwe ili license halali ziende kwa District ama kwa County Council badala ya pombe kutengenezwa ovyo ovyo na watu wanaletewa pombe kutoka pahali pengine ambazo zina madhara kwa waume wetu. Turudishiwe pombe ile ya kienyeji ya mwasina. Kuhusu afya ya mama, mtoto na family planning, hizi huduma tulionelea zirudishwe na ziwe za bure.

Bunge viti vya bunge theluthi, moja chini ya tatu vitengewe kina mama. Bunge liwe likiangalia usalama wa nchi. Kuwe na tarehe maalum katika Katiba ya kufanya uchaguzi. Mbunge asipotoa huduma kwa wapiga kura wake, wawe na uwezo wa kumrudisha nyumbani na atakaye fuata wa pili achukue kiti hicho. Mbuga za pori, tuligusia mapato ya mbuga za pori, 75% yarudishwe kwa District ili wanufaike kwa pesa hizo. Maji kama hii ya mzima springs kama City Council ya Mombasa irudishe kodi kama 25%

ili wakaaji wa Taita Taveta wahudumiwe na pesa hizo. Pia tukagusia, maji hayo yanapita moja kwa moja sisi hatuyapati. Tupewe huduma hizo. Katiba, tuligusia Katiba isiwe ikibadilishwa bila kuhusisha wananchi kama kwa vipengele vya uchaguzi, kuhusu ardhi,mipaka ya mikoa, hata na uakilishi wa bunge. Ahsanteni Kama kuna swali niko tayari.

**Com. Tobiko**: Asante sana mama, unaweza kujiandikisha pale na uweze kupeana karatasi yako. Jael Mwangore?

**Jael Mwongore**: Nawasalimu wananchi. Jina langu ni Jael Mwangore na tulizungumza haya machache na akina mama tulipokutana hapo Tausa. Jambo la kwanza tulizungumza juu ya tohara, tukasema upashaji wa tohara uondolewe kabisa. Maana unaharibu vile maumbile yaliumbwa na Mungu na hata wakati msichana kukaa nyumbani kwake ama wakati wa kuzaa anapata taabu zaidi. Kwa hivyo tulionelea kwamba tohara iondolewe kabisa.

Tukaja unajisi. Watoto wadogo kunajisiwa na mababa na watu ambao wanakaa nyumbani. Mwanume akinajisi mtoto mchanga, kina mama walisema akatwe uume kabisa akae hivyo hivyo. Ndio kina mama walionelea namna hiyo.

Halafu tukaja kutengana, yaani divorce. Bibi na bwana wakitengana, mali yote igawanywe katikati, hii ni kama nyumba, pesa, mashamba na kadhalika.

Mengine ni yale yale ambayo yamesemwa kule kwa hivyo sitaki kurudia. Kuoa; tukasema watu wanaoa kanisani, kisheria, kitamaduni. Hapa kuwe na cheti kamili. Zote ni njia za kuoa na ni vizuri baba mwenye wake wengi awape uridhi sawasawa.

Watoto wadogo wasioenda shule, hatua ichukuliwe na utawala yaani Assistant Chief kwa wazazi na iwe ni adhabu kali kwa mzazi ambaye anaweka mtoto bila kumpeleka shule. Halafu tukaja kwa afya; afya, ya mama mja mzito, mama pamoja na mtoto wa miaka mitano wahudumiwe bure kwa kila jambo. Kama ni mgonjwa, ahudumiwe ipasavyo.

Nafikiri yangu ni hayo, yale mengine ni yale yale ambayo tumeyazungumza. Ahsante.

**Com. Tobiko**: (Question inaudible).

**Jael:** Tunasoma kwa magazeti, tunaona baba anawachwa na mtoto mchanga, halafu kisha baba mtoto ameharibu mtoto yule yule aliyemzaa. Je huyo atakuaje? Kina mama walisikia vibaya sana moyoni, wakaona huyo afadhali akatwe uume maana yule mtoto ni mtoto wako. Wewe baba mtoto ndiye anayelinda mtoto, sasa kama mlinzi si baba, mlinzi atakuwa ni nani?

**Noisy Interjection**

**Com. Tobiko:** Tafadhali (interjection) No. Hiyo ni maoni yake, kama una maoni tofauti, ungojee mpaka utoe na tukusikize sawa sawa. Gabriel Mbogo? Thomas Mwambui?

**Thomas Mwambui:** Mimi ni Thomas Mwambui, ninatoa maoni yangu binafsi. Mimi kwa maoni yangu, naona kutunga Katiba peke yake hakutoshi kwa sababu, ni mioyo ya watu ambayo ingegeuka. Katiba peke yake haitoshi. Kitabu peke yake kuwekwa hakutoshi. Kwa sababu mimi nafahamu tuna manifesto ya KANU ambayo imeweka malengo ya chama hicho cha siasa. Lakini katika maoni yangu naona tangu tupate uhuru mpaka sasa, hatujatimiza yale malengo. Kwa mfano, elimu ya bure, Elimu ya bure mimi sijaiona mpaka sasa na watoto wengine wanapata taabu ya kusoma hasa waendao sekondari. Watoto wa maskini, wasio na uwezo, tunawaacha, hatuwajali kwa sababu hatutimizi tunayoandika. Twapendekeza dini ihubirie watu wageuke mioyoni ili hali katika nchi yetu iwe bora zaidi. Na pia nikagusia kidogo juu ya matumizi ya budget, nafahamu ziko pesa watu wa Kenya wanatoa, pesa nyingi, kodi ambazo tunatozwa (Pay As You Earn) pesa nyingi hizi, lakini hazifikii watu mashinani. Kwa mfano, hazifiki kwetu kule Ngongonyi, Lungalunga, Wajir, Lamu, hazitoshi. Na ndiposa, katika manifesto yangu hapa nimependekeza serikali inayofaa ni ya Majimbo. Kwa sababu kama tunakuwa na Majimbo huyu mtu aliye Ngongonyi, LungaLunga, Lamu, Wajir anaweza kuonekana kwa urahisi na serikali ya Majimbo.

katika maoni yangu, ninaona kama tungekuwa na jimbo la Pwani, serikali kuu iwe kule Mombasa, ni rahisi mtu wa Mombaa kuona Mngongonyi anahitaji nini. Mtu wa Lungalunga anahitaji nini! Mtaveta anamwona kwa urahisi. Aliye Nairobi ni shida kumuona mtu huyu.

Tangu tupate uhuru mpaka leo, mimi mzee wa miaka sabini na tano, karibu nitamaliza miaka sabini na tano July kumi nane, mwezi wa Saba. Mpaka sasa maisha yangu hayajakuwa bora zaidi tangu nipate uhuru. Najiona kama bado, kwa sababu tumesema hapo mwanzoni tunaandika Katiba, tunaweka Sheria, tunawachagua Wabunge, wanakwenda bungeni. Lakini mioyo yao haijabadilika.

Pia nikagusia juu ya vyama, vyama ninaona vimezidi, vimekuwa vingi. Tuwe na vichache visizidi kumi na viwili, visipungue vitano. Pia nikagusia uhusiano na Mataifa ya nje. Naona kama misafara inayotoka nje ina watu wengi. Sioni kama kuna haja ya kuenda nje sana maana ikiwa misafara itakuwa ikitoka nje, ilete faida kwa Taifa hili. Si kugarimu serikali hii, kutumia pesa nyingi kupeleka msafara mbali na watu wanapora pesa. Pesa hizo zingetumiwa na maskini na walemavu. Mimi nina mmoja nyumbani kwangu, nimemlea kwa miaka ishirini na saba, nikapata taabu mpaka sasa. Hana fahamu, ananyea kule kule kwenye chumba na kazi anafanya hapo hapo nyumbani na mimi mtoto huyo na bibi yangu tumemlea kwa miaka ishirini na saba.

Serikali haijanisaidia chochote. Napendekeza, walemavu, wazee, watoto wasio na kazi, maskini, wajane wawe na vituo vilivyojengwa na serikali kisha walelewe huko. Kwa mfano, kule Amerika pia ninafahamu wazee wanalewa na serikali. hata mtoto wangu anafanya kazi ya kuwalea wazee huko America. Akili za watu, wale watu hodari, wanatoka Mngongonyi, wanakwenda mjini Mombasa, wanakwenda Nairobi, wanakwenda America, wanakwenda Uingereza kuishi huko kwa sababu maisha kule nyumbani ni ya taabu. Mtu anayeyaweza ni mimi, mzee. Mtoto wangu aliye na degree hawezi hao maisha hata kidogo.

Barabara ni mbaya, hakuna hospitali, mja mzito aende Voi kuenda kuzalia huko. Gari anabahatisha, azalie njiani, mtoto pengine afe. Hakuna huduma za kutosha kule Ngonyonyi kwa hivyo ndiyo sababu ninapendekeza majimbo. Walemavu, wazee, watoto wasio na kazi, maskini, wajane ninaona kwamba ni Serikali ya majimbo ambayo inaweza kuona hayo mahitaji ya watu kama hao niliowataja. Pia ninaona, nimegusia kidogo juu ya mbuga ya wanyama. Hivi karibuni, kuna watu wawili waliouwawa, sijui kama watapata compensation. Sijui kama watafikiwa na serikali, lakini hii 62% ya mbuga ya wanyama nafahamu pia kwamba, kumbe sisi hutuimiliki, ardhi ina milikiwa na serikali ya Uingereza. Mpaka sasa, kutoka mwaka wa sitini na tatu mpaka leo, title deed ingali nje. Si ifaidi nini? Hi national park.

Watu wanao dhaminiwa ni wanyama kuliko mimi binadamu. Watu hawa wawili waliokufa, sijui kama wazazi wao watalipwa na nani! Napendekeza 62% ya mbuga iliyoko hapa Taita irudishwe kwa wataita, na wataita wenyewe waamue wataitumia namna gani. Iwe ni nchi yao, si inchi ya wakoloni tena! Ama ya malkia tena, iwe ni ya Wataita.

Pia ninaona kwamba ile sehemu yetu tuliyowachiwa wataita ya kutumia ni kidogo sana. Kama haitawezekana, ile 62% (sitini na mbili kwa mia) kurudi kwa wataita, napendekeza sehemu ya mbuga ya wanyama, ikatwe irudishiwe wataita kwa sababu wataita wanaishi mahali padogo sana. Kwa sababu nimeandika memorundum yangu natumaini pengine mkiwa na maswali, mnaweza kuniuliza. Lakini hii ni yangu binafsi, siko katika kikundi chochote.

**Com. Tobiko:** Ahsante sana mzee Mwambui

**Com. Zein**: Kuna swali tumeulizwa kuhusu maoni yanayofanana hatuzuii mtu yeyote kutoa maoni yanayofanana wala hatusemi kwamba ukija hapa useme, “hayo yameshasemwa sitayataja”. Unaweza kuyataja ili kuyatilia mkazo. Sijui kama tunaelewana?

**Audience:** ndiyo

**Com. Zein:** Utasema kwamba mtu amezungumza kuhusu haki za wanawake au kuhusu mbuga ya wanyama. Mimi nataka kuzungumzia hayo hayo na ukatilia mkazo Lakini usiingilie tena kwa kina kilichotajwa na mwenzako.Sijui kama tuko sawa hapo?

**Audience:** Sawa

**Com. Zein:** Na kabla sijakaa chini, mimi nitakuwa nimefanya makosa kama sikusema namshukuru sana Mzee Thomas kwa kuja yeye hapa na nina sababu kubwa ya kusema hivyo. Kwa sababu yeye ni mwalimu wa mwalimu wangu. Mzee Thomas kamfundisha Mzee Joseph Mwawasi na Mzee Joseph Mwawasi kanifundisha mimi Alidina visram!!

**Audience:** (Kicheko)

**Com. Zein:** Na isitoshe, Mzee Thomas alikuwa ni mmoja wa mwakilishi wa raia, katika serikali za mikoae katika Katiba ya Majimbo. Sijui wangapi wenu mnajua hayo? Na mwisho kabla sijatumia fursa hii vibaya, mwenzangu akaniambia, "kaa chini", huyu binti anayewaangalia, sio kwamba nimesahau kuwajulisha hawa wenzetu. Lakini kwa vile MIC zina matatizo, hatuna zile za mkono, naona tutapoteza wakati mimi kuwajulisha tu huyu binti aliyekaa akiwaangalia hapa ni Mtafsiri wa Ishara. Kwamba akija mwenzetu ambaye ni mlemavu hasikii, yeye ataanza kazi ya kutafsiri, kwa hivyo ukiona ameanza kutafsiri, usione ukajiuliza ni kwa nini anafanya hivyo. Atakuwa anatafsiri kwa mtu ili mwenzetu aweze kufuatilia mambo haya tunayoyazungumzia. Ahsanteni.

**Com. Tobiko** Ahsante Commissioner Zein. Nathaniel Mutunji (**not clear**) ooh, alipeana memorundum. Cosmas Mwakio …. Pia yeye. J. Mwawana, Mwawana?

**J. Mwachia:** Wapendwa nawasalimu kwa jina la Yesu. Kwa jina naitwa Joseph Mwachia Wamwana. Kwa maoni yangu, maoni yangu ninayotoa kuwa pombe isirudishwe, pombe isirudishwe.

**Com**. **Tobiko**: Umemaliza?

**J. Mwachia:** Ah – nimemaliza.

**Com**.**Tobiko.:** Amemaliza ahsante sana, sawa kabisa (laughter). Richard Landi, Richard Landi, Richard Landi, David Mwakuja?

**David Mwakuja**: Kwa makamishna na wananchi wenzangu, jina langu ni Daudi Mwakuja Jeffa.

**Com**. **Tobiko**: David Mwakuja.

**David:** Na ningependa kutoa maoni yangu kuchangia hii Katiba ambayo tunataka kutengeneza. Na kwanza, ningetoa shukrani kwa serikali kutupa wakati huu, wa kuweza kushiriki katika Katiba hii. Katiba ya kwanza ilitengezwa wakati wa mzungu akiondoka. Sisi hatukuapo na tunashuru sana.

Serikali ambaye ilikuwa inaondoka, ilikuwa imeacha Katiba iliyotengezwa ya majimbo, na hii ilikuwa ni kusudi ya kulinda masilahi ya jamii zote za nchi hii. Tukienda katika bibilia, Mungu aligawanya makabila na aligawanya kama mataifa. Wataita walikuwa na sheria zao na mamlaka yao. Kwa hivyo mimi ningechangia kwamba, serikali, sheria ambazo tunatunga sasa ziwe za majimbo. Majimbo haya, watafanya uchaguzi na watakuwa na bunge lao ambalo litakuwa chini ya Governor. Na mu-Governor huu utazunguka kwa kila kabila la jimbo lile kwa muda wa miaka mitano.

Serikali ya majimbo iliyo na mamlaka kamili, ya nchi ile, ya jimbo lile, wawe na uwezo wa kutoa passport, kutoa tittle deed, wawe na polisi wao. Serikali ya jimbo iwe na uwezo wa kuweza kukataza mtu kutoka jimbo lingine ikiwa tabia zake zitakuwa mbaya ama kumkubali kama amekuja kwa nia nzuri. Serikali ya jimbo hii iwe na uwezo wa kuchunguza ma-tittle deeds ama vibali vyote vilivyotolewa hapo awali, ambavyo vitakuwa vimetolewa kiharamu. Jimbo litasimamia, ama litaangalia masilahi ya jamii yake, ya jamaa ya jimbo lile na kila mtoto afikapo miaka mitano awe ametengewa kiasi cha shamba, ambaye ndiyo italinda jamii mingi. Sasa wataita hawana mashamba, kwa hivyo wawe na mipangilio ya miaka mia moja ya watu wa jamii. I mean, watu wa mkoa huo.

Jimbo hili liwe na mamlaka ya kuchukua kodi na jimbo hili linapochukua hizi kodi liwe linaweza kupeleka ishirini na tano kwa mia (25%) tu kwa serikali kuu. Mipaka ya jimbo, ya majimbo ichunguzwe. Tangu wakati ule mkoloni alipotoka kuna uhalifu mwingi sana umefanywa wa kubadilisha mipka ya majimbo. Tukizungumzia kama hapa Taita sasa, mpaka umesongeshwa mipaka maili nafikiri thelathini, ishirini kutoka Mtito-Andei. Hilo ni kosa kubwa sana maanake wataita wenyewe hawakuhusishwa. Kwa hivyo, mipaka hiyo ichunguzwe na irudishwe pale mahali mkoloni alipokuwa anaondoka. Jimbo liwe na uhuru na mamlaka ya kuweza kuitisha mkopo kwa mataifa mengine, umoja wa mataifa, ama mahali popote linaweza kupata mkopo direct. Isiwe inapitia kwa serikali kuu.

Nikirudia, serikali iliyoko sasa, muda wa Rais upunguzwe ama ubaki vile vile miaka kumi na mamlaka yake ipunguzwe. Asiwe na mamlaka juu ya Jeshi. Panapotokea vita asiwe na amri ya kuweza kuamrisha vita mpaka bunge liitwe, liweze kujadili.

Mali yote iwe chini ya Jimbo na hiyo mali yote ni kama nchi, national parks, madini, mali yote ya nchi na watu pamoja iwe chini ya jimbo lile. Maana kama hivi sasa national park, kuna watu ambao kwao wamekula mpaka nyoka, lakini wako hapo. Kwa hivyo, idadi ya wanyama wetu imepungua sana kwa sababu watu waliowekwa pale hawajui kuishi na wanyama. Sisi tumeishi na wanyama tangu vizazi na vizazi kwa hivyo sisi, majimbo na national park na yarudishwe kwa jimbo. Majimbo pia yatasimamia mambo ya maskuli, mahospitali, mahali zote ambazo ni za kuhudumia mwananchi wa jimbo lile.

Ikiwa mtu atatoka jimbo lingine kufanya kazi, alipishwe kodi ambayo itakuwa special ya kuchangia akiba ya jimbo lile Na ni kodi mwananchi atalipa, lakini kodi ya mtu ambaye ametoka nje kufanya biashara katika jimbo lile iwe ni lazima atalipishwa kodi ya mtu ambaye ametoka jimbo lingine akija kufanya katika jimbo letu. Nikichangia hayo, nafikiri mengi yameshazungumzwa. Na pia jimbo liwe na mamlaka ya kufuata kama ni wakoloni walipora nchi yao, wafuate ridhaa, walipwe ridhaa katika maharibifu ambayo yalifanywa. Kwa mfano kama hapa, Wakenya, I mean watu wa pwani wameporwa sana. Wameporwa sana. Kwa hivyo ikiwezekana, wapewe mamlaka ya kuweza kufuata kama ni Uingereza, kama Germany, kama ni nani alikuwa amepora nchi hii, arudishe mali ile ama alipe ridhaa kwa mali ile alipora.

Kwa hivyo tukizungumzia kwamba mali nyingi, kama mashujaa wetu, vitu vyao vingi vimechukuliwa viko Ulaya. Kwa hivyo,

jimbo liwe na mamlaka kuweza kufuata mali hiyo. Nikichangia kidogo kwa wale wenzangu waliozungumza, ni kwamba ikiwa, tutakubali sheria, mimi maoni yangu, tukubali sheria mwanaume na mwanamke kugawanya mali sawa. Nafikiri hiyo italeta uhasidi kwa sababu wanawake wengi watataka kuwachana na wanaume, wachukue ile mali wapeleke kwao. Labda wao ni maskini, watachukua ile mali wapeleke kwa jamaa zao. Pombe irudishwe, pombe ikirudishwa, hii inasimamiwa na serikali. Iwe na muda maalum ambayo mtu anakubaliwa kwenda kunywa. Sio kunywa kutwa. Na wenye vilabu wafungue kwa wakati utawekwa na serikali. Maanake kama pombe hii ni haramu, na hizo bia zipigwe haramu pia. Zipigwe haramu pia, ziharamishwe. Ahsanteni sana.

**Com**. **Tobiko**: Asanta sana, ngoja kidogo kuna swali. Commisisoner anataka kukuuliza swali.

**Com**. **Kabira**, Ningetaka uongezee kidogo juu ya yale mambo ulizungumza ya wanawake na wanaume (equality between men and women)

**David**: Kitu nimesema ni kwamba, maoni yangu ni kwamba, ikiwa wanawake, ambayo sheria itatungwa ya kwamba, ikiwa mali, mtu ameachana na bibi yake, mali igawanywe sawasawa, ile itachangia kuharibika kwa nyumba nyingi. Maanake wanawake wengi labda ni maskini, amekuja kwa nyumba ya tajiri akaleta chokochoko pale, ili awachwe, ili ile mali igawanywe.

**Com. Kabira**: Ok. Ahsante. Nina swali lingine pia. Ile 25% ile jimbo inapeleka kwa Central Government, Central Government, kazi yake itakuwa nini?

**David**: Central Government, ile ambayo Rais wake atachaguliwa na majimbo yote, atakuwa akisimamia uridhi wa nchi yote, maanake Kenya itakuwa ni moja tu. Lakini sasa, kila jimbo litakuwa na mamlaka ya jimbo lake na watu wake lakini mpaka yote litalindwa na jeshi laa nchi yote kwa jumla.

**Com Tobiko**: Ahsante sana, Bernard Babu.

**Babu**: Commissioner,s wananchi, kwa majina mimi naitwa Bernard Babu. Haya nayo - sema sasa mbele yenu ni maoni yangu. Kwanza, kitu ambacho nataka niseme sana kwa kutilia mkazo zaidi ni habari ya utawala, administration. Katiba ambayo inaendelea, iundwe, mimi kwa maoni yangu nasema hivi, utawala usinyanyase watu.

Lakini, ni ajabu, katika hapo, hapo ninapoishi katika vijiji, utaona hawa wazee wa vijiji wana kazi. Tena sana, zaidi na zaidi ambapo hawalipwi kitu. Wanafanya kazi ya bure.

**Com Tobiko**.: Pendekezo lako ni gani kuhusu hayo?

**Babu:** Pendekezo langu ni kwamba, nataka walipwe mishahara. Tena isitoshe, huo mshahara, hata kama watalipwa mshahara, maoni yangu ni kwamba wapewe vifaa kama mavuli , wapewe tochi, makabuti ya kunywea mvua maanake kwa nini nasema hivyo ni kwamba, wao wana msada sana katika kijiji. Kama pametokea kifo ama hatari yoyote yeye huzunguka kila sehemu ya nchi, kupiga filimbi ile ya kwamba pametokea kifo, pametokea nini na katika rural areas haswa kuna bush, kuna msitu sana, mtu anakwenda hakuna mwezi, hakuna taa, anapenyapenya kwe……..

**Com Tobiko**: Tunakuelewa.

**Babu**: Sasa hayo ni maoni haswa kwamba, walipwe mshahara. Maoni mengine pia ni kwamba, upande wa utawala, Chiefs na subchiefs wachaguliwe na wananchi. Wananchi wachague machifu wanaowapenda wenyewe.

Tatu, mbunge ambaye yuko ama ambaye atakayekuwako katika kila pahali pa utawala, awe huyo mbunge ametoka pale pale, kwa wananchi. Kwa nini nimesema hivyo? Kwa sababu pale kwa wananchi, ile lugha anayotumia ni lugha ya wananchi. Na Katiba itengezwe kwamba, ama useme kwamba mtu asitoke mkoa mwingine, ati tuna uhuru wa kuishi na kutawala, aje kupigania uchaguzi katika mkoa ule ambao si kwao. Na kuongeza zaidi ni kwamba, ninaunga, serikali ya majimbo. Zaidi naunga sana serikali ya majimbo iwekwe kwa sababu, serikali ya majimbo kama tuna governor, kwa mfano, Mombasa ama kokote, ni rahisi kumuona na kumuelezea. Siwezi kutoka hapa Taita niende Nairobi, ni vigumu. Mimi ninaunga mkono majimbo sana.

Hayo ndiyo maoni yangu ambayo nimesema. Katiba itengezwe kwa uangalifu na pia nawapa heko na ninawaombea baraka ninyi ma-commissioner, Mungu awabariki, kwa ninyi kuja hapa kusikiza maoni yetu. Na hayo ndiyo yangu, na mtanihakikishia baadaye ya kwamba msha yaandika.

**Com Tobiko**: Ahsane sana ndugu yangu, Ahsante Mwajuma Mwangongo, Mwajuma Mwangongo? Ameenda? John Mtoto? Stephen Mwakitawa?

**John Mtoto**: Wandugu wote namsalimu kwa jina la bwana. Yangu ni mazungumzo na mazungumzo yangu ni kama hivi, ni ya kuzungumza juu ya shida zilizoko. Jina langu ni John Mtoto na shida yetu iliyoko ambayo ningezungumza juu yake, ni juu ya njaa. Juu ya njaa ni hivi, wakati wote tunapata shida sababu ya njaa na tunataka tupatiwe suluhisho ya hiyo njaa. Na suluhisho lenyewe ni kutolewa maji ili tupate kulima na tupate chakula cha kutosha. Hilo ndilo langu la kwanza.

La pili, ni juu ya wazee. Tungeomba serikali, wazee watakapofika miaka sabini watunzwe na serikali. Hingine ni juu ya national parks. Lakini nafikiri hiyo ilizungumzwa.

**Com. Tobiko:** Ni sawa tu, usijali.

**John Mtoto:** Lakini kwa sababu yangu ni mazungumzo, kwa sababu yangu ni mazungumzo naweza kuzungumza. Ni juu ya National park na madini ambayo tunachimba katika sehemu yetu. Kwa mimi mwenyewe, ningesema ya kwamba, hizo sehemu zote zinazopatikana katika sehemu hiyo, National Park, madini yanayochimbwa ziwe zinaelekezwa kwa County Council.

La mwisho, ningesema kwamba watoto, kwa sababu wengi ni wale maskini, wapewe elimu ya bure. Ni hayo tu. Ahsanteni.

**Com**. **Tobiko**: Ahsante sana, ahsante sana. Jiandikishe pale mzee wangu, Stephen Mwakitawa.

**Stephen**: Hamjambo wananchi. Mimi ni Stephen Mwakitawa. Mimi ni Stephen Mwakitawa. Kwa nafasi yangu, maoni yangu ninavyofikiria, naona hii waya iliyopitishwa hivi mwaka wa tisaini na sita, ningependelea isongeshwe mbele, hata ikiwezekana ipelekwe kupelekwe mbele ya Irma sababu ndovu wanapita karibu sana na waya yenyewe imeendelea imefika Ndii. Sasa ndovu wanazunguka, wanakwenda zunguka mpaka waruka, wanaruka upande huu. Sasa wakijaribu, wakija upande huu, akijaribu kuruka upande wa chini, wanashindwa na ile waya. Basi kwa maoni yangu niliona ya kwamba ndovu ni wanyama wakubwa na wanawaumiza watu vibaya sana. Hivi juzi juzi, ndovu alizungunguka akaua mtoto mmoja hapa. Kwa hivyo hii waya naona ya kwamba, ikisongeshwa mbele ya Irima itakuwa, mbali, tena iende mpaka Athi River. Hapo nafikiri, itakuwa sawasawa, ndovu wawe upande wao. Sana sana, ningefikiria kwa hivyo pengine kama serikali inaweza fanya huruma kwa njia hiyo inaweza kuwa vizuri sana. Kwa hivyo mimi maoni yangu ni machache, ni hayo ninayoyazungumza.

**Com. Tobiko**: Ahsante sana mzee wangu, jiandikishe pale kwa mlango. John Kitawe, John Kitawe. Peter Mwanyalo?

**Peter Mwanyalo**: Bwana asifiwe. Nyinyi nyote nawasalimu kwa jina la Yesu. Maoni yangu ni kuanzia hapo kwetu kijijini juu ya wazee..

**Comm. Zein**: Jina, kwa jina mzee wangu na ukaribie ile microphone.

**Peter**: Jina langu ni Peter Mwanyalo. Maoni yangu ni juu ya hawa wazee wa kijiji na nilikuwa nikifanya nao ikawa ni taabu kubwa kabisa juu yangu, hawalipwi kitu. Maoni yangu walipwe. La pili, la pili dereva mlevi. Dereva mlevi anachukua watoto, anawapeleka mahali waendako, halafu yeye anangonja huko, anakwenda piga pombe yake, akija sasa gari, hataipeleka kama ilivyo, hajui kama anapeleka watu, basi hata gari ikigongana na mwenzake, yeye hajui chochote. Dereva aina hiyo, kwa maoni yangu, asipewe kazi. Lingine, lingine mimi niseme ya kwamba, yalizungumzwa lakini ilikuwa ikinigusia.

**Comm. Zein**: Kukugusia kivipi?

**Peter**: Pombe isirudishwe maana pombe ikirudishwa, hiyo ilioko, bado tunaona iko na taabu ndani ya manyumba hata

matumizi, vile vile nje, tunaona namna hiyo. Yangu inaishia hapo.

**Com. Tobiko**: Ahsante sana mzee wangu, jiandikishe pale chini. Fredrick Mwakundia.

**Fredrick**: Commissioners na wananchi wenzangu namsalimu kwa jina la yesu. Mimi ninatoa maoni yangu binafsi. Kitu nazungumza ni hi….

**Comm. Zein**: Rudia jina lako ndugu yangu.

**Fredrick**: Jina langu ni Fredrick Mwakundia. Nasimama hapa kutoa maoni yangu ya binafsi. Maoni yangu ya binafsi ni hivi. Ukweli ni kwamba serikali tuliyo nayo hivi sasa tunaijivunia tu kwa sababu tuna usalama. Lakini, hakuna chochote cha kutufurahisha juu ya serikali hii vile tunavyoendelea wakati huu. Maana tunaishi maisha duni kabisa. Watoto hawana kazi, parastatal boards zimekwisha hatujui tunaelekea wapi. Tunajivunia tu usalama. Kwa hivyo mapendekezo yangu ni haya;

Serikali hii ya leo iwe ya majimbo na kila jimbo liwe na Governor wake. Kisha, Rais achaguliwe kutoka kwa jimbo kulingana na vile anavyopendwa na wananchi. Na apewe kipindi tu cha miaka mitano akiwa mzuri, apewe ingine mitano, mwisho. Hata kama ana uzuri gani, aende, achaguliwe mwingine. Hiyo tu. Na kwa kweli ni kwamba tumefunga pombe, lakini watu wanaumia maana imekuwa ni ya kuiba, na kitu cha kuiba nikitamu sana. Ukizoea kuiba ni vibaya, wewe hutawacha. Afadhali vilabu virudishwe kimoja, kimoja kama zamani. County Council ipewe uwezo wa kutengeza hiyo pombe, halafu watu watakuwa wanaenda kunywa kwa County Council.

County Council zimefilisika, hazina pesa hata zimeshindwa na kulipa ma-councillors. Imekuwa shida. Hata hatujui tunaelekea wapi. Watoto hawana kazi. Tunasomesha watoto mpaka form four, wote sunarundika ndani ya nyumba. Kazi zimeharibika. Anakwenda anaandikwa kibarua wiki moja, mwezi mmoja, mwezi mwingine yuko nje.

**Com. Tobiko**: Pendekezo ni gani?

**Fredrick**: Sasa pendekezo ni kwamba, serikali hii ya majimbo, kila governor achunge rasilimali yake yeye mwenyewe. Maanake kwa mfano, hivi sasa tuko na madini hapa kwetu, lakini hakuna hata mkasiyao hata mmoja anaruhusiwa kuingia hapa. Watu wanatoka sehemu sijui ni wapi ndio wanamiliki hapa. Na sisi tutakuja kumiliki nini? National Park kubwa ni yetu, lakini hatuifahidi. Town ni yetu leo iliyoitwa city, lakini ukifika Mombasa, utacheka mwenyewe. Ni city aina gani hii? Siku hizi ndio afadhali kidogo usafi umeingia kwa sababu vibanda vimeondolewa ondolewa. Lakini ukifika Eldoret saa hizi utashangaa. Ile ikiitwa city na kweli na iwe ni city. Maana imenjegwa vizuri sana mpaka uwanja wa ndege maridadi. Na pesa zetu zote za national park zinakwenda huko, kila kitu kwa hivyo wazee……

**Com. Tobiko**: Kwa hivyo unataka aje?

**Fredrik**: Nataka national park hii yetu, irudi kwetu na rasilimali yote ya Coast Province ichungwe na watu wa Coast province wenyewe. Kila province ichunge rasilimali yake. Shukrani.

**Com. Tobiko:** Joseph Mwawasi;

**Joseph**: Jina langu kama mulivyoskia ni Joseph Mwawasi. Namsalimu nyote wananchi. Hamjambo?

**Wananchi**: Hatujambo.

**Joseph**.: Mimi narudi hapa, nilikuwa jana, nili present memorandum yangu na katika memorandum yangu nadhani nilikuwa na ma point kama tatu hivi. Majimbo, presidential powers na other grievancies. Lakini kwa sababu ya mazungumzo mazungumzo na wenzangu jana na wengine niliowaskia wakisema, imenilazimisha nije hapa kufafanua kitu kinachoitwa majimbo. Maana watu wengine wana hofu, maoni, naisikia maajabu sababu wengine wanaita economic majimbo, sielewi. Nasoma habari ya regionalism ya India, Regionalism ya America, United States of America, Canadian Regionalism, Australia, zote ni regional government. Na kila jimbo lina uwezo wake. Ukiita economic majimbo nasikia maanake eti ni ile raslimali tu mnazozi control. Na political power? Political power kwanza ndio number one. Political power, Rais Nyerere alikuwa anaiita 'shock'. Kwame Nkurumah anaiita political kingdom, "*shoot me first*", the first one. Ukipata ile shoka, sasa ndio anaanza kufanya kazi yaani ' shock'.

Huwezi kufanya decision katika jimbo lako kama huna ile political power. Ukiwachiwa eti "control minerals zako" na huna political power, utasikia Nairobi inasema ile, "after all we have the power". Hiyo kitu tumesema hatutaki. Kwa sababu iko huko Naiorbi. Jimbo lipewe kila kitu. Ile power ya ku-decide ni kitu gani tunataka kufanya. Ndugu huyu Mwakuja alinifurahisha sana, alisema kila kitu kinachofanywa katika jimbo liwe decided by majimbo. Hakuna mtu ambaye atakaye kuja ku-decide, uhuru ule uwe kabisa kamili. Isipokuwa moja tu, ambao wasipwe, na huo mmoja ni power to cede ile ifichwe, iende itiwe katika safe ambaye haitafunguliwa milele. Waamerica walipomaliza kufanya independence yao, walisahau hiyo. Halafu 1861 jamaa wa South wakasema "we must cede kwa sababu tunataka kuendelea na slavery na North wakasema "No", vita vikatokea. South ikamalizwa, ikashindwa halafu union ikaanza. Wakaapa wakasema "kutoka leo hakuna mtu, hakuna step, hata inaweza ku-cede in America".

Na hapa katika majimbo yetu, jimbo ni nchi kamili na kila kitu chake. Halafu tunawaambia, tunasema sisi wenyewe katika Bwana. Hata siku moja kusiwe na mtu yeyote anayefikiria ku cede wananchi ni kutoka, kusema sasa ile jimbo lile. Kwa mfano, wanyanza, tuseme ndugu zao wako Lamu, huko waseme kutoka leo sisi hatutaki kuwa wakenya, tunajiunga na Uganda, hiyo isitokee hata siku moja, kuna rafiki zetu hapa wasomali, wakati wa shifta walitusumbua sana, wanataka ati watoke waungane na

wasomali wa kwao. Hiyo hata siku moja isitokee. Kenya, mipaka ya Kenya tunaijua ni ile ile na itabaki vile vile, milele na milele. Lakini jimbo liwe na complete independence yake, hiyo ndiyo tunataka iwe ndani ya Katiba.

Sasa, kuna jambo lingine watu wana hofu hofu. Watu waliokuja hapa, wajaluo, Wakikuyu, walioingia katika jimbo lile na hakuna mtu (inaudible) hilo, hata mimi nikisikia watu wanaanza kufunganya, mimi natoka hapa. Hiyo sikubaliani nayo. Mtu yeyote aliye decide kuishi katika lile jimbo awe na haki sawasawa na indigenious person. Haki iwe kwa kila mtu. Tatizo ni wale wanaokuja sasa, baada ya kuunda majimbo, "eeh bwana" tutakuuliza "wewe unakuja kufanya nini?" Sisi tunatosheka hapa, unakuja kuchukua chetu. Unaweza kuwa criminal, tunaweza kumkaribisha criminal? Lakini wale waliopo kulea ni basi! Lakini kama unataka kwenda, unasema, "ah! Mimi siwezi kutawaliwa na governor mdigo," hapana wale wako wa akili nyingi zaidi za kijingajinga. Tumesikia, tumeziona katika magazeti "Mimi siwezi kutawaliwa na mtu ambaye hajatahiriwa", ati watu fulani tu wanafaa kuongoza ng'ombe, cattle, hawawezi kuongoza binadamu. Hii ilitoka wapi. Wote tumeumbwa na Mungu. Sote tu sawa. Sasa kama wewe bwana hutaki kuongozwa na governor Mtaita governor Mbajuni, basi kama hutaki, enda. Funganya. Akina (inaudible) si walienda zao? Kwa sababu walisema uhuru ukija nisikie Kenyatta ndiye waziri mkuu, mimi sitakaa hapa. Alienda, hatuna ugomvi na mtu kama huyo. Kwa hivyo, jimbo ni nchi kamili ambayo inajiamulia mambo yake kamili. Tunadanganyika. Juzi, kuna mambo haya yanaitwa District focus for rural development, hiyo ni namna moja ya majimbo. Lakini leo ni nani anayezungumza. Kwa nini haikuwa na political backing? Political backing was absent. Kwa hivyo leo haifanyi kazi sawasawa. Kwa hivyo, hiyo ndiyo nataka kufafanua kabisa, lakini huyu ndugu yangu Mwakuja, amenisaidia sana.

La mwisho, la mwisho ni hili la National Referedum; katika ile national convention, tunaambiwa kwamba wakienda kule watazungumza kwa miezi miwili. Kama hawatapatana, watarudi kwa wananchi kuuliza kura ya maoni. Sasa, kura ya maoni tulikuwa tunazungumza na jamaa mmoja jana, akasema hii kura ya maoni tunaweza kushindwa, wako hapo makabila mengine mengi kubwa, waki-vote wao peke yao, tutashindwa. Mimi suggestion yangu ni hii, lile litakalokuwa lina-pigiwa kura ya maoni liwe hivi. Provinces tano zikikubali, hilo litakubaliwa na wakenya wote, majority. Hilo ndilo nilitaka kufafanua. Ahsanteni.

**Com. Tobiko**: Ahsante sana mzee wangu unaweza kujiandikisha tena.

**Joseph**: Si nilijiandikisha jana?

**Com. Tobiko**: Lakini umeongea tena, (laughter) ndio tuwe na rekodi. Wilson Mwang'ombe?

**Wilson**: Ma-commissioners na wananchi, kwa majina mimi naitwa Wilson Mwang'ombe. Niko na maoni yangu ambayo ninahakika inawakilisha wengi. Tungependa kuona Katiba ambayo inajali maslahi ya watu wote ambao ni wananchi wote wa Kenya bila kujali status yao. Wawe ni wanaume, wake na kadhalika. Katiba ambayo inaweza kujua haswa wale ambao wameachwa wakati huu. Kwa mfano walemavu, Katiba ya sasa imewacha nje watu kama walemavu, kuna wale ambao wanaenda chini hawawezi kupiga simu kwa sababu simu ziko juu. Kuwa Katiba ya sasa ijali masilahi ya watu kama hao. Katiba

ambayo inaweza kuwasaidia wanakenya wote kugawanya ile keki ya kitaifa. Na kama kugawanya keki ya kitaifa kunahitaji mabadiliko basi mimi naunga mkono mambo ya majimbo. Sisi watu wa pwani, nafikiri ndio tumelemewa zaidi. Katika Katiba ambayo tukonayo. Tumelemewa namna gani? Tuko na raslimali zetu zile ambazo zimetajwa, nyingi lakini hazitufaidi. Tungeomba kwamba raslimali ambazo tukonazo zifaidi mwana pwani ama mwana voi constituency. Na kwa sababu tunaongea mambo ya majimbo ambayo naunga mkono, ningeomba raslimali zetu zifaidi watu wa hapa. Kuna miradi fulani ambayo imekuwa ikifanywa na political will. Kwa mfano, sehemu hii yetu ya Voi barabara ambazo mumekuja nazo mumeona, mpaka sasa, simu ya call box ni moja. Hatuna stima kwa sababu zile pesa ambazo tungefanyiwa nazo miradi hiyo zimeenda kusaidia watu wengine. So we would want, tungependa kuona kwamba benefits zibaki kwa watu wetu, na ziwe zimegawanywa equally. Kusiwe watu wengine wamepewa umuhimu zaidi kushinda wengine. Kwa mfano kama nilivyotaja, ukienda sehemu nyingine wako na kila kitu. Stima zimeingizwa mpaka vijijini, mpaka kwa choo huko ndani. Sisi hapa hata headquaters zenyewe hatuna. That’s a bit unfair.

Kumetajwa mambo ya lands, mambo ya national parks, nitagusia mambo ya national parks kidogo. Sisi nafikiri katika Kenya hii ndio tumeguswa sana na jambo hilo. Kwa sababu tuko na Tsavo East na Tsavo West na tuko na gates karibu arobaine na tano. Mamilioni ya pesa zinaingia lakini sisi hatujaona faida ya kukaa na wanyama hawa. Wametuua, wanyama hao wamekula chakula chetu, faida yake sisi hatujaona. Tungependa kusema hivi, uwandikishaji wa kazi katika K.W.S., shule ya kusomesha watu wanaoandikwa na K.W.S. iko hapa. Tungependa kuona uwandikishaji wa kazi ukifaidi vijana wetu wa hapa karibu, so that over 90% wawe ni locals ambao wameajiriwa kutoka hapa na may be 10% wewe wa ya kutoka sehemu zingine. Kwa nini nasema hivyo? Sisi ndio tunauwawa na ndovu, wanyama wa pori sisi ndio chakula chetu kinaliwa. Pili, kuwe na sheria kipengele, ndovu akivuka upande wetu, tumfanyeje? Kwa sababu sasa ng’ombe wetu wakivuka kwao sisi tunashikwa, na wamekula nyasi, hawajakula chochote, hawajaua mnyama, wamekula nyasi. Lakini wao wakija ndovu, wao wakija wanatuua, nothing happens.

Tungependa kuona kwamba kuwe na fair game, zao zikivuka, na sisi tuwe na ruhusa ya kuwapeleka kortini. Tuwashitaki na tulipwe gharama zile ambazo wametuharibia. Kuna waya ambayo imetajwa ya kuzuia ndovu kuja huku. Tulidanganywa tukaambiwa, “Nyinyi ni kwa sababu mnapata shida ya waya, wacha tuipige”. Nikapigwa “cha! next to the road. Sisi wakaaji wa hapa, mahali pa kuchunga hatuna. Wakati wa ukame, ng’ombe wetu wanakufa. Hii mbuga yote ni yetu. Tungeomba kuwe na kipengele hata kama itawezekana wakati wa ukame watu waruhusiwe mifugo wetu nao waingie wakule nyasi zisikule wanyama. Jambo lingine ambalo ningetaja ni mambo ya uwandikishaji wa kazi. Nimetaja K.W.S. maji ya mzima yanatoka hapa yanaenda mpaka Mombasa, hatupati faida yeyote.

Ukienda ofisini za maji, walioajiriwa huko, walioajiriwa kazi sio watu wa pwani, ni watu wa kutoka nje. Hatusemi ni vibaya, tunasema kuwe na fair game, tupewe first priority, tupewe percentage kubwa ili kwamba wenzetu ambao wanakuja kutafuta kazi wakute na sisi kidogo, tumeajiriwa. So all the jobs within coast province zipewe 90% wawe ni locals, na hizi ni mahali kama ukienda ma-hotels Mombasa, mahali kama port, tuko na port kubwa ambayo ukienda pale, watu wa pwani ambao wameajiriwa pale ni wachache. Watu ambao wameajiriwa wengi, bigger percentage ni ya kutoka nje. It should be the other

way round. Tuko na madini, mwenzangu ametaja, madini haya ni ya watu wa pwani. Sitaki kusema ni wakaaji hawa, nataka kusema ni ya watu wa pwani na ingeweza kufaidi watu wote wa pwani. Vile wenzetu walivyo na kahawa zao, chai na kadhalika ambapo mtu wa pwani hawezi kutoka hapa akaenda akatunda." Tungetaka mambo kama hayo, madini na kadhalika watu wa pwani nao wawe na sehemu kubwa. Kama ni uwezo umetushinda. Hatutaki kuambiwa tumelalia masikio. Labda mwenzangu angependa kusema tumelaliwa na hali. Serikali hiyo inaweza kutufinance. Iwe tunaweza kupewa mikopo, iwe tunaweza kupewa machinery ya kwenda kuchimba madini hayo kama hilo ndilo tatizo, but there should be a fair game kwamba kwa wale ambao wametoka nje na sisi wenyeji, wenyeji, wenyeji wachukue nafasi kubwa kwa kutumia rasilimali hizo.

Lingine ambalo ningetaja ni la uraisi, powers za Rais zipunguzwe particularly Rais asiwe mkubwa kushinda sheria. He should never be above the law. Hiyo ni moja. Pili, Rais apunguziwe uwezo wa ku-appoint zile key positions katika different institutions. Kwa mfano hizi parastatals, iwe mambo kama hayo yanaamuliwa na board na sio Rais peke yake kuchagua. Mambo kama Chief Justice, isiwe ni Rais anachagua, iwe inapitia kwa bunge. Chiefs and Assistant Chiefs niko na proposal mbili, either Chiefs na Assistant Chiefs wawe elected, wachaguliwe na wananchi kupitia kwa secret ballot na sio mlolongo au wawe transferable. Chief aweze kutoka hapa aende afanye kazi Voi, aende afanye kazi Mombasa, aende afanye kazi Kisiakao like any other civil servant. Tukifanya hivyo, na wao labda watakua a bit active na changa moto zaidi kufanyia wananchi maendeleo.

Mwisho, nikiendelea kumalizia elimu iwe ya bure kuanzia darasa la kwanza mpaka darasa la nane. Na sio bure ile tunaambiwa bure na huku tunalipa mamia ya pesa. Iwe bure na iwe ni lazima kila mtoto aliyezaliwa aende shule. Ile nyingine ya higher learning kuanzia form, form one (1) nakuendelea, hata kama kutakuwa na malipo, yawe yale ambayo yatakuwa affordable. Na kwenye hilo hilo, nakumbuka zamani tulikuwa tunaambiwa kuna Starehe Boys ambayo ni ya maskini. Leo hii, Starehe Boys sio ya masikini tena bwana, imekuwa ya wale wenzetu ambao wako na uwezo. Ningependekeza kuwe na shule ambazo zinaweza kusaidia familia zile ambazo hazina uwezo. Familia zile ambazo bila kusaidiwa, bila kupata bursary, hawawezi kusoma na shule kama ile Starehe kama itawezekana, irudishwe vile ilikuwa ya kusaidia watoto masikini.

**Comm Zein:** Niko na swali hapa, umesema shule kama starehe za wasiojiweza ziwepo tena ulikuwa unasema elimu iwe ya bure. Unasema nini hapo? Tunahitaji shule kama hizo za nini ikiwa elimu ni ya bure?

**Mwang'ombe:** Nimesema, from form one (I) upto form four (IV) Okay! Iwe payment ambayo iko affordable na affordability iko tofauti. Kwa mfano, siwezi kufuananisha shule za serikali na za private. Right? That's what I meant.

**Comm Zein:** Okay

**Mwang'ombe:** Nikimalizia, nasema Katiba ambayo nataka tuwe nayo iwe Katiba ambayo sio ya kuchezewa, Katiba ambayo kama itakuwa lazima ibadilishwe, isibadilishwe kwa sababu Rais ako na mamlaka ya kubadilisha. Kwa sababu sisi wananchi

tumeulizwa tukasema ibadilishwe kwa sababu ya kitu fulani Fulani. So, it should be as rigid as possible.

Mwisho, kama itawezekana, hatutaki Kenya tuendelee kuwa vile tumekaa. Maana vile nimefikia umri wangu, sijawahi soma Katiba. Kama itawezekana, Katiba ifundishwe kwa mashule yetu. Ili kwamba ikija kufikia wanafunzi, watoto wetu wakiwa wanajua haki zao, wanajua kutetea Katiba yao, na at the end of the day, wanaweza kujimudu na kugeuza.

Mwisho, nasema asante kwa kuja ndugu zangu Mungu awabariki na tuna hakika Katiba ambayo inayokuja itakuja Katiba ya kufaa kila mwananchi wa Kenya hii. Mungu awabariki.

**Com. Tobiko:** Ahsante sana. Jiandikishe pale pia. Mwangeka Richard?

**Mwangeka Richard:** Commissioners, mabibi na mabwana, hamjambo?

**Audience:** Hatujambo

**Mwangeka Richard:** Nashukuru ya kwamba mazungumzo haya yamefanyiwa kwa kanisa na kitabu kilicho hapa mbele yangu tukiwa wakirsto wa hapa Tausa, tunaamini neno la Mungu au nasema urongo?

**Com. Tobiko:** Taja jina lako ndiyo uendelee

**Mwangeka Richard:** Jina langu ni Richard Mwangeka. Hapa ni Bibilia, Kumbukumbu la Torati: Mlango wa thelathini na mbili, kifungu cha saba hadi cha tisa, kina sema hivi: "Mwenyezi Mungu aliumba nchi na akawapa kila Taifa na mahala pao. Taita Taveta, huyo ni nani? Ni mtaita, Kilifi kuwe nani? Mkilifi. Kwale kuwe mkwale, kisumu kuwe na Kisumu, Kajiado vile vile. Kwa hivyo ndugu zangu, serikali ambayo ningetaka iwe kuanzia leo, tukiandika maneno haya, ni serikali ya majimbo. Serikali ya majimbo, ambapo jimbo la pwani tunavyosifiwa, lina mali nyingi sana, hatungelia hivi. Kanisa hili lingekuwa limeisha likawekwa taa kila kitu. Kwa mali tulizo nazo. Hebu tujiulize Katiba iliyoko mwaka wa sitini na tatu (1963) ilikuwa ni gani? Ilikuwa ni Katiba ya majimbo, hata tumesikia sasa hivi mzee wetu Mwambui alikuwa mmoja wa wakilishi wakati huo. Kwa nini ikabadilika? Ilibadilika kwa sababu ya watu wachache werevu ili kufungua mlango.

Basi hebu tujiulize Katiba ilioko mwaka wa 1965 ilikuwa ni gani? Ilikuwa ni Katiba ya majimbo. Hata tumesikia sasa hivi mzee wetu Mwambui alikuwa huko wakilishi wakati huo. Kwa nini ikabadilika? llibadilika kwa sababu ya watu wachache werevu ili kufungua mlango tujaze nchi vile tunavyo ona sasa. Ndugu zangu njoo Voi uone sasa vibanda vyote ni watu wachache sana wataita wako nazo. Katiba hii tunayo andika iwe hakuna nominations katika Kenya.

Katiba hii tunayo iandika ndugu zangu ilegeshe kitu tuinaita Vagrance Act na watu wengine hapa hamuwajuii. Mwawaona tu.

Kumbe kwao waliua na wanakimbiaTausa. Wako hapa hapa tu hamuwajui. Kumbe walifanya makosa kwao. Hii Vagrance Act ilegeshwe. Mimi nimetumwa na chama cha Shirikisho Party of Kenya ambacho ndio advocate wa majimbo na nikaambiwa nije niseme hivyo hapa Tausa. Kwa wale wataita wanasema, "idimika, idimika". Wataka, hutaki serikali inayokuja ni ya majimbo. Ndugu yangu ukiwa hapa, sema Yesu ni Mwokozi , sawa sawa, ni majimbo. Kwanza nimeona kwa gazeti leo Commissioners mumechapwa kidogo na Reverend Musyimi.

**Com. Tobiko:** Tumezoea.

**Richard Mwangeka: Kumbe** mumezoea? Tungeomba muwaambie hawa watu watafanya Commission hii ikose uzito, wananchi wakose imani nayo kwa sababu kila siku kwenye magazeti tunaona kwamba kwa kweli tutakuwa na shida. Hata hivyo ndugu zangu Professor Ghai, Dr Ombaka, na lawyers nyote mlioko, some of you are historians . Kweli hamjui shida za Kenya? Ni mpaka tuongezewe muda? Bilioni 0.5 ni kweli lazima tuongezwe muda? Huyu ni mkikuyu, huyu ni mswahili wa Mombasa anajua shida vile tulivyo anza na waarabu nini na nini, si straight away we adapt majimboism, Constitution kwisha? Mambo yaishe. Si lazima tusikilize, nyuma uwasikilize hivi na hivi aha! Maanake leo nadhania mwenzangu angezungumza tofauti lakini ameni unga mkono – majimbo. Wako hapa walikuwa wakisema haya majimbo mbali. (taita dialect).

Jambo lingine ambaloningependa kusema ndugu zangu ni wakati wa kupiga kura. Nashukuru nimesikia zitahesabiwa katika vituo, katika gazeti Kivuitu amesema hivyo. Lakini, sisi wataita ni lazima tuje tusaidiwe kupiga kura na watu wengine? Ni lazima tusaidiwe? Hapana bwana. Nilivyosema kila mtu ako na kwao. Kwa nini wakifa wanakwenda kwao? Kwa nini hawazikwi hapa? Kwa nini? So what I mean is wakati wa kura, bwana wewe ni wa wapi? Ni wa Kiambu? Rudi huko ukapigie kura kule. Tuachie sisi tuchague mtu wetu. (**clapping).**

Maji : Tunataka sheria iundwe kwamba maji ambayo yanatoka katika district hii yaweze kufana au kufaa watu wa district hii. Pia kuwe na kifungo kinachosema railways wasi endelee kumiliki mpangiliwa wa maji. Sasa hivi hapa Tsavo kuna mambo pahali pa maji. Lakini hata hivyo ni serikali yenyewe ina zidi kuyanyasa wananchi kwa sababu mifereji iko. Kila kitukiko. Lakini wananchi wa Mbololo wame nyimwa. Kungekuwa na kilimo cha kufa na kupona hapo. Irrigation na kila kitu lakini ni bahati mbaya.

Mambo ya madini. Wenzangu walikuwa wakisema pole pole lakini hapana bwana. Mambo ya madini, nimekuja na mheshimiwa tukiyazungumza zungumza hivyo lakini ndivyo hivyo. Kitu ni ya kwamba madini kwanza, mkazirau angekuwa number 1 kupata ile mali. Angekuwa tajiri lakini ndiye maskini wa mwisho. That is very unfair. Hii sio siasa ndugu yangu. Tunaandika Katiba mpya ambayo itatufaa. Wale wakubwa wakubwa ambao wamechukua ardhi Kilimbasi, wapi, eh? Nasikia Kamlesh Pattni ameokoka. Lakini amezidi kuchukua ardhi ya wataita hapa ndani. kuwekwe kifungo kinasema kwamba Ardhi hii ibaki ya wataita wenyewe na watu wa pwani kwa jumla. Kuna watu hapa wanaongea ongea hivyo. Mimi ninasema hivi Provincial Administration, utawala mkoa uta ondoka wakati wa majimbo. Hautakuweko kwa sababu tutakuwa

na Governor. Provincial Commissioner atakuja kufanya nini? Leo hii, ni mfano nautoa, Rais amekuja wapi? Mombasa. Mtaita hatamwona Rais. Lakini watu kutoka huko juu, watamwona, sisi tunabaki mlangoni kwa gate hatumwoni. Lakini tukiwa na governor wetu, tutakuwa tukimwona tukimweleza shida zetu. Ama ninasema uongo?

Katiba tunayo unda isiwe questionable. Isibadilishwe overnight. Hapana. Lazima wananchi wajulishwe mambo haya. Political Parties. Vyama vya siasa. Mimi binafsi nimeondoka kwa Shirikisho, kusiwe na vyama vya siasa, Political parties zisikuwepo. Kwa sababu hizi political parties Zimetufanya tukawa maadui kweli kweli. Kuwe ni mtu anapigiwa kura awe ni Mwangeka, Mwangeka basi, hakuna chama. Mumeona ndugu zetu wa chama tawala wamefunga mabogi mengine ambayo si mazuri. Ni kuitikia tu, "yes sir, yes sir," ndio madhara tumeyaona katika Kenya hii.

**Com: Tobiko** Recommendation yako ni gani?

**Richard Mwangeka:** Nasema hivi; political parties zisiweko. Tuwe na koti za kikatiba. Katika hii Katiba tunayoandika, tuwe na constitutional courts. Vile vile, Katiba hii ambayo tunayotengeza, hii ambayo tunaitengeza hatuijui. Au munaijua? Sasa hii tunayotengeza tunayoijua, tunataka ifundishwe makanisani, mashuleni iwe tu, katika kanisa, ipewe kifungo kidogo kama dakika 15 wananchi wafundishwe nini? Kanisa.

Vile vile katika Katiba hii ningeomba kuwe na kifungo kinasema lazima tuwe na kilimo cha kufa na kupona, cha lazima. To avoid mambo ya chakula ya msaada, imetufanya wavivu kabisa. Ama nasema urongo? Halafu chama tawala inapata kura saa zote.

President's powers to be trimmed. Zipunguzwe. Zimekuwa nyingi. Tumeona madhara yake. Hata mtu akisema anataka kuingia Ford People, anawekwa ndani kwa sababu ya nguvu tu. Kusiwe na mambo yale ya kushika watu ovyo ovyo. Mikutano, mtu akitaka mkutano, aende apige repoti lakini sio mpaka andikiwe kitu na polisi. Iwe tu umeenda kupiga repoti basi. Maanake imekuwa lazima uchukuwe kitu kidogo, uende usumbuliwe kama sisi wataita ni waoga sana. Ukitaka kitu mpaka unapiga kelele bila uwoga sana. Kwa hivyo ningetaka kitu hiyo iwe ni free. Watu wasisumbuliwe. Na kama nilivyosema, ikiwa yangu haitaingia, tukiwa na more political parties, tuwe na registrar of Political parties badala ya huyo mwingine Ombago, anatumia ofisi yake vibaya sana.

Ya mwisho kabisa, mkenya awe ni mkenya amezaliwa na baba na mama. Kwa vitabulisho kusiwe na vetting. Hii vetting imeleta shida. Watu wanakula kitu kidogo na hatutaki corruption iendelee kwa mambo haya. Watu wengi wamekosa vitambulisho, na wasomali hapa Taveta wanapata mbila shida. Hao hufanyiwa vetting na akina nani? Kwa hivyo ndugu zangu nashukuru kwamba Katiba hii ambayo tunayaunda ni ya majimbo, itatufaa sisi na ukoo wetu ambao unaokuja zama zijazo. Asanteni sana.

**Com. Tobiko**: Asante sana ndugu yangu. Kuna swali moja.

**Com. Prof. Kabira:** Umesema tuvunje political parties zote? Tuwe hatuna hata moja?

**Richard Mwangeka:** Ikiwa itakubalika, ndio maoni yangu.

**Com: Kabira:** Tutafanya elections kwa njia gani? Au unataka wawe independent candidates? Au unataka tuwe movement kama Uganda au nini?

**Richard Mwangeka:** Tuwe movement kama Uganda.

**Com. Tobiko:** Reverend Silvanus M M?

**Reverend Silvanus Makoma**: Majina ni Reverend Silvanus Makoma. Nataka nizungumzie kwanza juu ya retirees, wale ambao wamestaafu. Shida za wale wamestaafu. Imekuwa kwamba katika Katiba ya sasa, ile ambayo tunaandikisha ambayo tunarekebisha, imewezekana katika kipengele kimoja kuonyesha wazi wazi kwamba ni wale ambao wamestaafu na wanapata pension yao wawezeshwe, ili kila wakati zinapo-ongezeka, za wafanyi kazi wale wengine, basi kipengele hicho kiweko ili na zao ziwe zikiweza kuongezeka sababu wamewachwa kule kule ambapo walipata na maisha inaendelea kupanda na wangali pale pale. Kwa hivyo wale wame-retire wanakuwa wana shida.

Pili, hii pension scheme yatakikana ifanywe kwamba mtu anapo andikishwa kazi, na mara moja ile pension inaanza kukatwa. Lakini ilikuwa ni kwenda Nairobi, rudi, kuja, rudi, kuja. Iwekwe katika Katiba ya sasa kwamba mtu anapo-retire, wakati ambapo serikali inatumana ile barua ya retirement tayari department ya pesa zake zianze kuja badala ya kwanza kuendelea na mambo mengine,Nairobi, arudi DO, chief, hakuna hiyo. Maana walimwandika, walikuwa wanataka, hawakuwa wanauliza DO, chief, hawakuwa wakiuliza juu account ilikuwa inakatwa moja kwa moja. Basi, sasa mara moja anapo-retire siku ile ya mwisho tu, basi mwezi ule ukujao, aanze kupata hiyo retirement yake moja kwa moja. Iwekwe kwamba katika Katiba yule bibi yake awe ana uwezo wa kuendelea kupata kile kiwango kwa muda fulani atakapo kuwa mzee yule ameaga dunia.

Nikiingilia katika upande wa serikali, powers za Rais zipunguzwe. Ni nyingi, kiasi kwamba yeye ndiye kiongozi wa kile, yeye ndiyo kiongozi wa ile, yeye ndiye kiongozi wa pande ile, na tena kuna wakenya ambao wanaweza kufanya kazi zile tofauti tofauti. Zile powers zipunguzwe, wakenya wengine wachukue nafasi ile hivyo, lakini basi huyo Rais abaki ni ceremonial President.

Pili, kuweko na waziri mkuu ambaye watasaidiana zile nguvu zake zikipunguzwa. Katika Katiba yetu nisameheni nikiwa ninapanga hivyo, lakini katika Katiba yetu, kuweko na ile tunaita preamble kwamba ionyeshe Katiba ni ya akina nani? Ni ya

Kenya na wakenya wenyewe kuweza kudhibitika kabisa. Halafu pia katika hali hiyo ionyeshe uhuru na haki za wa kenya.

Pia katika hali ya kuabudu, tuweko na uhuru ambao umeendelea kuwako. Lakini kumekuwa na mushrooming churches. Sasa tuzibitiwe ziweko chache ambazo zitazo-ongoza roho za wanadamu wale wanadhibitika kumsikia mungu wao. Maana kuna wale wa kutaka kwenda mbinguni na kuna wale wanataka kubaki hapa. Basi wale wanaotaka kwenda kule kufika kule kwa Baba, basi wawekwe na uhuru huo. Serikali na Katiba utambue maana kuna tatizo hapa inalo tokea mara kwa mara. Tunapo zungumza mambo ya kuabudu, mimi sina mipaka. Waisilamu ndugu zangu, waendelee kuabudu vile walivyo na wakristo waendelee. Lakini Katiba ya sasa isijaribu kuweka mipaka kwamba kutakuwa na chief Kadhi ambaye ata-deal na mambo ya ki-isilamu, sawa basi, wakristo nao Katiba iwapatie nafasi wawe na wao. Sijui hizi mahakama zingine zitakuwa za akina nani? Wale ambao labda watakuwa sio either Wakristo ama waislamu basi wabaki na hizo. Maana tumeanza kujigawanya. Kwa hivyo Katiba iwe kwamba kama tutakuwa na hizo koti, ziwe za wakenya wote. Hakuna msingi wa ile ni religion fulani, tuwe na hiyo moja ili tuendelee kuwa pamoja, na kuishi pamoja.

Pia nitaunga mkono majimbo. Lakini nita unga mkono majimbo ya uchumi ili ile uchumi itakuwa, kile kina-chotoka, hapa, tuna mawe, tuna wanyama, tunataka pia tupate ardhi hapo, lakini uchumi unaotoka pale, 75% ibaki hapa. Commissioners wenzangu time sio zangu. Sorry lakini mimi ni member katika constituency ambayo tulikuwa tunapata shida. Naweza kuwa hata mimi ni mmoja wa commissioners huko. Lakini kitu kilichoko nyinyi mlipokuwa mnakuja na gari, maana nimekuja na mmoja wenu, amelalamika kwa sababu ya barabara. Lakini zote tunazopata zaenda Nairobi. Hakuna kitu twabakiziwa. Basi Katiba itegenezwe kiasi kwamba, 75% ibaki hapa ili ifaidi mwananchi wa hapa hapa.

Katika kipengele cha marriage, kuoana ni sawa sawa - waoane katika kanisa, waoane kwa DC waoane vile wataoana. Lakini ingawaje katika bibilia yetu haikubaliwi hii tunaita divorce. Lakini kuna shida na shida hii inakuja vipi? Mzee anaweza kutoroka ama aende miaka fulani aache yule bibi. Nasema kwa sababu walifunganishwa ndoa takatifu ama ile ya kwa DC, hawezi tena kukagamuka ama kupata mtu mwingine wa kumsaidia yule mama ama yule mzee hawezi kuoa kwa sababu alikuwa amesha funga ndoa. Basi Katiba nataka iwe hivi; ama maoni yangu iwekwe kiwango. Mama akitoroka akimaliza miaka 20, ile marriage certificate iweze kuwa revoked na huyu mzee aweze kuokoka. Kwa sababu ashatoroka, watoto wamekuwa wakubwa, mzee amebaki pale na ana taabu na kwa mzee na mama vivyo hivyo ili tukaweza kuwa na jamii yakusimama. Asanteni.

**Com. Tobiko:** Asante sana Reverend. John Ingura? Roy Mwakazi?

**John Ingura:** (absent)

**Roy Mwakazi**: Commissioners, wananchi wenzangu, ningetaka kutoa maoni isipokuwa nimetoa maoni jana. Lakini ukisikiliza sikiliza, unakumbuka mengine ambayo yame sahaulika.

Kuna kitu ambacho tunaita passport ambayo inaonekana tunatakiwa tuwe na kipengele cha kusema ya kwamba Mkenya yeyote ambaye ametosha kupata passport ikiwa anaihitaji, isichukuwe zaidi ya mwezi mmoja.

Na jambo la pili ambalo nataka kutoa ni kwamba kuna kitu kinacho-itwa blue book katika DDCs. Hizi DDCs ni za district na hapa utakuta katika district hii, wageni ndio wengi maana ina include Heads of Departments. Na utakuta ni wageni watupu ambao wanaketi katika zile DDC na watu wachache sana ambao wanatoka katika sehemu hii yetu. Kwa hivyo mambo mengi ambayo tunayafanyiwa kwa DDC ni kama tunafanyiwa na wageni ingawaje wabunge wetu huwa pia ni members lakini sioni kwamba kuna fairness katika mambo ya DDC. Tunataka yageuzwe ili iwe watu wengi zaidi tuweze kuwa na three quarters ya DDC iketiwe na wananchi wa pale pale ambapo tunatoka. Mimi nilikuwa na hayo machache tu. Asante sana.

**Com. Tobiko:** Asante sana. Jiandikishe pale. Livingstone Mwanduu? Apollo Mwamugunda?

**Apollo Mwamugunda:** Majina naitwa Apollo Mwamugunda. Ninamsalimu nyote kwa jina la Yesu. Mimi sina mengi sana. Ni watu ambao tuliandika Katiba yetu kule nyumbani, tukaandika barua. Tunataka isomwe.

**Com. Tobiko:** Sawa asante sana. Michael Madeo? Ameenda. Evanson Maduu?

**Evanson Maduu:** Kwa majina mimi ni Evanson Maduu. Maoni yangu ya kwanza ni kilabu. Maana ya Vilabu: Vilabu ina maana, maanake pombe ni lazima. Hata ufanye nini,
pombe haiwezi isha. Kwa hivyo Katiba lazima ipendelea vilabu vyenye afya maanake mwingine anakunywa ile pombe ndio inam-keep busy. Lakini siku hizi ile muratina kila mtu anakoroga kivyake. Kwa hivyo naona ikiwezekana, official clubs zifunguliwe na time ya kunywa ijulikane. Haiwezi kuwa club bila wale wazee wanao zikunywa, kwa hivyo, wameenda wametuachia bila ufundi na bila kuhalalisha vilabu, pombe ya muratina haiwezi kwisha. Kwa hivyo, naomba zirudishwe.

Ya pili, yangu ni mbili tu. Ya pili, mbeleni watoto wa kike wakipata mimba, walikuwa kuna kitu taita wanaita "***koora***" yaluni kuondolewa. Yaani wanapewa garama kutoa na tena yule ambaye amemharibu yule mtoto amchukue yule mtoto amlee, amsomeshe skuli mpaka awe miaka 18. Lakini siku hizi hakuna. Maana ya hiyo nitaeleza. Maana hiyo, mimi nina uwezo wa kulea huyo mtoto babu amezaliwa. Kuna mwingine hana uwezo ndio naona wanakuwa wana randa randa. Yaani hiyo kitu mfikirie. Yangu imeishia pale.

**Com. Tobiko:** Asante sana mzee. Neebert Hituuka?

**Neebert Hituka**: Commissioners, wananchi mlioko, hapa mimi nimeyasikia mengi na yangu nimeyapunguza.

**Com. Tobiko:** Rudia jina lako.

**Neebert Hituka Ingila:** Nimesikia mengi na yangu tu ni kuunga mkono. Utawala ni wa majimbo. Hapo nimemaliza. Mipaka iheshimiwe. Mali ya asli tuliyo nayo hapa vile vile,hii kitu lazima iheshimiwe. Si kwamba mali yetu inakwenda hivi hivi.

Kitu kingine ni mishahara ya wabunge. Sisi jamani, nchi ni maskini. Tunalia umaskini lakini mishahara ya wabunge hata siwezi kusema. Hii mishahara ipunguzwe maana na wao ni wananchi wa kawaida, wanakula ugali kama sisi. Nyumba na mashamba tunalima na wawa hawa. Kwa nini wale mishara zaidi ya watu wengine? Mishahara ya wabunge ipunguzwe kulingana na hali yetu.

Habari ya pori imezungumzwa sana. Mimi sitaki kuongea zaidi ya hapo juu ya pori. Pori iko lakini sasa sisi wananchi hata kama mtu yuko usingizini, hawezi kujua jamani sisi tuna- rithi theluthi moja one third na wanyama two thirds. Sasa hata hii ni kitu ya kuzungumzwa? Ni kitu ya kuona kwamba hawa watu wamefinywa.

OK. Hapa kuna mambo yametajwa jinsi vile wanyama wanavyofanya. Kuua watu, kuharibu mashamba; hii tumeyaona, eti unalipwa Kshs.30,000. Maisha imepotea. Ile familia, Itafanya nini? Ni kwa nini hawa wanyama wafugwe wengi namna hiyo? Huyu mtu ambaye anataka kuja kuona ndovu kwani hata akiona ndovu ishirini si ndovu ni wale wale? Ndovu wanafugwa kupita kiasi. Hata wanakufa na njaa.

**Com. Tobiko:** Sasa pendekezo lako kwa hilo ni gani?

**Mr Neebert Hituka:** Pendekezo ni wale wanyama wapunguzwe. (laughing and clapping) Wabaki wa kiasi. Wasichana wanapata mimba, adhabu imepunguzwa ndio mambo imekuwa holela holela. Wasichana wetu wanawekwa miiba ovyo ovyo kwa sababu hakuna sheria yoyote. Mbeleni, kulikuwa na sheria ukimdunga msichana mimba, lazima uketishwe. Na tena mpaka siku ya kujifungua ndiposa kufanywa kwa sababu ile mimba, either anaweza kufa wakati wa kujifungua. Kwa hivyo, wataita waliichukua ni jambo serious kabisa. Mpaka ajifungue ndipo sasa mzungumze. Na akifa, utalipa rithaa ya yule msichana maana ni wewe ulimdunga mimba. Lakini, kwa sababu sheria hizo zimelegeshwa, hakuna basi mambo hii inakuwa ni holela holela. Mayatima wamejaa.

**Com. Tobiko:** Pendekezo lako kwa hio ni gani mzee? Hilo jambo la wasichana kudungwa mimba?

**Neebert Hituka:** Adhabu ziongezwe kwa wanao weka mimba. Maana kuna sheria ukisha- dunga mimba.

Halafu mayatima, mimi sijui nitazungumza aje. Kuna watu walioko hapa wanaopata bursary na mayatima hata hajui iko namna gani. Yule yule mwenye uwezo ndio yeye anaye pata bursary. Hapa, hakuna haki.

Kuna lingine. Nataka shule zirudi kwa usimamizi wa missions. Maana sasa munasema shule ni za serikali. Sasa inakuwa walimu hawajali, watoto hawajali. Imekuwa migomo mara kwa mara, kuchomana, na kufanya nini, kwa sababu imekuwa ni government schools. Zirudi kwa mission, watoto wafundishwe adabu na mission, wafundishwe dini.

Nikimalizia mimi, kuna upungufu wa kazi. Lakini tutaipunguzaaje ikiwa mtu mmoja atakuwa na kazi tano? Kazi moja kwa mtu mmoja. Kama wewe ni mwalimu, mwalimu full stop. Kama wewe ni mbunge, mbunge basi. Hapana mbunge, chairman wa hii na hii, mtu huyu huyu mmoja na wengine wana kufa hapa hawana kazi. Kazi kwa mtu mmoja. Kama haikutoshi, basi shika lako. **(laughing)**

Utawala, utawala, mimi ninaona afadhali machifu wachaguliwe na wananchi. Hapana kuletewa chifu chifu tu. Achaguliwe na wananchi. Nimemaliza.

**Com. Tobiko:** Asante sana. Hon. Mwakilingo.

**Honourable Mwakilingo:** Mimi nilizungumza jana Voi kwa hivyo ni kuongezea tu. Ni yale ambayo labda yamezuka wakati wenzangu walipokuwa wakizungumza hapa. Kwa ufupi tu, jana nilikuwa nimezungumza jana kwamba yeyote yule ambayo atataka diwani, mjumbe au Rais, ni mtu lazima awe na familia ambayo imesimama. Tusiongozwe na watu (**taita dialect)**. Hiyo ndiyo niliyo zungumzia jana maanake hata vitabu vya Mungu vyote vinatwambia kiongozi yeyote yule awae lazima awe na nyumba kamili.

Nikazungumzia mambo ya ardhi, nikizungumzia mambo hayo mnayosema ya ma-chiefs, nikazungumzia uhuru wa siasa, na leo tu nataka niongeze kwamba stakabadhi za kumilki ardhi, ikiwa zimetolewa na ije ijulikane baadaye kwamba ardhi hio ina mzozo ambayo ni lazima usuluhishwe waziri awae ni wa ardhi awe na uwezo wa kufutilia mbali stakabadhi hio mpaka mambo hayo yasuluhishwe. Kwa sababu tumeona bunge, utasikia waziri anasema "Ndio, hiyo ilikuwa ni road reserve, ilikuwa ndiyo ni shamba la fulani, na title deed imetolewa kwa bahati mbaya lakini sina uwezo wa kuifutilia mbali". So, tunasema kwamba ifutiliwe mbali wakati wa mambo hayo mpaka isuluhishwe. Awe na uwezo huo wa kufutilia hiyo title deed. Lakina niogezee kwamba tunapo-zungumzia mambo ya majimbo, utawala wa ki mikoa, nini na nini, ni sawa. Nimeenda nchi za nje tangu mwaka jana na hata mwaka huu, utakuta hizo ziko. Lakini kitu ambacho pia ni lazima tusisitize ni kwamba ni jukumu la serikali na Katiba iseme hio kwamba serikali ihakikishe kuna vuuo vikuu viwili, at least 2 universities katika kila mkoa. Maanake hatuja gawanya rasilmali. **(taita dialect).**

Hii ya hapa Taita Teachers Training College, mimi ndiyo napigana vita na hio mpaka sasa na nitapambana na hayo mpaka dakika ya mwisho. Hayo ni lazima yatimizwe tuwe na vyuo vikuu at least viwili katika kila mkoa.

Mambo ya vyama vya kisiasa kwangu mimi ningeona twende njia ya uingereza au America. Ambapo tuwe na maoni kabla ya uchaguzi. Kama vyama ni arubaine na viwili, tuvipigie kura mapema. Ni vingapi na tuseme ni vile vya kwanza vitano ambavyo vitakuwa vimepata kura ndivyo hivyo vitasimama hapo. Maana vingine vimeenda mpaka vikakuwa ni vya kiukoo. Vipigiwe ile inaitwa kwa kingereza "opinion poll". Tujue sasa vile tano vya kwanza ndivyo hivyo candidate yule ambaye anataka kusimama, asimame na vile vitano kwa sababu ndivyo vinaonekana vina nguvu. Ndio twende na hivyo maana saa zingine tuna changanyikiwa. Unapatiwa list hapo, unakuta Mwakilingo arubaine na wawili, sasa unashindwa kwa sababu kuna alama ya sungura, mwingine ni unga, mwingine ni vidole viwili, mwingine ni mtoto, hujui kama ni wa devil worship. Sasa unashindwa upigie nani? Lakini ningeomba tu Katiba ionyeshe kwamba tupige kura mapema hasa miezi 6 kabla ya wakati wa kura, ndio tujue ni vyama vingapi ambavyo vitasimama kupigania siasa.

Tumezungumza mambo mengi. Uwezo wa Rais upunguzwe na hasa mimi ninazungumza ule wa kuunda zile wilaya za kisiasa. Utaona Mwakiringo anakuja hapa kwa sababu yeye ni KANU damu na sijui ile damu yake ilitoka wapi anasema "tunaka Voi ipatiwe wilaya." Sawa utapatiwa wilaya lakini hujajua garama zake – DO lazima awe pale, DC awe pale na maofisa wote. Na huku tunataka tufufue uchumi. Serikali inapopunguza wengine, huku Rais amesema Voi ipatiwe District – tena lazima tuajiri watu wengine. Kuna mwelekeo tunaelekea kweli hapo? So, we are saying political Districts should be gotten rid of unless umepitishwa na bunge . Lakini kama hivi sasa, saa hii mwenzetu mmoja amepeleka serikali kotini kwa kuunda wilaya ishirini na nane kwa baraza bila idhini ya bunge. Mlikuja mkaomba Mwambiro. Mwambiro sasa saa hii watu wa mngongonyi hawajui ako Voi au ako mwatate. Sasa unashindwa uko wapi? Mimi mwenyewe Madoka kwenda kwake Mngongonyi hawezi. Mimi mngongonyi, maana sijui ni kwangu si kwangu. So hivyo ndivyo creation ya tarafa za kisiasa ambazo hazina mbele wala nyuma na hii imedhihisha mwongozo ulioko maana tumekuwa watu wa kutingisha kwa muda mrefu zaidi hiyo mambo ya KANU. Tuseme kwamba, serikali ikiwa ina fedha ihudumie wale watu wote wako miaka 65 kwenda mbele wapatiwe pension ya bure. Whether alikuwa anafanya kazi ama hafanyi kazi. Ukihitimu miaka 65, uanze kupatiwa fedha na serikali za kukuweka mpaka umalizike. So hiyo iingie (clapping). Maanake tulipokua uingereza juzi tukichunguza au observing upigaji kura wa huko, utakuta kwamba wazee wa miaka 65 wanapatiwa hiyo pension bure, wana nyumba za bure wamejengewa na huduma za hospitali za bure. Hapa kwetu, watu wengi wanakufa kwa sababu hamna huduma. Miaka 65 unaambiwa unatakikana uende pia ufanye cost sharing. Mpaka lini? Tunasema hizo ziondolewe , na wapatiwe huduma kama hizo bure umehitimu miaka 65.

Na mwisho ningemalizia kwamba elimu ile ya zamani irudishwe. Hii ya 8-4-4 ifutiliwe mbali. Tatizo ni kwamba, tangu mfumo huu wa elimu mpya ulipokuja wa 8-4-4 ni kwamba tumeanza kupeleka watoto vyuo vikuu ambao hawajakomaa, ndio wameanza kuleta tatizo la migomo kila wakati. Lakini wakati ule ulikuwa ukimaliza kidato cha nne unaenda cha 5 mpaka cha 6. Kitambo uingie university umekomaa ki-akili. Kwa hivyo, unaona mambo mengine ni ya kijinga kuyafanya **(taita dialect)** na hii nadhani ndio imeanza kuleta matatizo haya . So nina imani kwamba hayo ambayo tunayatoa maoni, mtarudi nyuma vile ilivyo katika sheria ya tume hii, tuone kwamba yale ambayo tumeandika pia tutakuja tuyasome na pale ambapo hayajaingishwa, mengine yaingie. Kwa hivyo unaposema mambo nina washukuru **(taita dialect)** kanyanga vile iko wasikie

hao. **(taita dialect).** Bwana asifiwe.

**Com. Tobiko:** Asante sana Mheshimiwa. Sijui ndugu yangu, jiandikishe pale. Josiah Mwaiboro? G Nyange?

**Gregory Nyange:** Mimi kwa majina yangu naitwa Gregory Nyange. Maoni yangu ni kama vile wengine wametoa kuhusiana na mambo ya pombe. Mimi maombi yangu na sisitiza kama pombe haitakubaliwa, pombe zote ambazo zinatoka nje zifungwe, hata mabaa ikiwezekana brewery zifungwe. Lakini kama itakubalika pombe ya kienyeji irudishwe irudishwe ili itatuondolea mambo yale tunaona yanafanyika siku hizi.

Ya pili, tumesikia mambo ya national park. Kuna skuli imejengwa hapo Manyani, mahali kunaitwa Tsavo. Tumeona vijana wetu wamesoma, wengine wamefika form 4. Lakini siku ile ilitangazwa waende wakafanye ile interview, waliwachwa, wakachukuliwa watu wa kutoka sehemu zingine peke yake. Kuonyesha kama sisi hiyo elimu hatuna, na elimu tunayo. Kwa hivyo, ule msemo unasemekana wa kitu kidogo, maoni yangu naona ndio inafanyika. Wengine wanaambiwa eti ni wafupi na wamefika futi tano na labda inch nane lakini atasemekana yeye ni mfupi. Wanachukuwa watu wale warefu warefu. Kama vile pia polisi wanafanya. Lakini ukienda ukiona sehemu zingine utakuta polisi ni mfupi hata mimi ni mrefu kidogo. Hiyo inafanyika kwa nini? Kwa hivyo maoni yangu ni kwamba, kama ni ki—elimu, hata mtu akiwa 5 ft, aandikwe kama anataka kazi ya polisi. Ama hiyo kazi za National Park ikitokea, isiwe ubaguzi wa kusema ati huyu mtu ni mfupi, hana kifua kikubwa, na ukiona wale polisi wengine utakuta hata mimi kifua changu ni kikubwa kidogo. Kwa hivyo tunaona hio mambo, Taita ni kama tuseme tunaonewa. Kwa hivyo yangu ni hayo.

**Com. Tobiko:** Asante sana. Kijana jiandikishe. Mwalimu Mganga?

**Mwalimu Mganga:** Nimemsalimia kwa jina la Bwana. Basi mimi naitwa Mwalimu Mganga. Mimi ni mtaita wa hapa. Basi mchango wangu vile ambavyo Katiba imekuja kwetu, tunataka tuseme ule ukweli uliopo.

Kwanza hapa vile mnavyoona kitambo tukae hapa taabu ilioko ni wazee wa vijiji. Wanatumika kama wajinga. Sababu mzee wa kijiji yuko nyuma ya sub chief lakini hakuna kitu chochote anapata. Ni mhangaiko tu. Wewe unatoka shughuli yako, umeshinda unachunga au unatoka shambani umechoka, unakuta barua inatoka kwa sub chief. Unatakiwa kesho kwa mkutano wa DC au wa chief na umechoka na unaambiwa sasa upige firimbi kesho, watu wanatakiwa kwa mkutano. Hakuna torch, huna chochote na ni jioni, ni usiku. Wengine ni wazee kama sisi huoni. Ukilala hujapiga firimbi, kesho watu wale wanatakiwa kwenda kwa mkutano, hawafiki. Wewe unatoka kupiga firimbi asubuhi, wengine wameshatoka wameenda mashambani. Wewe unaondoka asubuhi unapiga firimbi kwa sababu hakuna tochi, hakuna chochote . Anasema "haa! hii kazi kwani ni ya kulipwa hii, usiku nani anaweza kuzunguka namna hii? Na sina torch nitaenda nikiumia bure? Sina chochote …" Basi inarudisha maendeleo nyuma. Ya pili …

**Com. Tobiko:** Sasa pendekezo llako kwa hio ni gani?

**Mwalimu Mganga:** Tunataka anakosana na bibi yake usiku, wewe unakuja kuitwa uende usululishe hayo maneno.

**Com. Tobiko:** **T**unakuelewa. Haya nenda mbele.

**Mwalimu Mganga**: Uende usuluhishe hayo maneno. Na ni kazi mbaya ukienda kuamua unasikia. "Huyu mtu anakuja kuamua maneno yangu na bibi yangu." Unaulizwa, "Wewe uliona … Unakuja kwa mzee wa kijiji naye akuelezee ndio upeleke hio maneno kwa sub chief. Halafu ndio iingie kwa chief. Hiyo ni kazi ambayo inafaa hata kupewa mshahara.

**Com. Tobiko:** Tumekuelewa kabisa. Tumeandika, enda kwa point nyingine. Asante sana.

**Mwalimu Mganga**: Sasa, hapa kwetu Taita, sisi tuna pori kubwa sana ambapo hata serikali ikisema kwamba hawa watoto hawana kazi walete wanawafadhili hii pori yote wajenge machine zingine kama zozote za kazi, watoto wetu watapata kazi. Tume somesha watoto., wako hapa wanamanga manga tu. Hawana kazi na pori yetu iko kubwa ambapo wanaweza kutujengea, wafadhili wakaijenga hata machine zozote ambazo zina weza kusaidia watu. Ndovu anakula chakula chetu. Hata ukishinda shambani huwezi kula papai. Yameliwa na ndovu. Mihogo inango'lewa na ndovu.

**Com. Tobiko:** Pendekezo ni gani?

**Mwalimu Mganga:** Pendekezo ni hao ndovu tupewe ruhusa kama zamani zikiingia kwa shamba, ikiuawa, moja zinaweza maliza hata mwaka hazikanyagi hapa. Ikisha uawa moja ikinuka wenzio hawatarudi mwaka. Lakini siku hizi ukiua moja hata wanakomputa wana angalia ndovu ameuliwa pahali fulani. Kesho unakuja kuchukuliwa, unaenda kufungwa. Ngo'mbe wetu wakiruka huko chini, unashikwa unapigwa hata mengine, watu wanafanywa vibaya sana, yale mambo mabaya sana. Hata si ya kusema hapa mbele ya watu. Hii serikali yetu iangalie mambo kama hayo. Ambayo ile mateso yako hapa kwa wataita.

Ya tatu, sisi hapa tuna mali nyingi sana, Taita hii, ambayo serikali ikitusaidia vile tunaweza kusema tunaweza kuwa tajiri. Mashamba haya yanaweza kuwa tajiri sana mpaka ndii. Maana wakati mvua ina nyesha, maji yanatiririka bure yanaingia kwa mchanga na serikali tunasikia ina pesa nyingi. Kwa nini haiwezi kutoa milioni fulani hivi wakajengea watu dam kubwa. Wakati mvua inanyesha upande wa chini matangi yajengwe, kila mtu ajenge tangi lake shambani kwake. Mvua ikinyesha, yale maji yanaenda yainaingia kwako, kwa fulani, kwa fulani kila shamba. Kama hivi sasa, si unaona mahindi inakauka. Saa hii ndiyo wewe una tangi lako, unalima. Hata njaa inakwisha. Ni uwezo sisi tinakosa ndio tunaumia na njaa. Kwa hivyo, serikali iangalie mpango kama hiyo ya wananchi wake. Kwa hivyo asanteni, yangu ni hayo.

**Com. Tobiko:** Asante sana. Jiandikishe hapa. Lucas Mwadema?

**Lucas Mwadema:** Commissioners mabibi na mabwana . Kwa majina mimi ni Lucas Wamugunda Mwadema. Kwanza napenda nimshukuru kwa siku ya leo. Tumesikia mengi ambayo yamezungumzwa na wale ambao wametangulia. Lakini hata hivyo, ningelipenda pia nichangie au niongezee kidogo. Hapa tunapo simama leo nafikiri ni miaka 39 toka tumejinyakulia uhuru wetu. Tukipiga mahesabu, ki maendeleo tukilinganisha maendeleo yale yamefanyika katika mkoa wa pwani na mikoa mingine, tukiangalia katika asilimia, tutaona ya kwamba watu wa mkoa huu, sisi tumepata hasara. Katika kuchambua chambua mambo haya na kuona vile faida imeingia pahali pengine na vile hasara imeingia mahali pengine kwa wakati ule mmoja, itatubidi tuongee mambo fulani wakati huu tumepata nafasi kama hii. Na inanipendeza mno kusimama mahali hapa ili niseme machache ijapokuwa nilikuwa na mengi niseme lakini yamesemwa.

Katika sehemu ya Taita Taveta, katika mkoa wote wa pwani, sisi tumesha pata hasara kweli kweli. Na niki kumbuka wakati tulikuwa tunapata uhuru mwaka wa 1963, nilikuwa kijana mdogo mwerevu, nilikuwa nasikia. Nikasikia yakizungumzwa mambo ya vyama vilikuwa viwili. Kile kinachotawala sasa na chama kile kingine kilivunjwa vunjwa baada ya mapatano fulani kufanywa. Katika akili yangu nafikiria kwamba, kulikuwa research fulani ili kuwa inafanywa baada ya kuunganisha hivi vyama vyao kutatokea nini baadaye. Na katika uchunguzi huo, mimi naona kana kwamba, wakati tunaongea sasa, nashukuru wazee wengine wako hapa ambao walikuweko wakati huo, wameona yale yalisababisha viungane, halikuzaa yale matunda ambayo walikuwa wanatarajia wakiungana itakuwa ki namna gani. Namaanisha kusema ya kwamba mfumo huu ambao uko sasa sio mzuri. Ningelipendelea mfumo wa majimbo. Kupendelea mfumo huu ni kwamba, wale ambao wako katika mkoa huo, kutakuwa na mpango ulio maalum ambapo kutakuwa wale ambao wako katika mkoa ule, watakuwa na wabunge wao ambao watapewa mamlaka hata akiwa waziri mkuu wa mkoa huo ambaye atakuwa akichukuwa maoni ya wale na akitambua xasilmali na mambo yote yale ambayo atapata kwa manufaa yao ili apeleke katika ile serikali kuu. Katika hali hii, itamanisha ya kwamba mambo yata balance. Nimesababika niseme hivyo Commissioner, kwa sababu katika mkoa wa pwani tukiangalia, utakuta ndio kuna hii mambo ya kuanzisha mambo hii ya ma-squatters. Unasikia sijui ni Mpeketoni, sijui ni Bura, sijui ni Taveta, zina-anzishwa. Kuna siasa hapa ya kusema mtu ana uhuru wa kuishi mahali popote anapotaka. Lakini katika kuangalia kwangu, na wengine wale ambao wa udaku wa kudokoa dokoa kama mimi, mimi nasema ya kwamba, ningependa niseme Mkoa wa pwani ndiko watu wanaweza kuishi wote. Hapo ndipo watu wote wanaweza kuishi. Lakini tukiangalia mikoa mingine,huwezi kuta watu wengine wanaishi hapo. Hakuna.

**Com. Tobiko:** Pendekezo lako kwa hiyo ni gani?

**Lucas Mwadema:** Nilikuwa nasema namna hii, namaanisha kusema ya kwamba, mimi napendekeza ya kwamba tuwe na serikali ya majimbo, ambapo kutakuwa na mpangililo, watu watakuwa na ruhusa ya kusema hili hatutaki na hili tunataka. Watakuwa wakiwa na kura ya maono, wao wenyewe waseme, “Je hapa, hii national park, kwa nini inachukua sehemu yote?” Nimetembea sehemu za Ukambani National Park ni kidogo sana. Umaasai, National Park ni kidogo sana. Taita nzima national park. Pesa hawapati. Basi katika mpango huo tutaona ya kwamba watu wa mkoa wa pwani watakuwa na njama

moja wakizungumza jambo hilo na wakiamua, wenyewe wakishirikiana na ule upande mwingine. Simaanishi kusema ya kwamba hakutakuwa ushirikiano. Ushirikiano utakuweko .

Jambo lingine ningependa niseme ni kwamba, shuleni katika Katiba hii ambayo tunapendekeza mapendekezo yetu ni kwamba juzi juzi tulisikia kiboko kiondolewe shuleni, mimi maoni yangu ningeliona ya kwamba kiboko kirudishwe shuleni. Kwa sababu kiboko kiko hapa kwa bibilia. Ya kwamba usipo mchapa mtoto basi hawezi kuwa mkamilifu kabisa. Kwa vile mengi yamesemwa ningelipenda kusema tena nipendekeze hivi. Kuna watu ambao wanaumia wakiwa kazini . Mtu ameumia, amevunjika mguu, amekuwa mlemavu kabisa, na hatafanya kazi kamwe kwa maisha yake. Huyu mtu awe akipewa kiwango fulani cha pesa, pension kama shillingi elfu tano kiasi kadri atakapoishi . Na hapo kama ameondoka pia kwa bahati mbaya, basi bibi yake naye aendelee kufanyiwa vivyo hivyo.

Mambo ya national park yamezungumzwa sana sitaki niyarudie na ningalipenda niseme ya kwamba, mpaka wa Taita Taveta ulikuweko zamani, ule wa kwanza kabisa, ulikuwa umetupakanisha na wale wakamba urudishwe. Kama ulikuwa umefika Taru, urudishwe, kama ni wapi, urudishwe pale pale huo mpaka. Kitu kingine ningelipenda niseme ni kwamba watoto ambao wamebahatika kuwa na bahati mbaya, wazazi wote wawili wamekufa, basi wapewe free education katika secondary level. Wasome hadi kumaliza na kama wanaenda university, pia wapewe nafasi kama hiyo. Vitu vimepanda bei sana na nafikiri kila mara tukiuliza bei, tunaambiwa ya kwamba ni kodi. Ingelifaa katika Katiba hii kupitishwe kiwango maluum ambacho kama inasemekana mimi nilipe Kshs.300.00 na nikilipa hiyo Kshs.300. Basi imefikia hiyo ni kodi yangu hio. Nikilipa kwa mwaka KShs.300 basi, kama vile ilikuwako mbeleni. Badala ya kuingizwa katika vyakula namna hii, basi ina pandisha bei ya vyakula, tunaambiwa hii ni kwa sababu ya kodi. Soda inakuwa ni shilingi hamsini tuna ambiwa ni kodi. Sukari inakuwa ni shillingi mia moja, ni kodi. Kodi iwe na a certain limit yaani kiwango fulani ambacho itakuwa ni easy to calculate 25 million times that. Serikali itajua imepata pesa kiwango gani kwa mwaka.

Kiwango kingine, ningelipenda niseme, nashukuru mwingine ameguza mambo ya mshahara wa wabunge. Hiyo sipendi niongezee sana lakini kwa kweli tukiangalia hapo kuna hatari. Danger hio. Tunataka huo mshahara wa wabunge uangaliwe. Tuseme kwa mfano umenipa nafasi mimi nijipakulie pilau mimi mwenyewe. Bila shaka yangu nitajaza mpaka ianguke upande huo mwingine na ya mwenzangu nimkatie kidogo kidogo hapo. Basi wale jamaa wasijipangie mambo yao wenyewe. Kuwe na chombo fulani ambacho kita angalia vile mambo ya wabunge yataenda. Wasiwe wanapanga mambo yao yote wao wenyewe na kupitisha wao wenyewe, hiyo itakuwa sio vizuri .

Jambo la mwisho kabisa ningalisema hivi., hizi Non Governmental Organizations (NGOs), katika nchi yetu kuna NGOs nyingi. Taita tuko na ma-NGOs wengi wanatumwa lakini tukiangalia ile faida inapatikana katika ‘grass root’, katika village level, maendeleo yale yana fanyika ni machache sana. Ningependa niseme ya kwamba, baada ya NGOs kukubaliwa kufanya miradi fulani katika sehemu fulani, sub DDC ihusishwe. Sub-locational DDC ihusishwe pamoja na ile locational kusikiza, kupanga na ku amua na kupitisha ni miradi gani ambayo wangependa na jia gani zingelipenda ziwe zikifanyika. Ningelipenda niseme ni

asante kwa nafasi hii. Asanteni.

**Com. Tobiko:** Asante sana. Jiandikishe upande huu. Agnes Mwashumbe? Gilton Kiringo?

**Gilton Karingo:** Bwana asifiwe. Basi vile munajua kabisa ya kwamba sisi ni watumishi wa kanisa, basi nilikuwa nikiona ya kwamba, labda nitakuwa nimekaribisha watu halafu nisikie watazungumza nini, halafu ndio tuone mambo yako namna gani. Kama ningekuwa nimejua ya kwamba watu huenda labda katiika taarifa wakaziwacha, basi ningependelea hil, lisomwe baadaye. Lakini kwa wakati huu kwa kuwa nimepewa nafasi kidogo, nasema ya kwamba …

**Com. Tobiko:** Taja jina lako kwanza mzee.

**Newton Karingo:** Jina langu ni Reverend Captain Gilton Karingo. Basi, mimi hupenda kusema hayo mambo ambayo huwa nagongana nayo kila siku. Lakini nikiwa nasikia kutoka kwa mtu mwingine, basi mimi hupendelea yule mtu ambaye anayaona heri ajisemee mwenyewe. Lakini mimi kwa upande wangu, yale huwa nagongana nayo kila siku ambayo ninaona kwamba yanakuja upande wa serikali, nimekutana na mambo hayokama mara tatu hivi. Yaani ni kuhusu hii bendera ya taifa letu la Kenya. Bendera hii, huwa inanipa shida mara nyingine kwa sababu, mara nyingine huwa napita nikienda shughuli zangu zingine halafu firimbi inapigwa. Firimbi inapigwa, nami mawazo yangu hayajaingia akilini yakuwa bendera ikiwa inashushwa ama inapigiwa firimbi mtu asimame afanye nini. Basi huwa mara nyingine ninaendelea na safari zangu. Nilikutana na mambo hayo siku moja, inapigwa na mimi ninakimbia mbio sana kama mtoto wa shule. Nimechelewa kwa ibada fulani. Firimbi ilipigwa kama mara tatu. Ndio nikaja kugundua kumbe huenda ikawa ni mimi ninapigiwa firimbi ama vipi? Na nilikuwa napitia katika kituo cha chief. Ilinibidi nisimame lakini mahali nilienda kusimamia ni kwenye kichaka sasa. Wao wako huko na mimi niko kwa kichaka. Nilikuja kumbuka nikiwa kwa kichaka. Lakini wale watu tulikuwa tunajuana wakanza kucheka. Wakacheka sana . Nikafikiria kwamba huenda ikawa ni mimi wanacheka .Maanake kwa nini nimekimbia nikaenda kujificha kwenye vichaka bendera ikiteremshwa.Lakini nilikuja kukumbuka baadaye ya kwamba kumbe ni bendera ilikuwa inapandishwa.

**Com. Tobiko:** Reverend. Sasa kwa hiyo yote, unapendekeza nini?

**Gilton Karingo:** Napendekeza hivi, kuwe na msimamo au maelezo bendera inasimamiwa kwa sababu gani? Mimi nachukulia kama ni kitambaa kinasimamishwa pale, kwa hivyo ikiwa ni wakati wa kuteremshwa, kiteremshwe tu, hakuna shida. Hasa mimi hushangaa ni kwa sababu gani nisimame?

Lingine ni hili, mimi kama mtumishi wa kanisa hupenda kusema ukweli. Unaweza ukaenda mahali pengine ukakuta jambo limetendeka. Kama mtu ameuawa pahali fulani. Sasa ameuawa. Hukujua kabisa. Huenda ikawa wengine wameona lakini wakafanya nini? Wakanyamaza. Lakini wewe kama mtumishi unaenda kuwaambia kwamba umekuta mtu ameuawa pahali fulani. Kwenda kuripoti pale , mara ya kwanza unachukuliwa kama shahidi, sijui namba 1. Lakini baadaye inakuja kugeuzwa.

Wewe si shahidi namba 1, wewe ni suspect number 1. Sasa shahidi atakuwaje tena awe ni suspect namba 1. Hawa polisi wanatakikana nao waangalie wajue ushahidi umetolewa kivipi. Nisije nikawa usichukuliwe hatua ya aina hiyo na uliona tu. Ndiyo nilikuwa nashangaa kama hizo ni sheria za kikoloni, basi heri zirekebishwe kwa zile njia watu wataona ni sawa. Maanake mimi…

Tena lingine ni kwamba, yaani hio ni sehemu ya tatu, Katiba inapotungwa, wale waliotunga huenda ikawa walishika biblia , ndio maana nikabeba yangu sasa. Na mkiangalia ukisoma mlango wa Matayo 5 mpaka wa 7, utaona sheria za Mungu vile alivyoziweka. Ni za kulinda nchi hii pamoja na binguni. Maanake ombi letu mambo yote duniani yanatoka binguni. Ndio tunasema hata uongozi unatoka mbinguni. Kwa hivyo tuwe na heshima ya viongozi wetu. Sasa nasema tunataka Katiba ilekebishwe kisasa kulingana na hali ilivyo sasa. Napendekeza Katiba irekebishwe kulingana na hali vile ilivyo sasa. Basi naomba ya kwamba kama Katiba itatungwa, wazingatie bibilia ama vitabu vya dini ile inayojulikana ni dini ya aina gani. Lakini iwe mwongozo. Msaada tunayopatiwa ya kuwasaidia ifikie watu yanahitaji. Kama msaada ni wakuja na kulipwa usije. Msaada ukitumwa hufikii maskini.\ikiwa ni mahindi yanatumwa haifikii yule ana shida sana. Basi nasema kama msaada unapokuja usianze kugawanywa huko juu juu. Na kama hutafikia wale wanaohusika, basi usije kabisa. Basi yangu ni haya. Bwana asifiwe.

**Com. Tobiko:** Asante sana. Jiandikishe pale. Rodah Mwaiboro? Elias Mwanjama?

**Elias Mwajama:** Kwa majina ni Elias Mwajama. Katika kurekebisha Katiba ningependekeza ofisi ya usajili, yaani Registrar of Persons ipunguze muda wa kuhangaisha vijana hasa wakati wanapotaka kuchukua vitambulisho.

Urithi: Nikizungumzia mambo ya urithi, hapa namaanisha ya kwamba wazee kwa wakati huu na hiyo Katiba ambayo tunaandika leo waache kun'gan'gania ardhi. Muda tu unapofikia miaka 18 mtu agawiwe sehemu yake. Hali kadhalika, wazee tena wasichukue jukumu la kuuza ile ardhi ya urithi. Kwa mfano, labda yeye aliachiwa na babu yangu halafu yeye achukue jukumu bila kujadaliana na sisi ambao tumeshafikisha umri wa kuwa na urithi. Zaidi ya hayo, kuna haya mambo ya NGOs kuja na kukutana na wazee na kuomba ardhi ambapo watajenga ofisi zao. Ingawa NGOs zinakuja zikienda, haingekuwa vizuri waje wapatiwe ardhi na mzee wangu wajenge hizo ofisi kabla sijakaa chini na mzee wangu tukajadiliana.

Ndoa za kitamaduni: tunaona wakati huu ni mgumu ki-uchimu na inakuwa ni wakati mgumu sana kwa vijana kama sisi kuoa na kumudu hayo mahari ama kufunga hizo ndoa. Sasa nilikuwa napendekeza ndoa ya kitamaduni ifafanuliwe kwa undani hasa tukichukulia kuwe na kamati ambayo itazunguka Kenya nzima halafu kanuni zinazofuatwa katika ndoa za kitamaduni, ili kwamba tutakapozifuata kanuni hizo, tuwe hata tuna uwezo kupata hizo certificate. Kwa sababu tunaona siku hizi, maisha iyamekuwa mafupi na kama kweli mimi sikufunga harusi either hiyo ya customary ama hiyo ya kanisani, sijui ceremonial, or whatever inakuwa vigumu, labda vile nimemwacha nyuma, ku-claim urithi wa mali yangu kwa sababu hana cheti cha kuonyesha ya kwamba tulionana kirasmi.

Wakati huu tena tunapendakeza Rais, mamlaka yake yapunguzwe sana. Hiyo ni kusema ya kwamba hata kama Rais atakuweko, asiwe na uwezo wa kuvunja baraza au bunge. Ila amwachie Speaker nafasi hiyo. Na zaidi ya hayo, bunge letu liwe linajadiliana kwa wakati mrefu na wala sio masaa mawili ama manne na tena hata hivyo, hizo siku zao za kujadiliana ziongezwe, waachiwe hiyo Ijumaa ndio waje kukutana na wananchi.

Na hapa kuna uhuru wa kuabudu. Mimi ningependekeza kwamba, kuwe na tume ya kuchunguza madhehebu na makanisa ambazo zinataka kujiandikisha. Hiyo ni kusema kama kanisa linapotaka kuandikishwa, ichunguzwe kama wanatofautiana na zile zingine na kama hawaafikiani, lisiandikishwe kabisa. Kwa sababu jambo kama hili ndilo limeleta mvurugano kanisani na hata makanisa yamekuwa mengi mpaka watu wamechanganyakiwa.

Hapa Kenya tuna utamaduni wetu na maadili yetu. Mimi ningependekeza katika hiyo Katiba tunaandika leo, kufafanunuliwe ni nini sehemu za siri. Baadala ya kusema uchi, sehemu za siri. Kwa sababu siku hizi, ninaingilia kina mama ,akina dada zetu na mama zetu wanatushangaza kwa mavazi ambayo yanaweza kufanya mtu akatenda kitendo kiovu. Na zaidi ya hivyo, kama kutawezekana, kuwe na dressing code, wakati wa hadhara na wakati wa faragha, yaanai wakati wa jumuia na wakati wako kwa uchache. Hiyo ni kusema kwa mfano kikao kama hiki wavaliaje? Na iwe wakati kama ni wakati wa kuvaa vile wanataka kama ni usiku ama kuanzia saa 6.00 pm, ielezwe kabisa katika Katiba **.**

Ninatilia mkazo kuwa Mahakama iwe huru na kuwa uhuru ninamaanisha ya kwamba, hakimu mkuu asichaguliwe na Rais bali kuwe na kikao cha majaji ambao wamehitimu na wana ujuzi wa muda mrefu ambao kati yao hapo wanaweza kumchagua mwenye wanaona anaweza kuhudumu vizuri katika ofisi hiyo.

Vile vile, hata Mkuu wa sheria singependelea awe anachaguliwe na Rais kwa sababu saa zingine kuna urafiki hapo na Rais vile tunajua katiba ya saa hii, imemruhusu Rais kuwa juu ya sheria yaani hawezi shitakiwa. Sasa ningependekeza Rais awe anaweza hata kushitakiwa akiwa ofisini. Hapo hapo, kwenye nguvu za ofisi ya Rais, ningependekeza Baraza la mawaziri liteuliwe kulingana na ujuzi wa kazi wala sio urafiki. Kwa mfano, Engineer achukuwe mambo ya ujenzi wa barabara na shughuli zinginezo na kama ni hakimu, awe anaweza kuchukua jukumu katika mambo ya nje. Na vile vile, hao makatibu wakuu wachaguliwe kulingana na ujuzi wa kazi na wala si kwa vile wana uhusiano kidogo ama karibu na Rais.

Hapa nilikuwa nataka kuongea kidogo kuhusu mahari. Pendekezo langu kwa katiba hiyo tunaandika leo, ifafanue umuhimu wa mahari na kwa vile siku hizi tunaona mapenzi hayana mipaka unaona mtaita akimpenda mjaluo, na pia mjaluo akimpenda mkikuyu,ningependekeza ya kwamba kuwe na kiwango cha kupimia hayo mahari ili mwananchi wa kawaida aweze kumudu.

Tume ya uchaguzi: Kwa sasa tunaona tume ya uchaguzi ime finyiliwa kidogo. Tungependa hii tume ya uchaguzi iwe na nguvu kamili. Kwa mfano iwe na uwezo hata wa kutaja siku ya uchaguzi na wala jukumu hilo lisiwachiwe Rais. Vile vile, kila wakati

tunaona vijana wetu wamehitimu umri wa kujiandikisha kupiga kura. Ningependekeza kujiandikisha kuwe kwa kila siku na wala sio wakati ule umekaribia uchaguzi. Zaidi ya hivyo, ningependekeza Bunge lipatiwe hata nguvu za kumwondoa Rais mamlakani kupitia kwa kura ya kutokuwa na imani naye **(clapping).**

Uhusiano kati ya askari na mwananchi: Sisi tunaambiwa mara nyingine askari ni watumishi kwa wote lakini hii imegeuka sio hivyo Imekuwa sasa askari hutumia ule uwezo wake kwa kumshika mtu na kuanza kumtesa. Ningependekeza iwe mshukwa anapotiwa mbaroni asiteswe kwa njia yoyote ile. Kama hakukataa kushikwa, haku- resist arrest.

Haki za ki Binadamu: Mara nyingi katika majela zetu tunaona magerezani, tunaona wafungwa wanakula chakula kibaya, wanavaa nguo zingine ambazo haziwezi kusitiri uchi. Ningependekeza serikali yetu kwa hii Katiba ifafanunue mavazi yanayofaa mahabusu na vile vile kama wanadamu, wapate chakula ambacho kinaweza kuwafaa. Zaidi ya hayo, tunaona katika hali ya kuwekwa gerezani na ubinadamu uko na tunaona kwamba hisia za kimwili zipo. Ningependekeza kwamba, wale wafungwa ambao wana mabibi, siku ambapo bibi anamtembelea, aruhusiwe kuonana kimwili . Hii itapunguza maovu ya kijamii kama ushoga. Asanteni.

**Andrew Safari:** Mimi ndiye Andrew Safari Mwalimo mapendekezo yangu mengine yamesemwa lakini yale yaliyobakia nitaweza kuwaambia. Ya kwanza ningaliuliza hivi, kama yawezekana, tunapotafuta passports, ikiwa kitambulisho cha raia kinaweza kutambuliwa , sielewi kwa nini naambiwa tena nitafute birth certificates. Mimi ningetaka Birth certificate iondolewe, ibakie kitambulisho pekee yake ambacho ndicho kila mtu anaruhusiwa kuwa nacho. Maana ukienda hata kutafuta pesa au wapi, wao huuliza ulete kitambulisho sio leta Birth certificate. Kwa nini tunasumbuka na birth certificate tukitafuta passport? Nataka ikiwezekana hiyo Birth certificate iondolewe.

Sasa upande wa kuoana mtu akioa akiwa kanisani anapata certificate. Akioa kwa DC anapata certificate. Hata waislamu wanaenda kwa kadhi wanapata certificate. Kwa nini hii tunaita Customary Marriage hatuwezi kupata barua na sisi tunaoa hapa kila siku. Kuna watu wengi hapa wanaoa kila siku? Lakini hawana Barua. Kwa nini tusi ruhusiwe kupata barua kama hizo? Ningeliomba iwezekane na hata hawa watu wanaoa kinyumbani, tuwe tukipata barua zetu. Hiyo ni moja. Mengine yameguzwa guzwa kama vile, nimesisikia tuwe tukipata hata kule, kama ni kamati gani itaka potengenezwa, ya kienyeji ya kutoa barua, iwepo. Na nataka ikiwezekana ipatikane. Hiyo ni moja ya zile. Hao machief na ma sub-chief tunaambiwa tuko nao nataka tuwe tukiwakipigia kura. Tukiwachagua watu wamesema wachaguliwe lakini hawakusema kwa nini tuwachague. Ingalifaa tunapo wachagua tuwe na sababu. Wengine, chifu akikuchukia, utangojea mpaka a-retire au kwa bahati mbaya apatwe na neno lolote kama kifo. Sisemi ati awe akifa; hapana - aje afe ndipo wewe anayekuchukia utaweza kupumua. (**laughter)** Kwa hivyo, afadhali kumchagua, watu kumfanyia campaign ya kumkataa mpaka mkamwondoa. Hiyo ni nyingine. Tena yaweza kuwa yeye hajui maendeleo mnamuweka tu, mnamuweka tu. Mkiona akiwa hamumtaki, munazungumza na ukifika wakati wake, miaka yake imekwisha, munaambiana. Munamuleta mahali, munaambiana, wakati wa kura munamtupa. Maendeleo yenu yanaendelea. Sasa mnasema chifu achaguliwe na watu kwa nini achaguliwe na watu? Hizo ndizo

sababu zangu na mengine yamesemwa semwa sasa nikirudia nitaonyesha nimechukua hizo points za wenzangu nikiwa hapa hapa. Kwa hivyo, asanteni sana .

**COM. Tobiko:** Asante sana jiandikishe hapa. Elijah Mwamugunda? Richard Ingila?

**Richard Ingila:** Macommissioners na wananchi jina langu ni hilo mimesikia Richard Ingila. Basi mimi sina mengi kwa sababu mengi yamesemwa hapa. Lakini nitasema mawili, matatu tu. Basi mimi maoni yangu mwenyewe naunga mkono tupewe serikali ya majimbo, na tukipewa hiyo serikali ya majimbo yaani ni kama sasa tumekwisha pewa mamlaka tujitawale sisi wenyewe. Sasa hiyo serikali ya majimbo basi hapo tutakuwa na Katiba yetu. Katiba yetu sasa ni wana majimbo ambao watakaa chini na watazungumza vile wanataka kutawaliwa na basi hapo sasa tutajifanyia kila kitu sisi wenyewe.

La pili, serikali kuu lazima iwekwe na serikali kuu itakuwa na kazi yake. Zaidi, itakuwa na ulinzi, defence, halafu na pengine Judicial System ikuwepo hapo kwa serikali kuu. Sasa hapo ni kama nimemaliza lakini nikiongeza mengine kidogo, serikali ya majimbo vile vile, hata nyinyi mtakubaliana na mimi, tukiketi chini tutaanza kuona tutajitawala namna gani. Kitu cha kwanza, mapato yetu tutapata, natukipata mapato yetu, lazima tukumbuke serikali yetu kuu basi mimi nasema kwamba, yaani maoni yangu, sisi tubaki na70% na serikali kuu tuwapatie kama 30% yakuendeleza mambo yao.

La pili, serikali kuu isiwe na nguvu kuliko serikali za majimbo. Na pia, President asiwe na nguvu kuliko serikali ya majimbo. Kwa hivyo mimi yangu ni hayo tu. Asanteni.

**Com. Tobiko:** Asante sana mzee , jiandikishe hapa. Augustine Gaintoki?

**Mwadime:** **T**afathali mnaombwa mukija hapa hebu tumieni hii hii stand badala ya kutoa kwa sababu ita tatiza hapa kwa ajili ya kushikwa.

**Com. Tobiko:** Fundi Kilonzo, yuko?

.**Fundi Kilonzo**: Mabibi na mabwana hamjamboni nyote? Mimi jina langu ni Fundi Kilonzo, kama mlivyosikia. Natoa mchango wangu kuhusu elimu, ijapokuwa wengine wametangulia. Ijapokuwa ni kitu nilikuwa nimeshandika, nitaendelea hivyo hivyo. Mimi mchango wangu ni kwamba napenda watoto ambao wamefiwa na wazazi waweze kupata elimu ya bure kutoka Form one mpaka university.

Mchango wangu wa pili ni kwamba nachukia mambo ya ulevi. Kwa hivyo ningesisitiza kwamba ulevi, pombe na bhangi, pamoja na madawa ya kulevya yaweze kuondolewa ili vijana wetu waweze kuwa na msimamo na kuendelea vizuri.

Mchango wangu wa tatu, napendelea chifu pamoja na sub chifu wawe wanachaguliwa kwa kura. Kwa sababu kufanya hivyo, itakuwa mwananchi atakuwa ameridhika ni kiongozi wake ambaye amemchagua yeye mwenyewe. Mimi sitakuwa na mengi, nafikiri hapo nimeishia.

**Com. Tobiko:** Asante sana, jiandikishe hapo. Mwakio Lewala? Jairo Mukunji?

**Jairo Mukunji:** (Translator) Anaitwa Jairo. Anatetea ardhi yake, ya kwamba imepitiwa na maji na hawa wenyewe hawana maji na Kenyatta aliwasaidia ili wapate maji. Majibu yake ni hayo kwamba anataka maji, Irina. Hana mengi zaidi, yake ni hayo.

**Com. Zein:** Saul Mwanyumba

**Saul Mwanyumba:** Commissioner pamoja na wote waliohudhiria, mimi kwa majina kama vile mmesikia ni Saul Mwanyumba. Na kwanza na shukuru kwa kuhusishwa katika Katiba maana tulikuwa hatuelewi mambo ya Katiba. Ilitengenezwa na watu wengine ikaendelea, ikabadiiishwa, sijui mara ngapi. Sasa ni kushukuru kwamba tumehusishwa. Na kule kuhusishwa, pendekezo langu kwanza la kuhusishwa ni kuwa isiwe inabadilishwa kama sisi hatujaambiwa. Tuwe tunaulizwa kama tunaweza kubadilisha kipengele fulani. Tukiambiwa hivyo, tukikumbali, sawa sawa. Maana kwa sababu ilikuwa imetengenzwa, hatujui na ikabandilishwa hapa na pale, hatujui. Kwa hivyo nafikiri sasa kuyazuia hayo, watu tuwe tunaulizwa.

Pili, Kutokana na huko kubadilishwa na-kumbuka wakati mwingine ilikuwa mtu akitia msichana mimba, anamlea yule mtoto mpaka amalize shule ndipo awachane na hizo garama. Lakini ilibadilishwa. Pendekezo langu hiyo irundishwe. Huu mchezo umekua mmbaya, umezidi hata siku hizi unaingilia hata wengine ambao wako under-age. Lakini tuangalie hapo hapo na ninafikiri wote ambao mko hapa ni wazazi. Sijui tendo kama hilo, mtu anayetenda mambo kama hayo tutamfanya je? Kwa maoni yangu, ilikuwa huyu mtu hana tofauti na muuanji. Kwa hivyo awe charged kama muuaji. Kama sasa, mtoto wa miaka mitatu au minne huyo ni kama kuuwa?

Pendekezo lingine ni kuwa, tunataka Katiba itulinde. Nikisema hivyo kuna hii corruption inaendelea. Na hii corruption, serikali inashindwa na kumaliza hii corruption, Kwa sababu pengine hatulindwi na Katiba. Wale ambao wanagombea viti, serikali itulinde. Kama wewe ulikuwa corrupted wakati unafanya kazi, uzuwiwe na katiba kusimama parliamentary ama civic elections. Kama wewe unataka kusimama, mpaka testimoniasl zipatikane kuonyesha wewe hukuwa corrupt mahali ulipokuwa unafanya kazi. Maana tunachagua mtu aliyekuwa corrupt akienda parliament anaendelea na corruption. Sasa mtu kama huyo tutamfanyaje. Kwa hivyo, tunataka Katiba itulinde. Kila mtu anayetaka kusimama, testimoniasl zake sionyeshane pale alipokuwa akifanya kazi alikuwa clean. Sio kusimama kwa sababu ati una pesa na wewe ni currupt. Sasa serikali haiwezi kumaliza corruption. Kwa hivyo Katiba yetu itulinde hapo.

Haya mengine yamesemwa-semwa lakini nitayarudia. Mwanamke ambaye wameungana na mume wake kwanza nitaanzia akiwa nyumbani, kama mimi mzazi nisibague wakati wakugawa uridhi. Kila mtoto alindwe na Katiba ana haki ya kuridhi chochote awe niwa kike ama wa kiume awae na haki kwa uridhi wa baba yake ama wazazi wake. Na hapo hapo kwa kuendelea, mama ambaye tunaishi pamoja, tunataka alindwe na Katiba kwamba mali yote ambayo tumeteingeneza tukiwa pamoja, awe naye na haki ya hio uridhi. Maana unaweza kupata ati mama anafanya kazi, wakati mwingine wakikosana na bwana atazuiwa hata kwenda na sanduku lake la marinda yake kwamba wewe ni mwanamke, tumekosana kwenda. Awe na haki, alindwe na Katiba kwamba chochote wametengeneza pamoja kama ikiwa wanaachana, wawe wanagawana.

Na kwa upande wa hizi ID naona zinaleta kuzunguka zunguka kwa vijana. Kama vijana popote walipo Kenya, kama wawe identified kwamba ni mkenyan, wapate ID mahali popote walipo.

Kuna hii mambo ya Area. Ingawa pengine inaonekana sijui sana lakini nakumbuka zamani ilikuwa sijui ni miaka ya hamsin,i zile Title Deed za zamani. Sasa ilikuwa ni lengo langu eti wakati wanafanya re-new hata hii National Park, hizi shamba kubwa kubwa ambazo sijui ziliuzwa ama zilipeanwa, na kwa sababu ilikuwa wakati ule ambao sio wakati wetu wa uhuru ndio hayo yalifanyika. Kwa hivyo mambo kama hayo kama yalifanyika wakati ambao ulikuwa sio wetu, tutaomba katiba nayo itulinde. Maana sasa ukiangalia district kama hii, sehemu nyingi ni National Park. Na tuna-ambiwa wenye hiyo area ni watu ambao wako nje. Kwamba area kama hizo, pendekezo ni zile title deed zao zikiisha wasipewe tena mpaka wenyeji wa area hiyo wa-ulizwe ama wahusishwe. Kwanza plots nyingi ambazo zimekuwa grabbed ama zimetolewa hivi hivi, wakati hizi title deed zinakwisha,wenye kuhusika ama wananchi wa pale waulizi watoe maoni yao we kama watapendelea zile renewal isiwe ni commissioner peke yake anafanya.

Lingine ambalo nilikuwa nalo kuna haya mamlaka ambao hatuelewi sana ya ku-create posts na kufuta kazi ama dismissing hao watu wote, ma-ministers, PS, PCs, Directors hata nafikiria ma DCs ambao hayo yote ni mamlaka ya Rais. Hata wakati mwingine wananchi sisi ambao tunahusika na katiba huwa hatuelewi huwaje hata wengine unakuta wanaachwa hivi hivi. Unakuta Permanent Secretaries hao ndio wamechaguliwa, wengine wanaachwa hivi hiv,i na-fikiri mambo kama hayo, yawe ni mamlaka ya parliament. Yasiwe ya president to create offices, iwe ni mambo ya parliament. Hao tunaowachagua wakilishi wa parliament ni kusema tumewamiini na wao wenyewe hawawezi kuharibu wakijuwa sisi ndio tumewachagua. Kwa hivyo, mambo kama hayo yawe ni mambo ya parliament, yasiwe ni mambo ya appointing person ama President.

Lingine, hii mambo ya kutengeneza serikali ama forming the government. Wakati mwingine unakuta KANU imeshinda tena ina-form the government halafu anachagua watu wake hata wengine hawana ule uwezo waku ongoza idara kubwa hata ministries. Kwamba hata chama kikishinda, sisi tunachotaka, ni kiongozi bora lakini isio ya chaguo. Nakumbuka safari moja nilienda nikakuta Director ambaye alikuwa askari wa prison, sasa na-shangaa huyo mtu amekwenda kuwa director, kweli kutokea pale, hata kama alikuwa na akili kwenda mpaka yeye pengine alikuja kuwa SP au whatever it is, lakini kweli anaweza kuwa yeye Director of even a bank? Kwa hivyo mamlaka kama hayo, ile winning party ituchagulie viongozi ambao wanaweza

hizi kazi si kwa kuchagua tu kwa sababu huyu ni mwana KANU, askari anenda kuwa Director au mtu mwingine alitoka sijui wapi alikuwa hata minister ambaye hata ukimwangaliwa unawesa kushindwa anafanya kazi gani.

Lingine hapo hapo, ni hii wakati mwingine na shindwa na kuelewa civil servants. Maana wakati ulikuwa civil servants, na unaweka sahihi utafanya kazi popote Kenya. Sasa tukirundi katika hii local administration, unakuta chief ni civil servant, assistant chief ni civil servant. Sasa tuna-shindwa tunataka kuwa sijui kama zamani ukiwa na assistant chief ama weak chief ati wananchi hungoja thirty years ndio a-retire.

**Com. Zein:** Unapendekeza nini? Unanjua ni kumalisa tuna malizia

**Saul Mwanyumba:** Napendekeza, hao tuwe tunawachagua kama wajumbe.

Mambo ya pension yamezungumzwa, nafikiri na mimi nimeyaguzia kidogo. Kwa akina mama kwa sababu ni mwili mmoja kufwatana na dini, nisiwe ni mimi peke yangu napewa mpaka nife. Maana sasa ni-na pension nitakula mpaka nife nitakula lakini ni kifa, yule mwenzangu nimemuacha, naye ale mpake afe.

Nakufuatana na serikali hata safari moja nilikuwa kwenye very remote areas ni kashindwa kweli hapo uhuru umefika. Unashangaa kwa sababu hii serikali tuliyonayo sasa haiwezi kuona kila corner ya nchi yetu. Napendelea kuwe na ile federal government, ile itaona kila mahali.

Kuna hizi natural resources zetu tumezungumza hapa maji Tumezungumza hapo madini madini na tunataka na hizi, serikali ama Katiba yetu itulinde. Maana sasa hata haya maji ya mzima inayo-wafaidi sana sio wale ambao haya maji yanayotoka.

**Com Zein:** Unataka tufanye namna gani?

**Saul Mwanyuimba:** Sasa tunataka hizi natural resources ziwe mikononi mwa wale watu wanapoishi pale. Tuulizwe, hatuwezi kukataa na maji hata kama tuna uwezo wa madini, hatuwezi kukataa nayo kama wewe una uwezo lakini ziwe ni mali ya wale wanoishi pale. Kwa hivyo, wataita wanasema (inaudible).

**Com Zein:** Ahsante sana Nathan Mbogori, Stanley Mwakesi. Stanley? Ngoja nafikiri mmoja amekuja. Wewe ndiye Nathaniel?

**Nathan Mbogori:** Mimi ndiye Nathan Mbogori. Commissioner, nashukuru sana nyinyi kufika hapa turekebishe hii Katiba. Mambo mengi yanatusumbua rohoni ikiwa kweli mmekuja hivi tunashukuru sana na mengi yangu yamesemwa sana, ndio ninafuraha sana.

Kuzungumzia kidogo, kuna ya hawa watu tunaofanya kazi nao hapa ambao tumesema Chief na subchief. Hao watu yafaa tuwachague sisi wenyewe kama wabunge kwa sababu ndio watatusikiza na sisi tuta-wasikiza kwasababu hatuwezi kufanya kazi na m tu ambaye hana maendeleo sisi sote tutakuwa wanjinga kwa ya miaka nyingi mpaka a-retire. Tunataka vile akiwa hatuendeshi kama tunavyo-taka, maendeleo ya kisasa abandilishwe. KamaTaita District aende akae hapo, abandilishwe mradhi aone mambo mengine ya wale watu, aone maendeleo angalau na sisi tupate mtu mwingine ambaye anaweza kutufanyia mazuri zaidi.

Kisha jambo lingine na-shukuru sana kwa hii Katiba kurekebishwa, irekebishwe sisi mahali tutapata njaa miaka yote hii na wabunge wetu na serikali yetu angaa itufanyie muhimu sana irrigation katika nchi yetu hii tupate irragation. Inaweza kutosheleza na mambo mengi. School fees tunashindwa, hatuna mchango. Mchango wetu ni kidogo sana kwa sababu sisi wenyewe tunanjaa na mashamba hayana kitu. Kwa hivyo tukipata irrigation, inatuwezesha kupanda mboga, vitu nyingi sana kama matunda. Na hivi tena kitu kingine tunachotaka ni bore hole. Hii bore hole ni muhimu sana lakini naona ajabu na nina- shukuru kwa sababu ni kurekebisha Katiba. Kwa hivyo hizo bore holes nazo ziwe ni muhimu sana zituzaidie kulima mboga na njaa tuiondoe na maji katika mashamba yetu.

Na mambo mengine, kama wanyama wa pori. Unatia mti wako maji miaka kum,i pengine wasumbuka na maji. Sasa leo mnyama mdogo huyu ndovu anamaliza kabisa hata unausahau kabisa. Kwa hivyo tunaomba Katiba iwazuie sana hawa wanyama wasije katika mashamba yetu.

Na mambo mengine tupate hao watu wajuzi wanaotufundisha mambo ya Agriculture ambayo tukilima tusifeli tuwe tunashnida ili tupate chakula kingi.

Pia na mambo ya shule zetu ziwe zina angaliwa sana kupatiwa walimu ambao wanafaa. Tusiwe mtoto unamutolea fees mtoto anafanya vibaya warundia rundia ata mimi nitachoka wakati mtoto hajapata elimu ya kutosha.

Kisha tunataka bara bara sitengenezwe, maanake hata hayo matunda ama hizo chakula tutasafirisha na nini? Lazima barabara ziwe tayari za kusafirisha mazao au mali hiyo ili tupate pesa ya kuendeleza economy.

**Com. Tobiko:** Umemaliza mzee wangu ama bado?

Nataka kumaliza. Kuna jambo ndogo. Nikukumbuka nitakuambia. Kwa hivyo, mengi, mengi tunashukuru. Hayo yaliosemwa hapa yalikuwa rohoni mwangu kabisa lakini sitaki kuyarundia. Lakini mengi sana yamenifurahisha sana. Nafikiri hata katiba hii ikimalizika itakuwa nzuri sana na tutakuwa hatuna shida kwa sababu seventy five per cent ni mazuri yote.

**Com. Zein:** Ahsante sana mzee wangu. Jiandikishe hapo. Stanley Mwakes.i

**Stanley Mwakesi**: Commissioners, bwana Abubakar Zein Abubakar, na Tobiko na Madam Wanjiku kabira na kamati yake na wananchi ambao wamekuja mkutano huu wa mageuzi ya Katiba. Mimi ni mmoja wa wanakamati tume ya kurebisha Katiba lakini nina machache ingawa nimeandika memorandum lakini nina machache tu ambaye nitaguzia. Na hata kwamba kwangu mimi, sijui nitakua tofauti na wengine kwa sababu ya background yangu. Pahali nilifanya kazi nime-operate na hii Katiba ambayo iko sasa na kwa kweli nita sema kwamba Katiba iliyoko sasa, hata hivi kama serikali imetumia pesa nyingi ili Katiba ibandilishwe, ukweli wa mambo ni kwamba kama haikuwa kwamba Kenya kutokana na Katiba hii tukonayo tulipoteza viongozi ambao hatungelihitaji kugeuza hii Katiba kama wangelikuwa wako hai. Lakini maisha yao yalipotea kwa sababu ya Katiba ambayo tukonayeo ambayo inampatia Rais uwezo karibu kuwa mtoto ama mungu mdogo. Ni mungu mdogo Kwa sababu yesu mwenyewe aliuwawa na wanadamu. Lakini Rais wa Kenya is above the Law. Na hii ndio ilisababisha kwamba tuliwapoteza watu muhimu sana kama JM, Tom Mboya, Ronald Ngala. Ni katiba hii ambayo tuko nayo. Kwa hivyo ina hitajika kwamba Katiba hii ifanyiwe mageuzi na isitoshe, mukiangalia ni kwamba Kenya ya leo inaongozwa na vipofu. Vipi kusema hivi? Rais wa Kenya ndie Chancellor wa all the universities in Kenya na hana Degree, lakini mdogo wake ni professor. How comes? Inawezekena na-mna gani? Professor Saitoti ni Msomi na ni professor.

**Com Tobiko:** Bwana Mwakesi, pendekezo lako ni gani?

**Stanley Mwakesi:** That is where I am heading to Mr. Commissioner. Ni uwezo wa Rais. That the powers of the President should be trimmed. He should not be above the law. He should not be the chancellor for all universties in Kenya. Neither should he be the commander in chief of all armed forces because it is well known that he cannot even fire a gun or a bullet for that matter.

Similarly, he doesn't have a degree. Why should he be called a chancellor? Why should he be a professor? Why should he be the head of those who are learned? If we check with you guys just now as the Commissioners. You are all very learned people. I am sure of that. Kabira is a lecturer at the university. Clearly, anybody can see that this is a learned guy. You are all learned. Lakini kwa sababu Katiba ya Kenya inaruhusu aina hiyo ya utawala, ni kwamba Rais amekuwa na mamlaka makubwa .

Twende kwa nomination. Yeye ana-nominate wa-bunge kumi na wawili. Hiyo iondolewe kwa sabubu mfano mzuru bwana Tobiko ni kwamba hata wakati President Moi alichukuwa delegation kwenda London, alichukuwa mbunge mmoja kutoka Ukambani ambaye London mzima anaulizwa, "what will you take?" anasmea na anaongea kikamba kule London. Na that one is because he has got the powers to do what, to nominate anyone he wishes.

Now, ukweli ni kwamba uwezo wa Rais umekuwa mkubwa sana ambako yeye anatatiza kila hali ya utawala. Tuangalie sasa,

Rais anauwezo kwamba bunge imepetisha. Baada ya bunge kufanya shughuri nyingi kimjadala, kupatana na wapitishe swala fulani tumekubaliana, Rais kama atatoa kibali, assent as in assenting to a bill hiyo inakuwa Shelved. Attorney General ambaye ndiye anamchagua, yeye mahakama ya chini inapata mtu na hatia ina recommend aende katika High Court. Akifika high court inampata na hatia Raisi ana uwezo unaitwa Presidential pardon. Now hii mahakama kwa nini itaambike na mtu kama huyo harafu Rais anaenda pia anasema kwamba mtu huyo nimemuachilia under presidential pardon?

**Com Tobiko:** What do you recommend?

**Stanley Mwakesi:** Presidential pardon iondoke. Mahakama iwe independent ambayo itafanya kazi kufwatana na haki za kisheria.

Twende kwa bunge. Bunge bado niko kwa Rais tu, huyu ndiye mtu ambaye naona kwamba ofisi yake ndiyo inaharibu Kenya. Yeye bado ana uwezo wa ku summon to adjourn and to dissolve the parliament. Why? One guy ana amua tu leo naenda kufunga bunge, leo nimeivunja. Why? Now where is the power of the parliament. Unaona Judiciary, it has been interefered with by those presidential powers. Parliament imekuwa interfered with, now where are we? Kwa hivyo kitu kinataka kupiganiwa katika hii Katiba ni Rais awe kwamba uwezo wake uwe wa kadiri na bunge……

**Com Tobiko:** What is your recommendation?

Mr. Mwakesi: my recommendation is Parliament ipewe uwezo zaidi kuliko sasa. Parliament should be the supreme law making body. So far as we know ni kwamba bunge ndio hufanya makadiri ya pesa za serikali ya Kenya, bunge ndio link between the government and the people. Now it should be empowered.

Twende kwa foreign affairs, Katiba ya sasa inampa uwezo Rais wa Kenya kwenda na kufanya mapatano na nchi yeyote bila kuwasiliana ama bila kuhusisha wanachi ama bunge lenyewe. Na ndio sababu Kenya tuna mandeni mpaka saa zingine unasikia mtu anaenda kuomba ati mwingine afutwe. Kwa hivyo, parliament ipewe uwezo.

Na recommendation ingine ambayo na weza kutoa ni kwamba, wacha bunge liwe kama vile lilikuwa zamani. Lets have a lower house and an upper house. Kwa sababu tukiona uchumi wa nchi ambazo tunasema leo zime endelea mpaka tunaenda kuzikopa kila siku mpaka zinatuona kama wanjinga kama wa IMF. Sasa wanaona wa Kenya kama ni waezi wote. Not all of us that were thieves. A few Kenyans ambao wako katika top echelon katika hii government ndio wanafanya mambo kama hao na wa-Kenya ambao wanyanyaswa ha wahusiki kwavyo mambo ambayo yanayohusiana na Kenya na nchi zingine za nje iwachiwe Parliament. Na ikiwezekana, wabunge, kwa maana ndio tunawatuma kwenda kutusimamia warundi kwetu ikiwa mambo yamekuwa magumu kwao, wachukue mandate yetu. It is us tunawapigia kura.

Kitu kingine cha ajabu sana Kenya ni kwamba wakati tuko hapa, tukisema sasa hivi tutachanga, wengi wetu hapa watatoa pengine shilingi hamsini shillingi mia moja. Lakini utasikia Rais Moi ametoa elfu mia mbili. Kuna jamaa mwingine hapa yeye huwa anatoa milioni. Now this gap, how can you fill it? If the Constitution will not be made in a way that we reconcile, then you can see the danger. Hii ni tabia ambayo imesababisha wizi. Mimi nina-lala njaa halafu njilani wangu hula chapati na nyama za kuku akatupa kwenye mapipa. Kwa nini mimi watoto wangu wakilala njaa wasiende kula hiyo chakula ya mapipa? Halafu mpumbavu kama huyo ndio anasema watoto wa Mwakesi ndio wanakula kwa mapipa. Kwa nini wasikule na ulitupa nyama zikiwa live live?

**Interjection:** Laughter

**Mr Mwakesi:** Tuende kwa defence ya nchi hii. Kwa nini mtu mmoja apewe uwezo wa kutangaza vita au wa kutangaza curfew ama awe ndio preserver wa Public Security. Public security should be enhanced or should be handed over to Parliament. Bunge, Kwa sababu kwenye bunge, tuna watu ambao wanasimamia watu wote katika nchi yetu. Kwa hivyo, hapo ndio sauti ya mwenye nchi iko. Kwa hivyo…..

**Com. Tobiko:** Tumekuelewa hapo.

**Mr Mwakesi:** Sasa naenda kwa basic rights na mambo kama elimu. Mimi naonelea kwamba sisi wakenya kidogo tumeonekana ni wapumbavu. Maana tunaambiwa masomo ni ya bure ama chochote kile. Lakini tunaona sisi wazazi tuna adhirika sana ambako sisi ndio tunanua kalamu kutoka pencil, biro pen, exercise books, text books and school fees tunalipa. Na huku tunaambiwa masomo ni kama ya bure. Ukweli ni kwamba, Primary Education, elimu ya msingi, it should be compulsory and free. Ya lazima na bure. Wewe Mkenya upatikane una mtoto hapo nje ambaye haendi shule upate adhabu ya kukufao, ile inatoshana na wewe. Wewe angalia ni adhabu gani inakufana. Wewe mwenyewe. Kama wewe ni mkenya, angalia ni adhabu gani itakutosha.

Kitu maji sisi taita ni kutu ambaco si-pendelei ni hali ile ambayo iko. Maji ambayo yanaenda Mombasa, ambaye yananyosha meli na watu wa Mombasa yanapitia hapa tu, hapo kando kando. Lakini kama mngalikuja wakati wa ukame, hapa, mngaliona mwanamke angeweza kutoka asubuhi kutafuta maji arudi jioni. Kweli hapo kuna haki? Ni kwa nini tutendewe hivi na maji yanapita hapa? Kwanini tusigawiwe . Pia tukiangalia topographically Lake Jipe is at a higher latitude. That means that if the government would have, that is kama kungalikuwa kuna utawala wa kisawasawa sisi tungalikuwa tumepata maji kutoka lake Jibe kwa sababu it is a fresh water lake and it is at a very high latitude na haya maji yangalitusaidia kulima na pia ya kunywesha wanyama wetu na sisi wenyewe.

Tuende kwa mambo ya madawa. Haya yameongewa sana. Ukweli ni kwamba Kenya nzima sasa, usipokuwa na pesa, afadhali usipeleke mgonjwa wako hapo. Kwa sababu hospitali, badala ya kusaidia watu wapone wanaishia watu. Wewe

unapeleka mgonjwa wako na huna pesa, anza kuchanga nyumbani pesa za kukomboa gari ibebe maiti. Sababu ma nurse wote wanasema, "mna chapaa?" Chapaa ni kusema je na nina mgonjwa hapa anakufa? "Eh, una chapaa baba?" Sasa hii lugha ya chapaa halafu unakuta nurse anashona crochet yake, ni nini hii? The government should take care of its own citizens. Tuko katika peril ya ukimwi ambaye tunapoteza watu wengi kwa hivyo, wale wanashikwa na magonjwa mengine afadhali wasaidiwe waishi kuliko wale wanashikwa na ukimwi maana tunajua hao wanaenda.

Na kwa upande wa ukimwi, mimi nafikiria kama itakubalika lakini naona ni wazo nzuri, Kenya, wacha itengeneze natukubaliane kwamba doctors should be allowed to finish up a dying patient . Sheria itengenezwe ambayo katika Katiba ambako mkenya ambaye anaonekana ni wakufa amalizwe na madaktari. Kwasababu gani nasema hivo? Mtakubaliana na mimi kwa sababu tumeona hivi ata watu wengine, watoto wengine sasa wamepata laana kutoka kwa wazazi wao kwasababu ya nini? Mtu unakuwa umeenda lakini ….. (Taita dialect)

**Mr Mwakesi:** National Park, Taita Taveta vile tumeelezwa mara nyingi sana thirty two percent of Taita Taveta ni mbuga za wanyama.

**Interjection:** Sixty two per cent.

**Mr Mwakesi:** Ahsante sana. Sixty two per cent ya ardhi yetu ni mbuga za wanyama, sisal estates and ranges ambapo sisi, na kwa maana kidogo hapo nyuma tumekuja kujua kwamba Title Deed ama lease, nafikiri hii ni Title Deed hizi mbuga za Tsavo east and west ziko kwa great danger. Kama hujajua, na kufahamisha. Ukitaka, tukimaliza mkutano unipate nikuelezee vizuri. Sasa tunataka, tunaomba hivi hii lease ama Title Deed, tuifanyene ili itoke. Uingereza irundi hapa ili tuwe na sisi wataita kwa hii National Park ambaye ndie imechukua ardhi yetu kubwa kuliko sisi pahali tunapoishi angalau tupate chochote?

Tukifikiria kuchagua wabunge nafikiri wale mmekunja hapa, mimi sina miaka mingi sana. Kuna wazee wengine wakubwa kuliko mimi lakini na-ona wakati, wowote, kwa sababu ya unyonge wetu ama saa ingine ni-kisema bila kuona haya wacha niseme kwa sababu ya ujinga wetu, sababu hapa Taita naona kitu hutokea mtu ukija ukiwa una kipara kikubwa na tumbo kubwa, wewe unaenda bunge. They do not know that what matters is upstairs. Viongozi wachagulie kwa sababu wana-akili na wanaonekana kwamba wanaweza kufanya kuongoza watu. Tusichague watu kwa sababu ya siala, vipara na tumbo kubwa na pesa

**Com. Tobiko:** Mchague kwa nini? What are the qualifications?

**Mr Mwakesi:** The qualifications for a member of Parliament; should have form four level of education and above and he should have passes in English, Swahili and Mathematics. Why I am saying so is this, because if the parliament is just a place where people expenditure estimates for the nation are carried out, then they should have some knowledge in mathematics.

**Com. Tobiko:** Understood Okey. The other qualification?

**Mr. Mwakesi:** And the other one is age. The age of a member of parlimanent should be twenty one years for the minimum and maximum should be seventy according to his performance, that one should be open. A member of Parliament who fails to deliver the goods , yule ambaye ame enda kwanza yule mbunge tukipiga kura kama hizo sijazo tukipiga kura, yule ambaye amepita halafu ameshindwa na kuhudumia wananchi yule alikuwa wa pili, kuzuia serikali isiweke garama zingine kwa kodi ya mwananchi wake, yule alikuwa namba two aende. Huyu namba pili akienda akishindwa hiyo area ibaki tu mpaka next election. Kwa sababu hio niku-punish the electorate ambao hawajui kuchagua. Mbona muchague mtu wa kwanza hafai, wa pili hafai basi ata nyinyi hamfai. County council the same.

**Com Tobiko:** Hiyo iwe hivo tu. Hizo umesema. Jaribu ku-surmarise unajua dakika zako zimekwisha.

**Mr Mwakesi:** Ahsante sana. Najaribu sana. Maneneo yamekuwa matamu zaidi.

Naomba kwamba watu ambao wanatoka jeshi, watu ambao wamekuwa wakubwa katika jeshi, wale military retired men, kwetu iko mmoja ni mkubwa sana. Kuna mwingine ukambani. Sioni sababu gani mtu ambaye alikuwa anafanya kazi ya bunduki aende kuwa Director kwa ministry of Health. Is it related ? Tofauti inakuwa kubwa sana. Sindano na bunduki? Military men wakiwa retired, hata mtu wote Kenya tuseme aki-retire, aende kwa bibi yake atulie. Kama hana bibi aoe mwingine mdogo, hakuna shinda…………

Na watu ambao ni wenye masomo, watu wenye kisomo kama wame retire, tuna universities sasa. Kama sasa watu wa military men, tuna so many military academies. Why can't they go and become lecturers there. To lecture to those young people. Wawafundishe vile wanaweza kuwa wanajeshi wazuri kuliko sasa Kenya tunasomesha watoto harafu unakuta tena mzee kama mimi ndio tena naambiwa ati mimi ndio Chairman wa pahari fulani. Mimi ambaye nina mtoto ambaye ana Degree nyumbani. Harafu mimi tena ndiye napatiwa kazi nyingine . Kwa nini mtoto asipewe? I don't know sijui? Nyingi ndio mume soma ndio mnaweza kueleza vizuri.

Kitu kikingine ambacho kinafaa kuangaliwa ni provincial administration. Mimi nafikiria kwamba hii mambo ya ma-PC. Mimi sioni PC anafanya kazi gani in the first place I do not see what job the man does. PC anafanya nini? Nani anaweza kunisaidia hapo PC hana kazi yote. Harafu angalieni utawala huu ambao uko sasa. Mambo yanaanzia kwa mzee wa kijiji. Hiyo ni namba one, inaenda kwa assistant chief, namba two, inaenda kwa chief namba three, inaenda kwa DO namba four, inaenda kwa DC namba five inaenda kwa PC namba six inaenda kwa Permanent Secretary namba seven. Inaenda kwa minister ambaye anahusika namba eight, namba nine ndio imefika mbunge. Kama ungalikuwa mgonjwa, utakuwa umekufa na unazikwa na ukaoza. Ile mambo ulipeleka, haijafika.

**Com. Zein:** So what do we do with it?

Tuwe na system moja, majimbo kitu kikitoka Coastal province au ni mkowa wa Central, province moja kwa moja kwa lower house, lower house inaenda kwa upper house na kupata matokeo. Kwa nini itakuwa (taita dialect). So kwa hayo machache, niko na memorandum ambayo ina mengi na nitawapa.

**Com. Zein:** Makofi kwa huu jamaa tafadhali. Iko swali lakini ujue iko swali swali langu ni ndogo tu . Tukiwapa madaktari madaraka ya kutoa roho za watu, hufikirii kutafika wakati watatumia madaraka hayo vibaya waue watu ovyo ovyo? La pili kwamba hayo hayo ya kumpa madaraka cheo hicho watu wananchi kama hawa wakijua kwamba daktari ana cheo kama hicho kuna mtu atapeleka mgonjwa wake hospitali kweli?

**Mr Mwakesi:** Ah! Bwana Abubakar , Commissioner kwa heshima nitakujibu hivi. Mgonjwa asiuwawe bila ya idhini ya watu wake. Kama mimi Mwakesi nimekuwa mgonjwa na nina bibi na watoto wangu, watoto wangu waitwe na iwe na proforma, a sheet they should sign to avoid any future legal action against that appropriate doctor. Waweke sahihi kwamba sisi vile tumeona baba yetu. Now I give a very good example of the late President of Tanzania, the late Nyerere. His son flew to London, lakini wakati alikuta babake ako katika hali mbaya alisema, “No, it is only God who makes people live and die. So , muondoeni huyu babangu. Mnamuweka mapumzi, pumzi gani ?” (Taita dialect) and he died. So there should be a mechanism. I am not saying that it should be done wantenly, ati mtu akionekana huyu ni wakufa awekewe doze. There should be a way, a method, a plan ata ikiwezekana, kama kuna Magistrate aitwe.

**Com. Abubakar:** Thank you. Allan Mkoji? Chrispus Msagha?

**Chrispus Msagha:** Wanakamati wa Constitution na-shukuru sana, majina ni christopher Msagha. Kwa vile mengi yamekwisha na sema hivi kwa vile wengi wameshaongea mambo mengi kuhuuza ii mageuzi ya Katiba, mimi nina mawazo kidogo, mawili, matatu. Ya kwanza ningependa zaidi ya kuhusisha land ceiling katika jamaa. Hii inakuwa tatizo kubwa sana, inakuwa mtu mmoja ambaye kwa shida zake binafsi inabidi auze hilo shamba, langu lingekuwa kwamba jamii ihusishwe ikiwa kwa vile tuna clan hii (Taita dialect)

Lingine limeongewa sana ni kuhusu mbuga za wanyama. Kwa kusema kweli sisi wataita tungekuwa tuna faida katika hizi mbuga tunajua serikali ya Kenya imepata pesa nyingi kweli kweli. Ni kwa nini kama shule za hapa kwetu na bara bara na pahali pa kutibiwa, dispensaries, kwa nini tusipewe uwezo wa hizo pesa zitumike kwa kuinua hali hii. Njia, pia, mradi wa maji tunakoza, wakati wa ukame watu wako na shida sana kupata maji. Wanatembea usiku na wanyama hao hao ndio wana-wasambua kuchukua maji, na wana waua wanadamu na nchi ni yetu. Basi pendekezo langu (Taita dialect)

La tatu ningesema, nitaingilia hali ya biashara na voi town, tukiangalia hapa, hii voi town mtaita hayuko. Vijana wote wako nyumbani. Unakuta mzee ako na watoto kumi. Karibu wote wamemaliza shule. Wako hapo tu na biashara katika mtaa wa voi, ni kabira zingine zimepewa kipawa lakini sisemi ni vibaya, wanauwezo. Lakini, tupewe priority sisi ambao tunatoka area hiyo tuhusishwe. Ukienda kama Karatina, huwezi kupeleka matatu ama uwe na kibanda bila wewe kupitishwa na wananchi.

Haya la mwisho ninge ingilia haya mambo ya akina ma-chief na assistant-chief. Hawa watu wana uwezo mwingi ambao ingefaa tuwachague. Limesemwa sana. Kwa vile ikiwa hamsikizani ama mukiungana anaweza benefit. Kama kipande changu cha shamba, chief akisema huyu muondoe ana uwezo kama huo. Kwa hayo machache (Taita dialect)

**Com Zein:** Ahsante sana. Jiandikishe hapo. Reginald Mghanga? Peter Mshambala?

**Peter Mshambala:** Commissioners, na wananchi wenzetu, nafikiri haya yote yalizungumzwa mimi nitachukua muda sana kuyazungumza lakini hayo yote yamezungumzwa ndio ilikuwa niyazungumze. Hasa yale pia nataka kuongezea point haya ya mipaka na Majimbo kwa hivyo sina zaidi ya kuzungumza kwa sabubu kuna wengi. wanangojea hapa. Kwa hayo machache, Ahsanteni.

**Com. Zein:** Ahsante sana Mzee. Philliip Poka.

**Philip Poka:** Hamjambo nyote? Mambo ya Kati hii Mambo ya Katiba hayakuwanza leo. Sisi Katiba mwaka wa sitini na tatu huko Mombasa, ilikuwa ni KANU na KADU. KADU na KANU tunapigana tupate majimbo. Tukamtuma mzee wetu Jomo Kenyatta, na Jaramogi Oginga Odinga na upande huu tukamtuma Ngala na Mzee huyu marehemu. Walikwenda mara ya kwanza, hawa kuelewana. Mara ya pili, hawakuelewana. Mara ya tatu, hawakuelewana. Mara ya nne, wakaja na majimbo. Majimbo saba ile ilipokuja, sisi wenyewe KADU na KANU twapigana. Majimbo saba tuliposimama, ilianza kazi ikapitishwa ni majimbo saba. Ikawa ni upper house na lower house. Pengine kuna wengine hapa rika langu watajua upper house na lower house. Tukaambiwa ile upper house ni President, lower house ni ya majimbo saba. Mnasikia. Yale majimbo saba, watu wanasema kwamba President siku hiyo alipewa askari jeshi wake navy wake, anga za juu au uwanja wa ndege ni wake. Mnasikia. Sisi majimbo tulipewa polisi, askari jela katika majimbo na yule mzee akapewa yeye ana uwezo katika manjeshi. Yale leo unaona nasilaha kali. Sisi tukawa, Katiba ilianza kazi hata tukafanya uchaguzi. Kuna mwenzangu hapa kidogo aliguza mwaka wa sitini na tatu na tulikuwa hapa. Unaona mahali. Tulikuwa twapigana sisi wenyewe kwa wenyewe KADU na KANU. Wanasema majimbo sasa. Na sasa majimbo haya haya yamerudi msingi. Hata nikiangalia kitabu hiki, sioni majimbo ya zamani ikitajwa na kitabu hiki, mnaona ni kiekundu hiki, mwakiona? Kama hamjatengeneza majimbo sawa sawa damu

itamuagika. Mnasikia? Mimi nimepigana na nilipigania chama changu. Vyama vilikuwa viwili tu. KANU na KADU. Hata ndugu yangu tukikutana pale kama ni mlevi tu mimi na- mwambia mimi ni KADU naye ananiambia KANU, tena ni ndugu yako wa tumbo moja. Bibi yangu ni KADU mimi ni KANU. Vyama vilikuwa viwili na kama ilikuwa ni haki katika Kenya, vingekuwa vyama vitatu, uchaguzi ungalikuwa mzuri sana. Sasa vyama vimekua vingi. Vyama vingine hata havinjafika hapa. Hapa tunajua KANU na DP basi. Zingine twasisikia kwenye radio tu. Kwa hivyo mambo, mseme wazi wazi twataka majimbo, mnasikia? Maana siku ile sisi tulisema twataka majimbo, na tukatengenezewa majimbo, leo mwaficha. Na majimbo ilikuja kwasababu gani? Niwambie tuna kabila kubwa na ndogo. Kabila kubwa zinazopatikana ni tatu katika Kenya. Walio wengi zaidi. Tulipoingia katika majimbo sasa, twatafuta kabila kubwa kwenye majimbo. Wataita si wengi kuna jimbo pale wako wengi kuliko wataita. Wasikia? Tukazunguka tena kuenda upande wa juu. Wajua KADU ilikuwa juu na KANU chini, takapata jimbo moja, watu wako mia mbili na hamsini. Kabila kama taita, mnasikia? Ikawa tukazungumza tukasema KANU na KADU wameketi, waletewe madakatri kutokaka ulaya ma-nurse na tembe nzuri na ma-daktari kusudi wale wongezeke wafike angawa elfu moja. Watu mia ngapi? Mia mbili hamsini. Labda nyinyi mnaoketi pale…… pale na zungumza tuko pale. Kwa hivyo nyinyi msifiche. Semeni wazi nyinyi mmeokoka au hamkuokoka? Mimi sikuokoka. Mimi nasema nataka majimbo. Tosha.

Sasa hivi muanze kusikia panga zimevuma hapa mtakimbia nyote. Mmesikia Bethlehemu? Bethelehemu mmesikia vipi? Wote nima-ndugu wanapendana lakini chuma kinaendelea. Hta hapa (Taita dialect) Natetea chama changu na wewe utetee chama chako. Watu wamekufa Mombasa, hamjui. Sisi tulikuwa kule. Wengine wana mapanga wengine wana marungu. Na pale tunasema, tunaimba, wahindi kwao, wazungu kwao wa arabu kwao. Sasa hapo tunafikiria tukipata uhuru, wahindi, wazungu wata-kwenda na wa arabu wata kwenda na wahindi (taita dialect) Hii nimesema nini? Katiba utengeneze mwenyewe. Hii karatasi mumepewa bure, ati muanze kusema habari ya ati ndovu, nini? Semeni maneno ya ukweli maneno ya ndovu hizi, mkishapata jimbo, ndio mtauriza sasa maneno ya ndovu zitafanywa nini. Maana mkishapata jimbo lenu sasa tutazungumza maneno ya ndovu. Itakuwa lini, na ni hapo ndio mtazungumza. Sasa hujapata jimbo unazungumza maneno gani haya? Mambo ya ndovu.

Basi mimi nawambia kweli, mimi nilianza , tunatoka kazini twapigana njiani KADU, KANU, majimbo sasa. Majimbo sasa. Ukisema majimbo, saa hiyo hiyo wewe unakula chuma ya kichwa. Ukitoka ukifika nyumbani pale, hujui kama utafika. Pale ilikuwa nyumba za mwarabu. Mwarabu asema sisi twaende zetu. Kumbe ni urongo, hakuna chakwenda zao, ni wananachi. Wana barua zao na uhuru tulipopata, twaambiwa kila mtu atakwenda kwao. Yule aliyejiandikisha mwananchi ni mwananchi. Basi, munasikia hivyo? Mimi nawambia kweli.

**Com. Zein:** Mzee wangu sasa tumekuelewa, iko jambo lingine ungetaka kusema zaidi ya majimbo?

**Mr Phillip Poka**: Ni hayo tu nataka waseme kweli

**Com. Zein:** Wamesema, Ahsante sana. Shukurani.

**Com. Kabira:** Ahsante sana Mzee Poka na tutamuita Mwenda Kombe. Ako? Hayuko. Samson Mwandime, ata huyo hayuko. Na Verity Juda, Margaret Kombo, Doreen Ngori , Caroline kategwa, Betty wakio , Kasini Maku , hawako, Justus Mwafiso, uko? Ahsante.

**Justus Mwafiso**: Kwa majina yangu naitwa Mwafiso. Maoni yangu ni kwamba, jambo la kwanza twataka majimbo, maana haya malalamishi yote ya-kuja kwa sababu ya utawala ambao haukuwa sawa. Wakati ule tulikuwa twasema, "Rais Juu Juu Zaidi," kumbe tulikuwa katika makosa. Zaidi hata akiuwa mtu. Anakuwa kama mungu. Hiyo ikatwe. Awe Rais na wabunge wawe na mamlaka zaid. Rais akiwa na makosa ashtakiwe.

Na wao wanyama wanaoitwa ndovu hawa wanakuja wanakanyaga mashamba zetu. Na ng'ombe zetu wakikanyanga, tunaenda tunakatwa faini, elfu moja, elfu mbili, elfu tatu. Kwa hivyo, tunataka mnyama ndovu akikanyanga shamba wale watu wa wanyama washtakiwe. Ndovu akiuwa mtu, alipwe kama milion nne. Hiyo ndio dhamani inayoweza kupooza wazazi roho. Sio elfu tharathini, ni kitu gani hiyo? Hiyo ni kama mapeni tatu.

Lingine ni kwamba jamii zote za Taita Taveta ziwe na mamlaka ya ardhi. Mtu asitoke nje kununua ardhi kwetu. Tukatae. Nafikiria tukiwa na majimbo, ndio jambo hilo litatatuliwa. Kwa hivyo, yangu ni hayo machache.

**Com. Prof. Kabira:** Okey Ahsante sana Mzee Justus. Na huyo mwingine ni Festus Kindambi, ako? Mkaluma Kushushu, Benjamin Ndumbu, Benjamin ako? Wewe ni Benjamin? Eh Okey Ahsante.

**Benjamin Ndumbu:** Commissioners na wananchi wote na-wasalimia. Mimi sina mengi kwa kuwa yale yalikuako yalisha-zungumzwa, lakini nilazima sisi kama wananchi tudhibitishe yale ambayo yanatuhusu sisi.

Jambo la kwanza, ningelisema ya kwamba tunataka mipaka ya nchi yetu ya kitaita irudishwe mahali ilipokuwa. National Park ni lasima tuililie kwa vile sisi tunapata mateso mengi kuhusu mifugo tuna ambiwa watu wengine tuende mahali fulani, na Kuna wengine ambao hawajiwezi. Ardhi yao iko hapa karibu tu, lakini hatukuweza kupewa ingawa mwanya kidogo tu wakuweza kuruka na kurudi. Hiyo ni tatizo moja. Hapo, hapo, tukitazama, sana tutapata ya kwamba hao jamaa walitundanganya kwa kweli ili tuwe kitu kimoja watunyanyase. Tafadhari sina mengi zaidi isipokuwa yangu ni hayo tu. Mengi yamesemwa.

**Com. Prof. Kabira:** Ahsante sana Benjamin. Utaandika jina tafadhari. Ahsante. Na Juda Mwaghala? Uko?
Ahsante.

**Juda Mwaghala:** Hamjambo? Tumeshukuru sana kwa kufika hapa kwa shida ambayo ni ya Katiba. Hii Katiba

mwazungumza mambo mengine , mambo mazuri sana. Lakini kitu ningeomba ni kimoja. Sisi watu wa hapa tuamue kitu tunapigania ni kimoja. Kama ni majimbo, tuseme ni majimbo badala ya kupoteza wakati kuongea mmoja mmoja. Tupatie wageni waliokuja nafasi waende waitafutie maanake kama ni jimbo moja moja, tumalize kama ni majimbo ni majimbo. Na hiyo ndio tunataka.

Kitu kingine ni hawa wanyama. Wanatutesa sana kwa sababu wametunyima haki sisi wanadamu. Sasa tunaona ajabu serikali haituangalii.

Pili, kitu cha mwisho kabisa ningeona heshima ya kwetu irudi kama zamani ya mababu zetu. Wakati huu, heshima imekwisha kwa wakubwa wetu. Hata watu wakiitwa hawaji kwa mkutano. Kulingana na sheria zile ambazo ziko sasa. Zamani wazee wetu walikuwa na mila zao. Mtu akikosa kwa mkutano, huwa analiwa kitu kidogo, kama mbuzi analiwa. Hawa watu walikuwa wanaogopa. Lakini sasa watu hawajali wanaona tuko uhuru hata wakiitwa kwa mkutano hawatoki dio mnaona kusudi watu wengine wamekuwa wachache sababu jambo hili ni jambo tulikimbilie sote, nila kutufaa. Lakini sasa tunaona ajabu. Kila mtu akiitwa, anaenda shambani. Pale watu wanaitwa, hawaendi. Kwa hivyo kama sasa mkisikia ni vita, sisi wale watu ambao tumekunja ndio tunaumia. Wale ambao wako pale, hawaumii. Sasa kitu kidogo silaha za kutulinda sisi mnatuona wanyama tunapigania tumenyang'anywa uwezo kabisa hatuna cha kutulinda, tunategemea serikali. Mtu akipigwa na ndovu, tunakimbilia serikali. Sisi hatuwezi pewa nafasi kidogo angaa tukawesa kupewa kidogo kama silaha ya kujilinda nyumbani. Silaha kama ni kupewa, waturudishie zile silaha zetu za zamani zile za sumu kama mnyama anakuja, ni sumu kama ni bunduki watupatie bunduki maanake kwa sababu kama fibo hii nyumbani italida nini sasa?

Tatu, pombe naona inapiganiwa sana na wazee wangu. Pombe hatuikatai, pombe ni nzuri sana lakini ilikuwa ni nzuri wakati wa babu zetu. Lakini wakati huu sasa, ukiangalia hawa wazee, kitu wanaomba ni kwamba pombe, vitabu ikubaliwe, ni sawa. Lakini watoto wote wamekwisha maanake hapa hakuna wazee wanakwenda usiku. Watoto wameanza kwenda usiku. Hii pombe, kama vile ilikuwapo hatungefungiwa lakini tu sifunguliwe, hata hiyo ni biashara ya mtu binafsi. Hiyo mimi sioni kwamba ni mzuri. Hapo tunajiwekea kitanzi sis wenyewe sisi. Kwa hivyo mimi sina mengi ya kuzungumzia. Yamezungumzwa mengi sana. Yangu ni hayo tu.

**Com. Prof. Kabira:** Okey Ahsante sana Mzee Juda. Huyu mwingine ni Reuben Mwashuke, Margaret Isaya.

**Margaret Isaya:** Nashukuru sana kwa wageni wetu siku ya leo kwa maana wametusaidia kuja hapa. Na maoni yangu mimi katika moyo wangu tuna mashamba yetu sehemu ya juu lakini shida ni barabara kwa maana hata tukiwa na mizigo, tunashindwa kubeba kwa kichwa. kwa hivyo kama ingewezekana, serikali ikaweza kutusaidia kwa mashamba yetu ya juu tukapata bara bara. Mimi ni Margaret isaya Mwakesho.

**Com Prof. Kabira:** Ahsante mama. Jiandikishe. Janet Mwalimwo hayuko, Ibrahim Mwalimboro, ametoka. Marita

Mwajuma hata huyo hayuko.  Suzie Mwachari, ako? Okey

**Suzie Mwachali:** Commissioners na watu wote nimewasalimia kwa jina la Bwana. Mimi kwa majina ni Suzie Mwachari. Mimi nilikuwa na pendekezo moja. Limetajwa lakini nimeona nilisititize. Pendekezo langu ni juu ya wale wanoachwa wajane. Mimi nikiwa mmoja wao. Sisi, bwana zetu wanafanya kazi serikali, wanakufa kabla hawaja retire lakini kitu tunapatiwa ni kwa miaka mitano. Tuna-achiwa watoto wadogo hata wengine hawaja soma. Tunapata shida. Ningeomba kama ingewizekana tuwe tukisaidiwa tusomeshe hawa watoto, tupate hiyo kitu hata kama ni kidogo nafikiri mpaka mwisho wa maisha yetu.

**Com Prof. Kabira:** Ahsante sana mama Suzie. Naomi Nyambu, hayuko? Mwambuli, Justine Mbololo.

**Justine Mbololo:** Commissioners na wananchi hamjamboni. Basi kwa majina yangu ni Justine mbololo na nilikuwa na pendekezo moja nilitaka niongee juu yake kidogo. Tumeona kwamba katika hii hali tunaishi, serikali kidogo imeachilia kama haifanyi kazi vile inavyotakikana na hasa upande wa kisheria. Sasa nilikuwa na-pendekezo kwamba serikali iwe na wakili ambaye atakuwa anatetea wanyonge ama iwe kwamba kila mtu ana haki ya kutafuta wakili. Hii ni kwa sababu kwamba mambo mengi yanatokea, mtu ananyanyashwa lakini ikifika kotini, yule aliye kunyanyasa hutamuona, utapata wakili wake na mambo yatageuzwa hivi na vile na kesi inapotea. Kwa hivyo kila mtu awe kwamba anaweza kutafuta wakili au kuwe na wakili wa serikali.

Halafu ya pili, ninataka kidogo kusisitisha kuhusu mambo ya kuharibu wasichana. Kisheria, siko hizi naona kama hali ya kitamaduni imeachwa kidogo na nilikuwa nasititiza kwamba mtu yeyote ambaye atamharibu msichana wa mwenyewe atakuwa na jukumu la kumtunza mtoto mpaka amalize masomo. Maana imetokea saa zingine ni mtu mwenye mali, labda anaharibu mtoto wa shule halafu anaachana na yeye tu hivo hivo. Sasa mtoto huyo atakuwa labda atakosa malezi ndio unapata watoto wakuranda randa ovyo.

Halafu latatu nilitaka kuongeza juu ya elimu kidogo. Serikali ni kama haiangalii maslahi ya wananchi. Watu wengi wamesoma lakini hakuna kazi. Kwa hivyo nilitaka kuongea juu ya mtu yeyote yule atayesomea katika shule ya serikali, baada ya masoma atufutiwe kazi na serikali.

Halafu ya nne ni kuhusu hawa ma-chief, Subchief na DO. Wasiwe na ruhusa ya kuamua kesi ya uhalifu. Maana inatokea uhalifu inafanyika . Mshukiwa anashikwa ama muhusika lakini akifika kwa chief, mambo hayo yanaishia hapo hapo. Sasa ni kama koti hazifanyi kazi zake kama vile inatakikana. Kwa hivyo ma Chief, DO wasiwe na ruhusa ya kuamua kesi za waharifu.

Halafu na la tano ni kidogo limeguziwa mara nyingi kuhusu hizi mbuga zetu. Nilikuwa ninasititiza hivi, mtu yeyote akiuwawa na mnyama wa pori iwe kama sheria ama iwekwe kiwango fulani ambacho atalipwa badala ya vile watu wanavyo lipwa. Maanake hii idara ya wanyama pori inalipa kulingana na vile imejua. Mtu amepoteza maisha yake,watu wake wanalipwa elfu thelathini

ambazo hazitoshani na maisha ya mtu. Kwa hivyo, wawe na kiwango fulani na isiwe chini ya million tano. Kama nimesikia mwingine ameguzia hilo kidogo. Maanake pesa haziwezi kulinganiswa na maisha ya mtu. Kwa hivyo, kiwango hicho kisiwe chini ya million tano.

Halafu la sita ama la kumalizia, kuna hizi kesi sinatokea sana sana. Mtu anapora mali ya serikali. Mwalimu labda anakula pesa ya shule halafu badala ya kuchukuliwa hatua vile inatakikana anakuwa transferred. Hiyo pia serikali ingilie. Iangalie mambo hayo. Nafikiria hayo ndiyo mapendezo yangu. Ahsanteni sana

**Com. Prof. Kabira:** Ahsante sana Justine. Is there somebody who is back? Tulikuwa tumekuita kwa hivyo tunakupatia huu wakati.

**Ibrahim Ibolo:** Ahsante sana Commissioners ambao mmekuja hapa na wananchi ambao mmehudhuria. Tumefurahi, ninawakambisha, karibuni. Langu ningetaka kutoa maoni yangu kwamba….?.

**Com. Prof. Kabira:** Na tafadhali taja jina lako.

Jina langu ni Ibrahim Mwaliboro. Ningependa kutoa maoni yangu hapa kidogo. Langu la kwanza ni kusema kwamba hii National Park iko hapa, mahali inapo pakana na wananchi, wananchi waweze kufaidika nayo kwa sabau iko hapa karibu na sisi, wananchi ambao wanapakana waweze kufaidika. Kwamba hii National Park ambayo iko hapa, pesa ambazo zinazo kusanywa hapa, ndani za watalii, za hotel na wale ambao wanafanya kuuwa wanyama na wanauza, wanafanyia nini hizo pesa? Hizo pesa zote huwa zinaenda katika serikali kuu na sisi hapa katika reserve, wananchi wa hapa huwa hawapatiwi hata single cent. Napendekeza hizo pesa hapo ndani ambapo zinachukuliwa katika hizo gate za National Park zikusanywe, zigawanywe nusu kwa nusu katika county council sababu county council ndiyo inaangalia wananchi wa hapa.

Pili, ningependa kwamba hii National Park ilikuwa na Game Reserve na sasa hiyo Game Reserve imeisha. Imekuwa ni National Park. Ningependa hiyo Game Reserve irudishwe kwa county council. Hotel ambazo ziko hapa ndani, kama hii Voi Safari Lodge, tungependa nayo kila kitanda kiko pale ndani kiwe ni sheria kwamba half of that iwe inapeanwa County Council.

La tatu, nataka uwezo wa Rais upunguzwe. Nikisema mamlaka ya Rais ipunguzwe ni kwamba sheria, jukumu la sheria la watu wanasheria, liwe na uwezo wa kuhukumu kesi bila kupitia kwa Rais. Uteuzi wa mwanasheria, tuseme kama Wako, tunataka ateuliwe na wanasheria wenyewe.

Nne, rasilmali yetu kama madini, ushuru wao uwe unalipwa katika serikali kuu. County Council haipati hata single cent. Ushuru wake tunaomba kupeleka kwa County Council nusu kwa nusu.

Tano, upande wa pension, hata nyinyi mko ma-commissioners mnataka mki-retire mnataka pesa. Nataka pension ingie kwa Katiba. Panapokuwa watu wawili, bibi na bwana, mmoja anapoanza kumwacha mwenzake, nataka yule ambaye ameachwa ale pension mpaka afe. Na yule mwingine anapokula pension mpaka afe, ile miaka mitano iwekwe kwa watoto wake mpaka ile pension imalizike.

Sita, malipo ya wanyama wa polini tunaona kwamba hii serikali yetu imechukuwa mnyama kuwa very important kuliko mwanadamu na Katiba hii yetu ndio tunataka iingie kwamba mwananchi ahesabiwe ni very important kuliko mnyama. Kwa sababu mwananchi anapouwawa na mnyama kama ndovu, huwa analipwa elfu thelathini na unapo-gongwa na gari, unalipwa hata million moja. Je, kwa nini mwananchi ahesabiwe chini kuliko mnyama? Kwa hivyo, tanataka Katiba yetu hii imuhesabu mwananchi kwamba anafaa zaidi kuliko mnyama na ningetaka mwananchi akiuwawa na ndovu alipwe millioni moja. Hayo ni maoni yangu kwa sababu kama hiyo thelathini ingekuwa iko chin, hiyo millioni itatoka kweli?. Kwa hivyo lazima tuombe million moja ili wajue kwamba wachunge wanyama wao.

Saba, tuna shida. Naomba wananchi msikize kwa sababu kila mmoja ana jukumu la kutoa maoni yake. Na mkijua kwamba tuko katika jumba la mungu, lazima tuiheshimu maoni ili yetu yapate kuingia vizuri.

Ardhi yetu sisi kama watu wa pwani, usingizi hatupati kwa sababu tumenyanyaswa zaidi. Ardhi, yetu sehemu hii mipaka yetu imesukumwa mpaka imeingia ndani upande wa Mtito Andei. Tumesukumwa mpaka tumeingia ndani Mwakina ndoto. Napenda mipaka yetu irundi pale pale ilipokuwa na baada ya hivyo hii ni mpaka iheshimiwe sababu kutoka enzi za babu zetu kila mmoja alikuwa na mpaka wake. Nataka Katiba ingie ndani. Kwamba ardhi yetu, wale ambao wamekaa katika ardhi zetu tutakuwa tunawatoza ushuru kama wengine.

Nane, tunapendekeza uchaguzi wa mwaka huu ufanyike kwa Katiba mpya ili kusije kukakuwa na ulaghai wowote. Uchaguzi wa mwaka huu ufanyike kwa Katiba mpya kwa sababu hatutaki ulaghai wowote ndani ya huu uchaguzi. Kwa hivyo tunasema Katiba mpya itekeleze wajibu wake.

Tisa, napendekeza utawala wa mfuno wa mkoa yani majimbo. Nikisema hivo ninasema kwamba tunapokuwa na utawala wa majimbo, ni kuonyesha kwamba hapatakuwa na penyezo lolote la kugeuza Katiba bila majimbo yote kukubaliana.

Kumi, napendekeza rasilmali zetu, za serikali zigawanywe kisawasawa katika mikoa yote kama barabara, shule, ukulima, mambo hayo yao yanachunguzwa kikamilifu, ili tupate pesa kisawa sawa.

Kumi na moja, tunapendekeza uteuzi wa ma-chief, uwe mkononi mwa wananchi. Na tunapenda ma-chief wawe wanapigwa

transfer kwa sababu anapokaa miaka kumi ama miaka ishirini mahali pamoja huwa anaumiza sehemu ile, lakini akiwa anapigwa transfer huenda akapata maarifa pahali pengine.

La mwisho, Haki ya walemavu: Hapa tunawalemavu wengi. Ukisema walemavu, kuna wengine ambao walipata ajali na hawawezi kutembea, na kuna wengine walizaliwa hawasikii, na kuna wengine walizaliwa na mama zao wakawa paralyzed, hao wote ni walemavu. Tunataka wapewe haki zao za elimu, mahali mtoto yeyote yuko mlemavu, apewe elimu bure, aangaliwe na serikali. Na misaada wapewe. Kwa hayo machache, Mungu awabariki.

**Com. Prof. Kabira:** Asante! Lakini Bw. Ibrahim… Si ni Ibrahim

**Mr. Ibrahim:** Yaah.. Councillor Ibrahim

**Com. Prof. Kabira:** Waweza kuchagua ma-chief na wafanywe transfer pia?

**Mr. Ibrahim:** Ma-chief tunataka kwamba wao ni watu wa administrative wanaweza kwendwa popote

**Com. Prof. Kabira:** Lakini, if you elect.. ukimchagua, waweza kumpelekea watu wengine wale Hawajamchagua?

**Mr. Ibrahim:** Kwa mfano nasema hivi, wale ambao tunataka ma-chief, wakichaguliwa, watakuwa wanachaguliwa kwa miaka mitano. Ikiwa hatufai tunamtupilia mbali. Sawa hivyo?

**Com. Prof. Kabira:** Eeh.., hiyo ni sawa.

**Mr. Ibrahim:** Sio aendelee kukaa hapo tu na kuumiza mahali hapo, ikiwa miaka mitano imekwisha na hatufai, atolewe.

**Com. Prof. Kabira:** Atolewe, okay, asante Sana Bw Ibrahim. Na Suleiman Mwakichi, ako?

**Mr. Suleiman:** Kwa jina naitwa Suleiman Mwakichi. Napendekeza kwamba Rais wa nchi achaguliwe kila mkoa. Rais wa nchi atakapo omba kura, apate mikoa sita ndio awe Rais wa Nchi. Napendekeza waziri mkuu awe ndiye kiongozi wa shughuli

zote za serikali katika nchi ya Kenya. Pia achaguliwe na bunge la majimbo,afikishe majimbo sita ndiyo awe waziri mkuu.

Napendekeza kwamba Katiba hii iandikishwe kwamba mwanakenya yeyote ambaye ameajiriwa na shirika la umma ama la serikali akifikisha umri wa miaka hamsini iwe ni sheria ya mtu kustaafu.

Napendekeza pia wazee hawa wakisha staafu kwa miaka hamsini wasipewe chochote cha kuongoza mambo ya umma, wapatie nafasi vijana. Napendekeza kwamba wananchi wa Kenya,kwasababu hawajui Katiba na wengine wako kifungoni hivi sasa kwa sababu ya kutojua Katiba, twataka Katiba hii itakapotengezwa yule mfungwa apewe uhuru, ikiwezekana hata kwa mwezi mara moja kwenda kuangalia nyumba yake,kwa sababu ya kuchunga mambo ya ukimwi.

**Mr. Suleiman: (continous)** Napendekeza, wambunge ambao huchaguliwa wawe na vipindi viwili.Akichaguliwa mara ya kwanza, akirudi ya pili, ya tatu awache wengine nao wafanye.

Napendekeza kwamba mtoto yeyoye ambaye atazaliwa katika jamhuri ya Kenya na serikali ya Kenya itakuwa na haki ya kumpa kitambulisho. Serikali hiyo ya Kenya pia iwe na haki ya kumtengea ploti na imuandikishie kama ploti hii ni yake.Napendekeza pia kwamba sheria iwekwe mwananchi yeyote wa Kenya asiruhusiwe kuwa na ploti mbili.

**Interjection:** Maoni yake hayo

Jamaa ninaomba hayo ni maombi yangu, kama una yako utakuja hapa, unipinge nawe uzungumze yako.

Napendekeza kwamba vijana ama wanaume ambao wanamtungia msichana mimba, sheria hii isimuandame mwanamke peke yake kwa sababu mambo yoyote ambayo yanahusiana na utungaji wa mimba vitabu vya Mwenyezi Mungu kwanza vimekataa vinaa na hawa wote wamekubaliana na wamezaa mtoto kwa sababu ya makubaliano. Kama ni adhabu, yaende sambamba kati ya mke na mume. Na kama mwanamume huyu ametumia lazima yoyote kwa yule msichana ama kwa yule mwanamke na akamzalisha na akapokea ile mimba pasipo hiari yake, adhabu itolewe kwa mwanamume.

Napendekeza kwamba wafanyikazi wote waliooko wa umma wafanye kazi katika mikoa yao. Kwa sababu sisi wa pwani tumeumia vya kutosha hata kwa upande wa elimu. Utasikia kwamba mtoto ameanguka katika somo la kiswahili na kiswahili chatoka pwani, lakini kwa sababu tumechanganyika wanaokuja na kiswahili kingine mpaka watoto wetu wanaanguka mpaka lugha yetu tunayozungumza.Kwa hivyo tunapendekeza mwalimu akishaajiriwa, alegeshwe mkoa wa pwani. Polisi akiajiriwa, aregeshwe mkoa wa pwani askari tawala, askari wa majela, askari wa porini, wote waregeshwe katika mkoa wetu na wengine wapelekwe katika mikoa yao kufanya kazi katika mikoa yao. Kwa sababu ikiwa tutakua na shortage ya polisi tutajua kwamba kwa nini wapwani hatujaajiriwa. Tutakuwa na wazo na akili ya kujua kwamba sisi wa pwani hatuandikwi katika jeshi la polisi. Tuna haki ya kutetea. Kwa hivyo ni kila mfanyikazi, kila mwananchi wa Kenya akishahitimu, aregeshwe katika mkoa wake.

Kwa hayo machache nashukuru na hayo ni maoni yangu binafsi sijaingilia mtu yeyote, hayo ni ya kwangu, asanteni.

**Com. Prof. Kabira:** Okay, asante sana Suleiman. Na tutamuuliza David Maganga ako? Okay Donald Maganga. I'm sorry.

**Mr. Donald Maganga:** Jina langu ni Donald Maganga. Nimeandika mapendekezo yangu lakini ningetaka tu kusisitiza yafuatayo;

Kitu cha kwanza, ningetaka kusema ni kwamba Katiba ya Kenya iwe na utangulizi ambao una maadili ya wanakenya. Na maadili haya mengine yametajwa katika wimbo wa taifa na nasikitika kwamba ni wachache sana wanaojua wimbo wa taifa. Tukiuliza tuimbe saa hii utakuta watu wengi hawawezi kuimba. Mambo kama hayo ni kwamba tunatambua Mungu kama nguvu yetu.

Ya pili, tunatambua kwamba Kenya inastahili heshima, na Kenya vile ilivyo sasa ni kwamba imetumiwa kama pipa. Tunaenda

kuombaomba, mambo kama hayo yako katika wimbo wa taifa.

Halafu, ingine ningeomba iwe kama utangulizi ni kwamba Kenya haina vision, haina maono, Katiba yetu haielezi chochote miaka hamsini ijayo Kenya itakuwa iko wapi, tunatarajia Kenya iwe imekua wapi. Kwa hivyo tungependekeza iwe na vision Katiba yetu.

Katika umilikaji wa ardhi ningesema kwamba umilikaji wa ardhi vile ulivyo sasa ni kwamba tumeletewa mambo ya kigeni. Hivi vikaratasi ambavyo vinaitwa title deed, maoni yangu ni kwamba vitupiliwe mbali. Umilikaji wa ardhi urudi wa kimila vile ulikuwako zamani, kwa sababu vile imekuwa ni kwamba title deed watu wanaenda Nairobi na wananyakua ardhi, na wanauza na wanaendelea kujibilikizia mali na huku wanakuja kutunyanyasa katika hali nyingi. Kwa hivyo ningeomba kwamba uwe wa kimila. Wale ambao wako na ardhi ambayo haitumiki, wapokonywe na ipewe wale watu ambao wanaweza kuitumia.

Katika huduma ya serikali, tumekuwa na serikali ambayo haitoi huduma kwa mwananchi na hivi sasa serikali tu labda inakaa kwa sababu ya mashirika ambayo yanatoka nje. Wafanyi kazi wa serikali hakuna chochote wanafanya. Ningependekeza kwamba Katiba hii iweze kupeana civil servants nguvu, kama watakua ni wachache waweze kufanya kazi vile inatakikana. Na pia waajibike kwa wananchi labda tuwe na district council ambayo itakuwa inaangalia wafanyikazi kama hafanyi kazi kulingana na mahitaji ya wenyeji wa pale, sio kupigwa transfer ni kufutwa.

Ningependekeza pia viongozi wale ambao wanachaguliwa, wawe ni ma-councillors, wawe ni wabunge, kama haajibiki ipasavyo kulingana na wale ambao wamemchagua, aweze kurudishwa nyumbani kama ameshindwa na kazi. Kwa hivyo, isiwe mpaka miaka mitano ndio ati kura ifanywe.

Ningependekeza pia kuwe na limit ya umri ya watu hawa, kuanzia ishirini na moja hadi sitini na tano kwa councillor na mbunge. Kwa Rais, ningependekeza awe miaka thelathini na tano hadi sitini na tano.

Mahakama - vile ilivyo sasa ni kwamba mnyonge hana haki Kenya. Kumekuwa na walaghai kama ni wanasheria na nasikitika kusema kama mmoja yuko hapa. Wengi wamekuwa ni walaghai wananyanyasa wanyonge, ningependekeza kwamba Katiba iweke sheria kali za mwanasheria yeyote ambaye atanyanyasa mnyonge. Na pia kuwe na mahakama maalum ya kutetea wanyonge wale ambao hawana pesa. Na ikiwezekana, yale mambo ambayo yanahusiana na mila, na desturi za mataifa mbalimbali, kuwe na koti ambazo zitatatua mambo haya, koti ambazo zina husiana na mambo ya kimila na desturi kuliko vile mambo yalivyo kwamba mtu hajui mila ya kitaita na anakuja kutatua mambo ya kimila.

Halafu,mambo ya msaada kutoka nje. Imekuwa kwamba, viongozi wale walioko sasa, wanatumia mbinu hio pia kunyanyasa wananchi.Napendekeza kwamba msaada wowote ambao utatoka nje uwe umeidhinishwa na bunge sio mtu binafsi Napendekeza pia kwamba tumekuwa na Katiba ambayo mambo mengi tumeridhi kutoka kwa ukoloni na mambo mengi ambayo tunazungumza sasa ni kwa sababu ya wachache ambao wamepigania. Ningependekeza elimu ya uraia iwe ya kuendelea na ifadhiliwe na serikali sio tu wakati wa uchaguzi ama wakati wa mambo fulani ndio iwekwe, iwe ya kuendelea.

Ningependekeza pia kwamba zile wilaya na maeneo za ubunge ambazo zimeundwa kiharamu kwa sababu ya manufaa ya wachache ikiwezekana, Katiba hii ipeane uwezo wa kuzitupilia mbali zirudishwe zile wananchi watakazoamua. Na pia mipaka isiwe mtu mmoja ana uwezo wa kuamua kwamba mpaka fulani upitie pahali fulani ama kugawanya wilaya ama kugawanya kata. Mambo haya yalindwe na Katiba.

Ningependekeza pia, labda yangu ya mwisho kwa sababu nimeandika, Katiba iandikwe kwa lugha ya kishwahili na lugha za mama ili wengi waweze kuielewa. Asanteni.

**Com. Prof. Kabira**: Okey asante sana Bwana Donald. Ibrahim Kalamu from Gibran. Kalama ako?

**Mr. Kalama**; Ccmmissioner na mabibi na mabwana, nashukuru sana kwa maana wakenya siku hizi naona wamepata nuru ya majimbo, na majimbo ni kitu cha zamani sana, na marehemu Ngala ndiye aliye mwazilishi wa hii. Hiyo ni nuru ya hali ya juu sana

kwa wataita na wale wameweka akili zao katika majimbo. Majimbo ndiyo kitu hatuwezi kupika sima sufuria moja katika Kenya mzima. Mpaka tugawanye huku, hawa wapike huku na hawa ndiyo sima itaiva sio? Sasa naona hapo iko nuru na kwa sababu hiyo tena, naunga majimbo kwasababu sasa imepita miaka thelathini na tisa au arobaini, karibu miaka arobaini na hatujapata stakabadhi za kumiliki mashamba yetu hapa na hivyo tunakosa kwenda benki kuchukua angalau kitu kidogo tujisaidie.Unaona?

Kitu cha pili nataka kusema ni, unajua nchi hii yetu ya Taita ama Mbololo imezingirwa na mbuga za wanyama.Sisi tuko na sehemu kidogo sana sijui kwa nini. Pengine watoto wetu ndio watakuja uliza kwa nini hii ilitokea namna hiyo. Sasa hii tukiwa na majimbo, ni rahisi, naweza kupata stakabadhi zangu za mashamba hapa Mombasa kwa dakika moja, kuliko centralization huko Nairobi. Kwani huko Nairobi kuna nini? Na hii habari ya mashamba wakati title deed zimetokea watu wapewe nafasi ya kulipa stakabadhi za title deed polepole maana wengine sisi hapa tuko na mashamba pengine manne matano tupatiwe nafasi ya kulipa hizo title deed.

Kitu kingine ambacho mimi nilikuwa nataka kutaja hapa, wengi wamesema lakini pengine ni juu ya mbuga za wanyama. Hiki kifungu ninyi ni wasomi. Hiki kifungu cha kama ng'ombe wangu ameuliwa na simba ama shamba yangu imeharibiwa na ndovu kimefutwa nini? Manake siku hizi hatulipwi. Ninyi ni wasomi

**Interjection:** **(** inaudible **)**

**Mr. Kalama:** Kitu kingine ni juu ya ukulima. Serikali yetu kuanzia 1963 tunapambana na njaa hapa, ukame na nini. Mpaka dakika hii serikali haijashtuka, serikali ya Kanu haijashtuka kwamba watu wetu hawa, italea watu wa Kenya kweli? Ingefungua ingetafuta mbinu za kupata maji ya kunyunyizia mashamba kama hapa Mbololo, sehemu hii ya Mbalolo, miezi mitatu tu tunapata chakula. Unaona? Sasa kama serikali ingetupatia hasa maji, tungaliweza kufaidika hapa sana.Na mimi naunga mkono wale watu ambao wametangulia kusema hii habari ya watu wengine kuja kumiliki mali ya wataita hapa. Nafikiri haina sura nzuri hiyo. Sura

mbaya sana hiyo (**ululation**) Tunataka watu hapa hapa wenyeji wa hapa wamiliki mali yao. Sio mtu kutoka maili elfu mbili aje aridhi mali hapa. Hii ni dhalimu au dhuluma. Sina mengi sana lakini mengi yameshasemwa na majamaa.

**Com. Prof. Kabira**: Okay, asante sana mzee Kalama, na Priscilla Hezron. Priscilla ako? Hayuko. Henry Mabea?

**Mr.Henry Mabea**: Kwa majina mimi naitwa Henry Mabea. Ni mtaita. Kwanza nashukuru sana ma-commissioner na wananchi wote ambao wamekuja hapa leo.Nafikiri wamekuja hapa kwa sababu ya mfumo wa vyama vingi ambavyo huu mfumo wa vyama vingi ni juzi juzi tu tuliupata. Mbele ya huo mfumo wa vyama vingi tulikuwa na unitary government. Kwa sisi hapa, kwa wale ambao walikuwako wakati huo, hii unitary government ilikua inafanywa wanajua uzuri wake na ubaya wake. Uzuri wake ni kwamba ni wachache ambao wanafaidika eh! Ni wachache ambao wanafaidika ndiposa, ndio munaona katika jimbo letu la pwani, hakuna maendeleo yoyote yanafanyika, hatuwezi kulinganishwa na wale watu ambao wako sehemu za central province ama mahali pengine. Hiyo unitary government iliendelea kidogo ndio watu wakaona mwangaza tupiganie nini? Ambayo ndiyo sasa ninaona tunaenda kwa mfumo mzuri. Wakati huu kwa sababu sisi tumeachwa nyuma sana, maendeleo yote yanaenda mahali ambapo labda President yuko. Mahali kama hapa tulikuwa na president, unaona maendeleo inakuja pale, Na barabara zingine mara ingine yatengenezwa kwa sababu President anakuja pale. Siku akishapita barabara zinarudi pale pale, hakuna maendeleo inafanyika. Hivyo ndivyo mimi naona napendelea majimbo, kwa sababu majimbo tutapewa mamlaka ya kuunda serikali yetu hapo halafu ishirikiane na ile central government.

Tuwe na Prime Minister, alikuweko lakini kwa nini alikwenda? Kwanini ilifutiliwa hiyo Katiba ilipotiliwa. Si alikuwako? Kulikuwa na Prime Minister wakati tulipata uhuru. Unaona vipengele vingi vimeondolewa ili wachache wafaidike. Kitu kama hicho ndio sisi hatutaki na ndio sasa sisi tunataka majimbo ili na sisi tufaidike ki-coast. Mambo mengi yamefanyika ukiangalia hata kama universities, jamani? Hatuna hata university moja, mm!! Halafu tunasikia wengine wanasema bado watu wa coast hawako tayari kwa university, ama hamkusikia hiyo? Ilikuwako.Hicho ni kilio, na ni siku gani sisi tutapata university? Mombasa ingekuwa city zamani sana lakini leo juzi tu ndio ikawekwa city baada ya Kisumu. Eh, kweli hapo kuna haki hapo? Hakuna. Mimi mwenyewe najibu hakuna. Sasa rasilimali nyingi zetu zinaenda kwa central government. Nafurahi sana kwa wale wote ambao wamekuja hapa ama wamesikia ama wakawa na nia ya kusema tuunde majimbo. Wale nawapongeza, nafikiri Mungu

atawabariki. Katiba hiyo iende hivyo, twataka majimbo. Tukipata majimbo, mengi tumetengeneza. Kwa sababu kama tumepewa hiyo kitu, sasa tumeanza kuunda, sasa itakuwa kivipi? Rasilimali zetu ni nini, tutakuwa namna gani? Itakuwa rahisi kueleana badala ya kueleana na mtu kutoka Nairobi. Mali zetu zinaenda na nashukuru kwa sababu ya mfumo wa vyama vingi sisi wananchi tumepata mkoa kama huu ili tutoe maoni yetu na hayo maoni yetu ndiyo itatusaidia. Kijitabu hiki kinatuuliza Katiba inatengenezwa na nani? Kumbe ni sisi, kama jambo moja ni kwamba hii Katiba ya kimajimbo ikianza kama kuna marekebisho kwa sababu sisi ndiyo tumeiunda, tufanye nini, turudishiwe tena tuwaulize ama watueleze ni wapi, kipengele kipi ambacho kingetaka kubadilishwa. Wapenzi, mimi naunga mkono wa majimbo na tuendelee na majimbo.. Asanteni.

**Com. Prof. Kabira:** Asante sana Bwana Mabea, na Judy Mwagola ako? Okay

**Judy Mwagola:** Kwa makamishna wetu ambao mmekuja hapa siku ya leo, na wananchi nyote ambao mmekuja hapa siku ya leo kutoa maoni yenu, mimi kwa jina ni Julia Mwagola. Mimi nishatoa karatasi yangu nikampatia dada lakini nina kitu kimoja ambacho nataka niongezee, nina mambo kama mawili, matatu ambao nataka niongezee.

Mimi nazungumza juu ya nominated councillors na nominated MPs wote Kenya nzima hasa kina mama. Mimi nashukuru serikali yangu kwa sababu ya kuchagua nominted councillors na nominated MPs. Kwa hivyo mimi kwa maoni yangu ninaomba iendelee. Kwa sababu nominated councillors au nominated MPs…

**Interjection by Com. Prof. Kabira:** Tumupatie nafasi kwa sababu hiyo ni maoni yake, si ndiyo?

**Judy Mwagola:** Na hapa wakiwa akina mama ningependa wachaguliwe kwa wingi kwa sababu tunaona hawa elected councillors hata akiwa mume kusema kweli, wanatabia moja ambayo hata kina mama wengine wameshatunununikia sisi kama nominated councillors wa kike, Ukienda kwake, kama una shida zako, anakwambia, usiniambie hapa nyumbani au usiniambie sasa, ningojee wakati mwingine tuagane tukakutane mahali fulani, halafu ndio unielezee shida zako. Lakini, mimi si kama

ninajisifu, na wala si kwamba ninasifu nominated MPs au nominated councilors. Nominiated Councillors au nominated MPs, yeyote ambaye ni mama hata kama umekuja nymbani kwake unamweleza shida zako hapo hapo hata kama mmekutana njiani unamweleza shida zako hapo hapo na anakujibu hapo hapo, hawezi kukwambia ati ningoje tukutane kesho au tuende tukakae mahali fulani tuzungumze, halafu ndio nikujibu maneno yako. Kwa hivyo, mimi maoni yangu ninaomba nominated MPs, nominated councillors hapa akina mama waendelee kuchaguliwa.

La pili, mimi namuunga mwenzangu mkono ambaye amesema kwamba, councilor ye yote au MP yeyote si mama si mwanamume ye-yote yule achaguliwe mtu wa makamu kuanzia miaka thelathini, na miaka sitini na tano. Kwa sababu hao ni watu ambao ni watu wazima walio komaa na ni mtu ambaye anaweza kufanya kazi yake bila wasi- wasi, hana mchezo kwa sababu ni mtu mzima mwenye akili zake.

Jambo lingine ambalo mimi nimelikataa kama kiongozi na tena kama mama, pombe, kusema kweli pombe inarudisha maendeleo nyuma. Na hapa mkiangalia, kama hapa kwetu Taita utakuta watoto wengi wanakaa barabarani. Mama zao na baba zao wamekwenda mashambani, utakuta watoto wa kiume wamekaa barabarani wanavuta sigara hata zile sigara za sonyo wanavuta tu barabarani na mamake na babake wamekwenda shambani kulima na huyo huyo mtoto ndiye huyo huyo atakuja kutafuta chakula nyumbani, na huku barabarani alikuwa anarandaranda haji kumsaidia mzazi wake kulima. Na akitoka hapo anaenda kunywa pombe. Pengine yeye kwa bahati amebahatika, amekwenda akapata kibarua kwa mtu. Anafanya kile kibarua na zile pesa ambazo amepata hatazipeleka kule nyumbani aende akasaidiane na wazazi wake pengine nyumbani kulikuwa hakuna sukari, atakwenda kunywa pombe peke yake, na akija nyumbani anaanza kumfanyia mama yake fujo pamoja na baba yake anatafuta chakula, na hali yeye mwenyewe hana kazi yeyote aliyefanya. Kwa hivyo mimi kama kiongozi, mimi kama mzazi, tafadhali nimekataa pombe zisirudishwe. Pombe zifutiliwe mbali.

**(Noisy interjection)**

**Judy Mwagola:** Kwa hayo machache nafikiri nimemaliza, Asante sana kwa kunisikiza.

**Com. Prof. Kabira**: Okay, Asante sana mama Julia. Tuna Prudence Malamu? Tafadhali tumsikilize

**Prudence Malamu:** Kwa makamishna wetu, na wananchi. Mambo mengi yamesemwa na tukisema tukirudia naona tutamaliza saa. Isipokuwa pale ambapo hapakutajwa, ndipo nitataja. Ni juu ya mashamba yetu, Title deeds. Ningeomba serikali yetu itukubalie sisi akina mama, niko na bwana nyumbani, Title Deed ikija yeye ndiye anatia mkono peke yake, na kesho kukitokea jambo lolote mimi sina kitu cho chote cha kuonyesha hili shamba ni langu. Sijui kama leo kina mama mwaweza kuniambia una uhakika wa hilo shamba unalima? Kesho ukipigwa, wewe wakimbia moja kwa moja unaenda, kwa sababu huna shamba, Ningeomba serikali yetu ikubaliane na kina mama hizi Title Deeds zetu ziwe zinakuja, tutie mkono sote ni bwana na bibi. Tena tuangalie kina mama tumenyanyaswa kwa njia nyingi, bwana ametuoa wanawake watatu au wawili. Katika hii Title Deed, tutafanya aje? Mimi ni bibi wa pili, nitatupwa na tumeishi pamoja? Nyumba pengine tumejenga town, tunatia sahihi sote? Kina mama tumenyanyaswa kwa njia nyingi na hata ingawa tuwazuri sana tuombe serikali yetu itusaidie, itupe ruhusa tuungane na wanaume wetu. Tumeambiwa hapa rasilimali itagawanywa kama bwana akifa, je mimi bibi wa pili na watoto wangu nitapewa shamba wapi kulima na watoto wangu, kama sikutia sahihi kwa ile Title Deed? Tufikirie sana kina mama tusiwe watu rahisi kucheka tu na kupiga makofi. Tunatupwa mbali sana. Namukubali kwa hii serikali yetu hii tunayoiunda, sisi wenyewe Katiba yetu ,tunaunda Katiba ili itusaidie katika maisha yetu. Ningeomba wanawake tuunge mkono jambo hili la kutia sahihi Title Deed, Shamba iwe ni sote au nyumba imejengwa iwe ni sote na watoto wetu.

Jambo lingine, ni watoto wetu wanapata mimba kwa bahati mbaya, na tunaletewa kina nyanya nyumbani tunawalea vizuri na tunawapenda, lakini mkubali msikubali watoto hawa baba zao wengine ni watu wakubwa, maofisi kubwa kubwa. Na wewe unang'ang'ana hapa na watoto huna chakula, hana nguo, na babake ni mtu mkubwa, tufikirie tufanye aje? Ile ilikuwako zamani kwa Katiba ile natumaini ni waume walisema kusaidia hao akina mama, mtoto akizaliwa mtu amulee mpaka miaka kumi na nane. Lakini ilipoonekana kwamba akina mama, sisi hatuko nyuma ya hilo neon, likatupwa likaonekana kumbe twajitia mashakani sisi wenywe. Likatupwa, je kina mama tutaendelea kulea watoto namna hii?

**Com. Prof. Kabira:** Kwa hivyo unasema tuirudishe?

**Judy Mwagola:** Mimi ningekubaliana turudishe hilo neno, watoto wawe wakilipiwa

**Com. Prof. Kabira:** Ni Affiliation Act? Si hiyo?

**Interjection:** Yaah

**Speaker:** Okay, irudishwe? Inaitwa Affiliation Act. Ni hiyo unasema tuirudishe?

**Prudence Malamu:** Eeh, tuirudishe hiyo Affiliation Act. Jambo lingine la mwisho, tumesahau wenzetu wale walio jela, wafungwa, Kwa maoni yangu ningeomba tuwape ruhusa wapige kura kwa sababu ni wenzetu. Kwa nini tumewafungie nje? Kama kura zinakuja, ningeomba tukubaliane hata wafungwa pia wana maoni yao wameenda pale kwa sababu ya makosa pengine wengine wametubu na wanaweza kuwa na maoni mazuri na kuweza kuchagua kiongozi mzuri. Ningeomba nao wapewe nafasi ya kupiga kura sio kama siku hizi mtu akifungwa amekwisha kabisa hata hawezi kufanya chochote kwa nchi yake.

Na jambo hilo lingine ni juu ya walemavu, ningeomba serikali ifanye Act yoyote ya kulinda maisha ya walemavu, hasa walemavu wa wanawake. Wengi wanatendewa mambo mabaya na hakuna Act yoyote ya kuweza kumsaidia huyu mlemavu mwanamke. Unaweza kukuta.. nilikuta mwanamke mwingine akibebwa kwa wheelbarrow akapelekwa msituni ku-rape-iwa. Ningeomba serikali yetu tunayoendelea nayo au Katiba yetu iandike kipengele cho chote cha kumulinda huyu mlemavu, mwanamke hata mwanaume, kwa sababu wengine wanatendewa vibaya. Kuwe na kifungo fulani ukimpiga mlemavu kuwe na kipengele cha kusema wewe utafungwa kama miaka miwili au mitatu kwa sababu hawa wenzetu hawajiwezi. Nasingetaka kurudia kwa sababu mengine yamezungumzwa, ningetaka niishie na hayo kwa wakati huu.

**Com. Prof. Kabira:** Asante sana. Mama Prudence. Na tunauliza Charity Kalu, ako? Okay,

**Charity Kalu:** Mimi ndiye munayesikia naitwa Charity Kalu.

Yale yote nilikuwa nasema nitakuja sema yamesemwa na wenzetu lakini nitarudia moja tu yavishasemwa. Sisi wanawake kunyanyaswa, tunanyanyaswa kwa mengi. Mtoto akiwa na mimba bwanangu ananiambia ni wewe, ni akili zako. Mtoto akifeli shule mtihani ananiambia huyo ni mtotowako, hawa hawa wabaya wabaya ndio mimi napewa. Kwani mimi naweza kutuma mtu afanye mabaya? Twanyanyaswa hapo, sasa hayo yote kama yangewezekana hayo yalisemwa ati mtu akiweka msichana wa mtu mimba, amulee hiyo miaka kumi na nane ampe riziki.

Sasa nina lingine tena juzi juzi. Bwanangu alifanya kazi ya vita wakati wa wabeberu, vita vile vya 1944, akaacha akapumzika sasa yuko, ndio hapo sasa kumekuja form za kujaza wapewe malipo yao. Mpaka sasa amejaza mpaka sasa sijui hizo form watalipa, hawatalipa hayo mambo nayo nimekwisha shangaa naye kwani watu hata serikali wanasema uongo. Hayo yaangaliwe kama watu wanalipwa na bwanangu alipwe.

Asanteni.

**Com. Prof. Kabira:** Okay, andika jina lako tafadhali. Asante sana mama Charity Kalu, na Beatrice Taabu, Ako? Beatrice Taabu hayuko? Okay, Harun Mwaniki?

**Harun Mwaniki:** Ma-commissioners, na wote waliohudhuria nawasalimu. Mimi nimeandika yangu sijui munataka niyasome ama munataka niwapatie? Niyasome?

**Com. Prof. Kabira:** Ni sawa tu lakini ungetupatia summary points.

**Harun Mwaniki:** Okay. Ya kwanza, nimesema hivi, ile inaitwa parliamentary service commission ningependelea iwe scrapped kwa sababu imewafanya hawa wabunge na wananchi wawe kama hawako pamoja tena. Kwa sababu mambo yakiwa ni yao, wanajipitishia wenyewe kuonyesha sasa wamekuwa wachoyo. Jambo likiwa ni lakufaidi wananchi, hapo ndio wanajua upinzani, wanaanza kupingana hapo halafu hata halitapitishwa. Kwa hivyo na ile kujilindikizia malipo mengi, hiyo yote ni uchoyo.

Jambo la pili ni hizi national parks. Imechukua ardhi yetu kubwa sana hapa Taita. Ningependekeza kwamba sehemu ingine, at least a quarter of it, irudishiwe wananchi. Na wale ambao wana mashamba makubwa kama hizi sisal estates, and the like, wasiruhusiwe kuwa na title deed ya hizi vitu badala yake wawe wamei-lease wachukuliwe kama wamei-lease halafu wawe wakilipa land rent kwa county council. Halafu majority, ama wengi wa wafanyi kazi wa serikali ambao wanafanya kazi katika district hii, wawe wanatoka hapa hapa. Kwa sababu experience imetuonyesha kwamba wengi kwa hivi sasa wanatoka sehemu za nje.

Na wawe wakichaguliwa kama ma-councillor kwa muda wa miaka mitano mitano, ili yule hapendelei maendeleo aondolewe pale. Nafikiri yangu ni hayo.

**Com. Prof. Kabira:** Asante sana bwana Mwaniki. Na tunamuuliza Jemimah Mabruk.

**Jemimah Mabruk:** Commissioners na members of public, hamjambo? Yangu nimeandika katika form of memorandum. Lakini nitatajia tajia kidogo kabla sijai handover. Nafikiri leo ni bahati ama mwaka huu ni bahati vile mwenzangu mwingine ameongea, tuseme ni kwa sababu ya mfumo wa vyama vingi ndio tukajua mambo ya Katiba kumbe inaandikwa na mwananchi. Na kuzungumza juu ya Katiba, nafikiri si wengi wanajua Katiba, hata hivi tunavyorekebisha hatujui tunarekebisha nini. Kwa sababu hiyo katiba is not accessible to mwananchi. Mwananchi wa kawaida hajui Katiba ni nini, ama mnajua? Ni wachache sana, na kama itakua accessible ama itafikia mwananchi wa kawaida, cost yake itakua kiasi gani. Kwa sababu saa hii ukienda

ukitaka kujua mambo ya Katiba labda unaambiwa uende government printers, na ni wachache ambao wanaenda hapo. Ama ni wachache ambao wanajua hiyo ofisi. Na unasikia labda ina-cost mia sita ama zaidi ya mia tano ama elfu moja . Kwa hivyo mimi pendekezo langu nasema hiyo Katiba ambayo tunatengeneza wakati huu, iwe accessible to mwananchi wa kawaida, na kama kuwa accessible itakuwa office gani, labda administration office, sindio labda mwananchi wa kawaida anaweza kufika office hiyo labda ya chief ama ya D. O., Na cost hiyo ambayo itatakikana ili mwananchi apate hiyo Katiba iwe inawezekana, iwe cost ni yake labda mia mbili ama mia na kitu, kitu kama hicho, ama fifty shillings kwa sababu mwananchi wa Kenya kupata pesa zaidi ya mia mbili si rahisi. Kwa hivyo hiyo ndiyo pendekezo yangu, Katiba tuitengeze na sote tuijue Katiba ni nini, kwa sababu ni sheria yetu wenyewe ambayo tunatengeza.

Ya pili ni unyanyasaji wa kina mama kwa sababu bado uko tena mkubwa mno. Na hivi leo nilikuwa nataka nione akina mama wengi lakini nikiona katika hall hii ama church hii, naona akina mama ni wachache sana, na sisi ndio wenye shida zaidi. Kuna a lot of discrimination bado, hiyo discrimination bado! Ile discrimination ndiyo tunasema affirmative act bado haija fanywa. Tena affirmative act ni ule usawa, hatusemi usawa ati nigeuzwe niwe mwanaume, ni ule usawa wa haki kwa haki.

Hivi sasa tuna hiyo tunasema Affiliation act irudishwe. Ile sheria ambayo ilikuwa hapo awali, msichana kweli akitungwa mimba ilikuwa inaenda kotini, ama sivyo kina mama? Na ikienda kotini kuna charges na mzee ama ni mtoto ata-pelekwa awe charged, ama kama ni Kuowa kitaita si tulikuwa nayo? Saa hii tunazungumza mambo ya imorals, imorals tunazungumza mambo ya indiscipline, lakini kwa sababu sheria zingine zimeondolewa, sasa hivi msichana wangu yuko, labda primary ama high school, na kijana wako, na kijana wako ametunga msichana wangu mimba. Si wangu ndiye anayeondolewa, kijana anaachwa anaendelea, kwa nini?

Hapo kuna discrimination. Tunataka kama ni penalty inafanywa kwa watoto wote. Huyu msichana ameacha shule na lazima atakaa miaka miwili nje kabla ya kurudi shuleni, alee

mimba miezi tisa, azae tena alee mtoto mwaka mzima ndio nimrudishe, na kijana anaendelea ama haendelei? Kwa hivyo mimi naomba Katiba tukitengeza, msichana akitolewa na kijana atolewe. Kama ni miaka miwili penalty, inafanywa miaka miwili ndio nao pia watakuwa na hii mambo tunayosema ya discipline ama morals, itaanza kuanzia hapo. Na ndio ninafikiri tuta reduce hata

hii rate ya ukimwi, kwa sababu mtoto hata kijana ataogopa, nikitunga mtoto wa watu mimba pale, nafikiri nitafukuzwa shule.

Kwa hivyo hayo ndio nilikuwa nataka niongezee, ingawa mengi yako katika written, kuna inheritance ambayo imezungumuzwa, kuna citizenship ambayo imezungumuzwa, haki gani mwananchi anatakikana akae, mengi yamezungumzwa na wenzangu ambayo singependa kurudia kwa sababu wengi wana maoni ya kuongezea. Kwa hayo machache, na shukuru sana kwa kunipatia nafasi hiyo.

**Com. Prof. Kabira:** Lakini kwa memorandum umeandika?

**Jemimah Mabruk:** Nimeandika.

**Com. Prof. Kabira:** Okay ni sawa.

**Jemimah Mabruk:** I am going to present.

**Com. Prof. Kabira:** Thank you very much Jemima. Mbede Ngeti. Yuko?

**Mr. Mbethi Ngeti:** Makamishina, na kamati, na waheshimiwa wote ambao mumekuja hapa, nawashukuru sana. Leo mimi kusimama hapa, kitu ambacho ningeshukuru zaidi ni kuwa leo ndio nimejua kama mwananchi au mzalendo wa kawaida anaweza kupata haki yake. Basi ni kama leo. Mimi, kwa maana mengi yamesemwa kuhusiana ni kama nilikuwa na wale ambao wameongea leo. Maana mimi kwa wakati huu…

**Interjection: Com. Prof. Kabira:**Umejitaja jina?

**Mr. Mbethi Ngeti:** Mbethi Ngeti. Mimi ni Mbethi Ngeti. Kwa hiyo nafikiri tumeelewana hapo. Mimi ninashukuru kwa wakati huu hapa tulipofika, na wakati tumefika hapa nashukuru kwa yale yote yaliyozungumzwa hapa, ni kama nilikuwa na wenzangu hapa. Mimi naunga mkono majimbo ambapo ijapo walio wengi hawapendi majimbo lakini mimi ndio nimeiunga mkono zaidi na mimi ndio nitakuwa najua niko katika nchi yangu. Kwa hiyo, sitakua na mengi maana mengi yamesemwa.Na

isipokua sasa nitasema kidogo juu ya wafanyi kazi. Wamesahauliwa sana. Vyama vya wafanyi kazi vya faa viheshimiwe sana. Viwe na haki kama vile ilikua 1963, viwe vyaogopewa na serikali, kama kwa heshima viheshimiwe. Kwa hayo nina mengi lakini ningezungumuza lakini kwa vile naona tuko na msafara mrefu, kwa hiyo naomba asante sana.

**Com. Prof. Kabira:** Okay asante sana bwana Ngeti. Duncan Mjomba?

**Mr. Duncan Mjomba**: Ma-commissioners, wenzangu wale wote ambao mumefika ni asante sana. Jina yangu ni Duncan Amon Mjomba. Nafikiri mimi yale yote nimeandika mengi ni yale yametajwa lakini nitasema machache ambayo mengine hayajatajwa. Nafikiri taabu yetu iliyoko Kenya, ni ile keki ya national cake, yaani utajiri hauja gawanywa sawa sawa. Nafikiri hiyo ndiyo kiini cha taabu yote iliyoko, unakuta watoto wanamaliza shule wamepita vizuri hawawezi kupata kazi maana cake haija-gawanywa sawa sawa. Kwa mfano unakuta wakati wanafikiria kama mikopo, hapa sisi wengine hatuna title deeds, hatuwezi kupata mkopo kwa sababu hatuna title deed, na hatuwezi create kazi sababu hatuna ile title deed ya kuenda kuchukua loan, labda nifungue kahoteli niandike yule mtoto ambaye analala nyumbani kama ni msichana. Kama ni mwanaume, wanakaa kwa sababu cake yenyewe haijagawanywa sawa sawa. Tunautajiri mwingi Kenya.

Tuseme hapa Taita kulingana na mimi nafikiri ndio moja wapo ya districts ambayo ina uchumi mkubwa zaidi kulingana na resources kama minerals, (wanyama wa pori, utalii uko hapa.) Lakini kwasababu hatujapewa uwezo wa kutumia deed ama maarifa, kwa hivyo nafikiri constituency yetu ituingilie na kutusaidia tupate kutumia hizo resources. Kama minerals, ziko mingi kama hapa Kazigau na Taita kwa ujumla kwa wingi. Nafikiri tungepewa hii constitution yetu ikiangalia maneno hayo, tunaweza kuenda mbele.

Sitasema yale mengine maana mengine kama hiyo ya KWS unakuta watu ni wageni wana andikwa. Watoto wetu wanakaa, wana elimu lakini hawawezi kuandikwa. Kwa hivyo nafikiri constitution yetu iangalie sisi urithi wetu badala ya ile miwa ama chai, ni hiyo, kama wanyama na hiyo minerals, tupatiwe nafasi tuitumie. Kama vile unakuta mtu wa Mombasa yeye kazi yake anaweza kuvua samaki. Sisi hatuwezi kuvua samaki kwa nchi kavu. Kwahivyo ile kilichoko hapa, sisi tupatiwe nafasi ama constitution hiyo, Katiba itupatie nafasi na sisi tutumie hiyo rasilimali. Kwa hayo mafupi, nafikiri nitawachia hapo. Asante sana.

**Com. Prof. Kabira:** Okay asanti sana bwana Duncan. Na tutamuuliza Harry Mwakazi, Harry Mwakazi ako? Harry Mwakazi ako? Hayuko? Doreen Kasim?

**Doreen Kassim:** Kwa ma-commissioner wetu, na wananchi, nimewasalimia sana. Mimi kwa majina naitwa Doreen Kasim. Nimesikia mambo mengi yameshatajwa, hata yale nilikuwa nimepanga yameshaa tajwa, kwa hivyo hatuwezi kurudia maana nikupoteza wakati. Niko na neno moja tu ambalo ninataka nisisitize, nipendekeze.

Equality, yaani usawa. Hilo sikusikia hapa wamelitaja na hapa akina mama ndio tumekaliwa kwa mambo hayo. Sisi tumekaliwa kweli kweli na wanaume, na nyinyi hamkutaja, lakini mimi nitataja leo. Mambo ya usawa ni ya lazima sana. Hata vile mumesema tuwe na government ya majimbo tumeunga mkono, lakini hapo katika majimbo hiyo government iwe na usawa. Ninapozungumza hivyo, nimeona hasa kwa wasichana wetu, watoto wetu wa kike wakipelekwa shule, hufanya vizuri sana, ni sawa sawa na vijana. Lakini ukifikia wakati wa kupata kazi, vijana wanachukuliwa kwanza. Hata nafasi za form 1, vijana wanachukuliwa kwanza.Na marks zile zile msichana amepata, na tena vile mnajua, sisi akina mama wa wasichana tuna watatiza sana, ndio wanatusaidia kwa kazi za nyumbani. Lakini hata hivyo, wakifanya kazi za nyumbani husoma, na huitimu vizuri sana kama vijana. Na katika kugawanya kazi au nafasi za form 1, mnaona wasichana wameachwa nje. Kwa hivyo nimeomba sana, Katiba hii yetu mpya ya majimbo tuweke wasichana wetu, katika nafasi kubwa kubwa za kazi. Kama tuna ma D.O. kumi katika hiyo majimbo, tuwe na wasichana watano ma D.O. na wavulana watano ma D.O. Kama ni ma D.C. kumi, tuwe vivo hivo. Kama ni madaktari, tugawanye vivo hivo. Kama ni ma lawyers, tugawanye vivo hivo. Leo munaona hapa hii kenya, iko na wasichana weerevu sana ambao wanaweza wakatuongoza vizuri sana.

Na ningeomba kama ni President mwanaume, Vice President awe msichana. Kama pale Uganda. Munaona Uganda inaendelea vizuri sana kwa sababu vice wao ni mwanamke. Wanawake sisi hatujui kupora, hatuwezi kuiba mali, kwa hivyo akiwa kingozi vice president ambaye ni mwizi, sisi kama yuko vice msichana, anaweza kumuambia hapa, tusichukue hivi na hivi. Kwa hivyo hilo jambo nilikuwa nataka nisisitize kwa sababu sisi wanawake tumeachwa nyuma, na sisi akina mama ndio

tunafanya kazi ya muhimu sana, hata mliona walikuja hapa asubuhi wengi sana lakini tena wamerudi kupikia watoto, wana kazi nyingi sana.Kwa hivyo hata tukiingia kwa upande wa elimu, wana fanya bidii sana. Kwa hivyo nataka Katiba hii msisahau akina mama. Asante sana.

**Com. Prof. Kabira:** Asante sana mama Kassim. Naona kama wamekubali. Khalif Muganga? Khalif ako? Hayuko? Mary Shugula? Mary ako? Ameenda? Ameenda okay. Maalim Kiteto? Hayuko? Ako, okay.

**Mr. Maalim Kiteto:** Asanteni sana ma-commissioner. Mimi kwa kweli sitakua na mengi, maanake mengi yamesemwa. Isipokua tu kusisitiza point labda moja, mbili.

Ni-seme tangu tupate uhuru, sisi watu wa pwani, kwa maswala ya mashamba, tumelaliwa sana. Hatuna title deed. La kusikitisha ni kwamba, mawaziri ambao walikuwa wameteuliwa, kusimamia hii wizara ya lands and settlement, ni watu wa hapa hapa pwani. Sasa ndio haijulikani, kulaliwa huku ni kisiasa au ni kivipi? Tunaiomba Katiba hii ifanye mtu kuwa na title deed iwe ni right rather than privilege.

Jambo la pili. Kwa upande wa walemavu. Walemavu ni wengi. Na wanashida hii na lile. Tungaliomba Katiba katika kuwasaidia haswa viombo, aids. Vile vyombo vinawasaidia kwa mfano, vya kusikiza, masikio, kwa mfano, hii magongo ya kutembea, yawe yanapatikana kikatiba, iwe inapatikana kikatiba.

Jambo la tatu. Hawa wanyama kama mwenzangu alivyo sema, wamekuwa ni wengi. Wapunguzwe kitaalamu, halafu na hii national park pia, ipunguzwe ili tupate mashamba ya kulima. Yangu ni hayo tu. Sina mengi. Asanteni.

**Com. Prof. Kabira:** Asante sana Kiteta. Geoffrey Mwanoi? Geoffrey Mwanoi ako? Okay.

**Mr. Geoffrey Mwanoi:** Asante sana ma-commissioner na wananchi. Mimi sina mengi ya kusema. Isipokua mengi yamesha-zungumzwa. Lakini sana, mimi nilikuwa nataka kuzungumzia juu ya utamaduni wetu, kwa sababu utamaduni wetu kwa kweli umepotea. Maanake hata zamani, wakati dada zetu wanaolewa, tulikuwa na pombe za kitamaduni lakini siku hizi hakuna. Ukitengeneza unafungwa. Kwa hivyo naomba utamaduni wetu urudishwe. Yangu ni hayo tu.

**Com. Keriako:** Okay, asante. Turudishe utamaduni?

**Mr.Geoffrey Mwanoi:** Ndio.

**Com. Prof. Kabira:** Okay asanti. Okay Jimmy Mwang'ombe? Jimmy Mwang'ombe ako? Hayuko? Okay. Angelina Kovo? Angelina Kovo? Ako? Ameenda? Okay. Benjamin Kwanya? Ameenda okay. Faustin Mwabuda. Mwabuda? Mwabuda? Okay hayuko. Okay Magaret Maidoki? Ako? Ameenda? Okay. Laban Ngoromo? Hayuko? Okay Benson Muingi? Benson Muingi hayuko? Na kuna Hilton Mwakio? Hilton Mwakio? Samson Mathenge? Henry Mwakazi? Juston Mwavoga? Hayuko? Arc Mwamburi? Arc Mwamburi hayuko? Livingstone Mbotela? Livingstone hayuko? Peter Mwatibo? Sorry, Philip Mwatibo? Philip? Geoffrey Mwacharo? Hayuko? Josiah Kigombe? Oh yuko, okay.

**Mr. Josiah Kigombe:** Na kwa ma-commissioner, na wananchi kwa ujumla nawasalimu, hamjambo? Kwa jina naitwa Josiah Mambo Kigombe. Kwa kushangia kuhusu habari ya Katiba, nafikiri yale nilikuwa nayo mengi yamezungumuziwa. Isipokuwa nitataja mengine kidogo.

Kwanza kabisa mimi ningesema ninaunga mkono habari ya majimbo. Halafu pili ni kuhusu muda wa utawala kama ma-councillor, wabunge vile huwa inanasemekana iwe miaka mitano ningaliomba kama ingewezekana hii Katiba ya muda huu au ya wakati huu tunairekebisha iwe ya kwamba tukachagua either councillor au mbunge, asipotimiza wajibu wake kulingana na matakwa ya wananchi, huo muda au wakati huu atupiliwe mbali na uchaguzi ufanywe bila kupoteza muda mrefu

La tatu ni nguvu za Raisi. Naona nguvu za Rais kweli zimekuwa nyingi na kwa kwa hakika zimetatiza sana utawala wa sasa.Kwa hivyo, ningependa zile nguvu zake zipunguzwe na sio isiwe kuwa atakuwa eti yeye yuko juu ya sheria ama above the law.

Halafu kwa upande mwingine especially hapa kwetu Taita wengine tumesoma lakini kulingana na kutokuwa na kazi, ningeomba Katiba wakati huu ituruhusu,especially watu wa kupima mashamba wapime mara moja ili wapewe title deed kusudi zituruhusu wengine twende kama ni kwa mabenki kuchukua mikopo kwa sababu hatuna kitu cha ku-insure halafu hatuna mimea tunategemea kama cash crops. Kwa hivyo tukiwa na title deeds, tungeweza kuenda kwa ma- benki na pia tuweze kupatiwa misaada ya kujiendeleza

Halafu lingine ni kuhusu ma-chief na ma-sub-chiefs. Mimi nilikuwa na two alternatives; Kama itawezekana ma-chief na ma assistants wawe wakichaguliwa na wananchi. Na kama haitawezekana basi pia ma-chief na assistants wao pia wawe wakipatia transfer.

Na lingine ningependa kuwatetea wenzangu au, wenzetu wafungwa. Kwa vile pia na wafungwa wako na haki zao, ingekuwa ni vyema pia wasifikishe wakati wa (?) wapewe nafasi ama kama wakati wa kupiga kura tuwe na vikundi fulani wapelekewe zile mabox pia nao waweze kupiga kura.

Halafu na lingine ni kuhusu huu ugonjwa wa janga la kitaifa. Ningelipenda kama Katiba ingetungwa kwa sababu tunaona kama kuna wengine wenye wanafanya makusudi especially wenye ambao wako na pesa. Wakishagundua ya kwamba wako na ukimwi,wanachukua nafasi hio na kutumia pesa zao kwenda mtaani kusambaza ugonjwa huo wakitumia pesa.Sasa kama kungekuwa na kipengele fulani mtu akifanya kusudi pia apelekwe kotini akistakiwa kwa visa kama hivi ama hicho kingine. Nafikiri hiyo ingekuwa kisawa.

Halafu na uridhi, mUnajua kuwa wengine tunatetea sana habari ya hii. Labda bwanangu amekufa alikuwa akipokea payslip sasa

mke anapokea baada ya miaka mitano inakatwa. Mimi nafikiri baada ya tumeoana huwanga tu watu wawili, bwana na bibi, sasa tunaweza kuwa wote tunafanya kazi na ya Mungu ni tofauti unaweza kupata mume atangulie. Sasa ule uridhi wako pia labda ni miaka mitano ungekuwa unapokelewa na mwanamume, unakuta mashemeji wako ndio wanaukimbilia wanasema kwani huyu alikuwa ni dada yetu mali yake yote tutaileta upande wetu. Kwa hivyo ingewekwa kipengele fulani cha kulinda ile ndoa ya watu wawili

Halafu na lingine nafikiri kungekuwa na Katiba ya kulinda mila na desturi za kila watu kwa sababu vile tunavyoona kulingana na zile desturi wengine wetu hapa tumesikia habari ya pombe. Nafikiri hofu kubwa imekuwa ni kwamba baada ya kutupa mila na desturi za watu fulani imekuwa ni kwamba hata pombe ya kienyeji imetupwa na tukiangalia, labda areas zingine huko kando kando tunapata pombe za kienyeji ndizo zinaletwa huku mkoa wa pwani. Tuseme kama kina muratina ni pombe za kienyeji zinaletwa upande wa Taita halafu tunashangaa ya kwamba kienyeji za kitaita muratina umekataliwa. Ukipatikana ukitengeneza unachukuliwa hatua, ningeomba kama ingewezekana instead ya kuibia serikali vile saa hii inafanyika kwa sababu tunaibia serikali tunatengeneza kichonjo chonjo tuuze. Ingekuwa ni vyema hata vilabu vingerudishwa kwa sababu hii ingekuwa inafunguliwa kwa wakati na pia serikali ingekuwa inapata kitu kidogo kuliko vile tunavyofanya saa hii.

Halafu la mwisho ningalipenda Katiba ambayo tunaitengeneza imtabue mwananchi awe ni mtu tajiri na maskini na imlinde kwa mali na rasilimali ya kikwao. Asanteni.

**Com. Prof. Kabira:** Asante sana bwana Kigombe.Damaris Hamisi? Hayuko. E. M.. Mkala? Ako? Okey. Karibu Mkala.

**Mr. Mkala:** Asante sana. Mimi kwa jina naitwa E. M. Mkala na nimetoka sehemu hii. Kwanza ningependa kushukuru ma-commissioner kwa kufika hapa kwetu siku ya leo ili nasi tutoe maoni.Lakini sikitiko langu ni kwamba tulipata habari ya kwamba tungefundishwa kwanza ndio mfike. Sasa mumefika kabla hatujafundishwa kwa hivyo si hoja. Mimi tunasikia tunachangia mambo ya serikali na nini na nini. Kama tungekuwa tumefundishwa tujue hii ina ubaya gani na uzuri gani tungekuwa

katika nafasi nzuri ya kutoa maoni, mimi sijui kosa limetokea wapi maanake tulisikia tufundishwe kwanza halafu ndio tutoe maoni. Lakini sasa kwa sababu tumekuja kila mtu na programme yake, itakaa wengine watachelewa

Kabla sijasema lolote ningependa tusome Isaiah hamsini na tisa msitari wa kumi na nne na kumi na tano

**Com. Prof. Kabira:** Ni sawa tu hebu tumpatie wakati.

**Mr. Mkala:** Nipatie wakati, ni wakati wangu nimefika hapa ndugu zanguni.Hii mambo tunazungumza hapa ni mazito, tukiteleza kesho hatutamlaumu mtu.Kwa hivyo msifikiri jambo hiuli halina maana, hata Mungu Mwenyezi anajua tuko hapa.

Isaiah 59:14-15 hii ni Kitaita, ni nzuri?

**Interjection:** Soma

**Mr. Mkala:** Inasema hivi, **(reading in Kitaita).** Inasema ya kwamba kweli, nilipo taka kuingia nikakosa nafasi. Na kweli nilipokosa nafasi, ndio sasa kule kutokua na haki kunatawala ndio maana leo tuko hapa. Mimi nasema mambo ya Katiba ilianza mbinguni. Na Katiba ilipokua mbinguni shetani akakataa ile Katiba ya binguni, ndio akapigana na Michael, ambaye Yesu akatumwa hapa duniani. Ndio unaona lile vile unataka kufanya halifanyiki maana yake shetani yuko pamoja nasi. Mimi nasema hivi, Katiba ile tutakayo tunga, kama haitakuwa mfano ya Katiba ya kimbingu, tutakuwa tunaelekea kwenye janga ambalo baadaye tutajuta. Ninaposema hivi, saa hii tunazungumza juu ya Katiba lakini kuna Katiba zile za kidini ndizo zina nguvu kuliko tunayo yazungumza leo. Mimi najua kwa nini.

Watu wanasema tunataka majimbo lakini ninajua jimbo la pwani kama litapitishwa, sisi tutakuwa na maajabu makubwa sana.

Jambo la kwanza mimi ningependekeza ni kwamba kuwe na uhuru wa kuabudu na ulindwe na kila mtu apate nafasi ya kuabudu Mungu bila shida. Ninapo sema hivi ni ya kwamba, kuna watu hawalindwi na hiyo Katiba. Munaposikia kuna uhuru wa kuabudu, mimi ni mtu naabudu kulingana na kitabu hiki cha Mungu. Siku ya Mungu kulingana na Bibilia takatifu ilivyoshikilia ni siku ya Juma-mosi. Na ndiyo mimi huenda kanisani. Lakini ni ajabu ya kwamba, hatulindwi kwa sababu tunapo kataa watoto wetu wasiende shule siku ya Juma-mosi watoto wanapigwa, unapo-ajiriwa kazi,na unapo kataa kwenda kazi siku ya Juma-mosi unafutwa. Kwa hivyo tunataka Katiba inasimamia Bibilia takatifu.

Jambo lingine. Uhuru ya kufanya mikutano ya kihadhara. Ndio nayo naona inaleta shida. Mimi ni wiki ilioyopita tu nilikuwa Voi kwa OCS. Nilikuwa nataka kufanya mkutano wangu Voi wa mhadhara. Na nikaambiwa kama wewe ni mtu wa SDA unataka kufanya mkutano wa hadhara hapa hiyo ilipitishwa na kamati ya usalama ya ulaya kwamba haitatolewa. Sasa mimi nikashangaa. Huu uhuru wa kuabudu uko vipi na mimi nimenyimwa kibali. Ni wiki iliopita tarehe ishirini na tano nilikuwa kwa OCS ndiyo nika ambiwa haiwezekani. Kwa hivyo naomba Katiba ambayo inafanywa, ilinde mwananchi na itambue vitabu takatifu vya Mwenyezi Mungu.

Viwanja vinavyo-peanwa, kusiwe na ubaguzi. Ninaposema hivi, Kanisa la wasabato nimekaa hapo miaka mingi, na kila wanapo wakilisha hili jambo kwa mkuu wa wilaya, wao wanazungushwa hivi na hivi na hivi. Na madhehebu yalikuja hivi baadaye, yaka-pata viwanja vikubwa kuliko sisi tunayotaka. Sasa kama kuna haki, na sisi tumeandikishwa katika kenya, vipi tunapo taka kiwanja inakuwa hatupati na madhehebu mengine wana pata. Kwa hivyo uhuru wa kuabudu umenyanyaswa. Tunataka Katiba inayo tengenezwa itambue uhuru wa kuabudu, na kila dhehebu litambuliwe. Jambo lingine. Kama kuna kiwanja cha public, kuwe na dhehebu lolote wanataka kulifanyia kitu fulani pale, isiwe ikawa ubaguzi wewe ni wa dini hii hauwezi kupewa hicho kiwanja. Ni naposema hivyo, mimi kuna shule hapa kwetu inaitwa Makonge ilifungwa. Na mimi dhehebu langu likataka kufungua hilo shule, nilipofika kwa chief na kwa D.O, nikaambiwa haiwezekani. Na nikamuambia jukumu la waalimu na yote ni letu sisi, tutaleta waalimu, na tutaleta hata kama ni kuwalipa hata na wanafunzi sisi ndio tutaleta, hatuna shida bora tukubali. Lakini sasa kwa sababu ya mambo ya kidini, tukanyimwa hii nafasi. Lakini nashukuru wenzetu ambao walikubali, na iko pale inaendelea. Lakini ingekuwa iko hapa.

Jambo lingine ni miradi wananchi wanayo-fanya. Ninasikitika wananchi wanaanzia mradi, na ule mradi sijui kama ile Katiba ilioko inalindi hiyo miradi. Ningependekeza ya kwamba, Katiba hii tunayo tunga ilinde miradi ya wananchi. Maanake unaona wananchi wanaanzia miradi ya maana, na ule mradi unapoanguka, hakuna jukumu linachukuliwa. Kama ni pesa zilichangwa, zilivutwa hakuna ukaguzi unafanywa, na hakuna maelezo kwa wananchi, kwa nini mradi ulianguka. Mifano kuna miradi miwili hapa kwetu ilianguka. Mulolo Water Project, ulikuwa ni mradi mkubwa, ukaanguka. Mpaka leo hakuna maelezo. Ndio unasikia wananchi wanapokuja hapa wanalia mambo ya maji maji. Hiyo shule ninayotaja Mwakongo ilianguka, mpaka sasa hatujui rasilimali inalindwa na nani. Na iko na viti, iko na majengo, na ilikuwa na staff imewachwa hivi hivi tu, mali ya wananchi inapotea. Kwa hivyo tunaomba Katiba inayo tengenezwa sasa, ihakikishe ya kwamba, imelinda wananchi, na haki zao.

Jambo lingine ni kuhusu mtu kuitwa raia. Maanaake mpaka sasa tangu hiyo miaka 39 ya uhuru, tangu tupate uhuru mpaka sasa, hatujapata kinachoitwa title deed. Sasa, je hii Katiba iliyoko imetulinda? Na kama sisi ni wananchi, mbona title deed zina shida kutoka? Miaka 39, watu wa sehemu hii wanalia title deed hawajui itatoka mwaka gani. Kwa hivyo tunaomba hii katiba ambayo inatengenezwa ihakikishe kwamba mwananchi kama ana ardhi yake, title deed itolewe mara moja. Maanake ndio unaona tunazungumza hapa hata tunashindwa kama wananchi wa Kenya na hatuna ardhi, maanake hatuna vitambulisho. Kwa hivyo sijui tunaitwa masquatter ama tutaitwa jina gani. Na hiyo tumelia, tumelia, tumelia. Kwa hivyo tunaomba Katiba inayo tengenezwa, ihakikishe ya kwamba, mwananchi ye yote, ajiandikishe, kama mwananchi na ardhi yake apatiwe kibali, ili ajue kwamba mimi ni mwananchi, na nina miliki ardhi yangu kihaki.

Jambo lingine, ni kuhusu assistant chief na ma-chief. Mapendekezo yangu ni wawe wakichaguliwa na wananchi.

Jambo lingine, ni kuhusu mambo ya kuteua hawa wagombea uchaguzi wa ubunge. Ninge pendekeza ya kwamba baada ya watu kutoka wengi kusumbua wananchi, wananchi wenyewe wapendekeze ni nani watasimama,katika Katiba hii inayokuja. Maanake imekuwa ni fujo, unakuta hata kwa kijiji wanatoka wawili watatu, hata mwingine hatapata, anataka kusumbua mtu. Kwa hivyo wananchi, Katiba inayo-tengenezwa, wawe na haki, ya kuteua wagombea uchaguzi, kama ni councillor, kama ni

mbunge, sisi tusema wewe utasimama. Si kutoka wewe na bibi yako nyumbani mnaamua mnasimama, mnatusumbua. Kwa hivyo wananchi wapatiwe haki ya kuteua hawa watu. Kama sisi wazee tutakaa, wazee waseme sisi tunataka fulani asimame.

**Com. Prof. Kabira:** Bwana Mkala tafadhali, jaribu ku-summarize.

**Mr. Mkala:** Na-summarize. Jambo lingine ni kuhusu pensioners. Tunashangaa maisha yana panda, na kama wewe siku uliostaafu, pension yako inasimama pale pale. Kwa hivyo inaonekana mtu ambaye ni pensioneer halipwi, maanake maisha inapopanda, wewe unawachwa pale pale, kale kale uliandikiwa utakuwa ukipokea ni kale kale. Kwa hivyo wakati maisha inapanda, na mshahara unaongezwa, na pensioneer naye aongezwe. Na mambo ya kuchelewesha hizi pension iangaliwe.

Halafu, jambo lingine linasikitisha ni wale ambao wanastaafu ama wale ambao wamefiwa. Hii ni pesa ya mtu ambaye amekufa au mtu ambaye ame staafu, matayarisho iwe ikifanywa kwa mkuu wa wilaya. Maanake watu wengi wameenda Nairobi wamesumbuka na wengi hata akina mama wamekata tamaa, wamesema pesa hizo sipati tena. Maanake ukienda pale 'ingia ofisi hii, ingia hii,' hata wengine karatasi hizo wamezitupa. Kwa hivyo, hakuna haki kwa mtu anapostaafu anapotafuta haki yake. Iwe ni mama amefiwa, iwe ni mzee anatafuta haki yake. Wengi hapa walikuwa na wazee wameacha hayo mambo, kwa sababu ya kusumbuliwa. Kwa hayo machache au mengi, Mungu awabariki, lakini tutunge Katiba ya mfano wa mbingu. Asanteni.

**Com. Prof. Kabira:** Asante sana bwana Mkala. Florence Mbeiyu.

**Florence Mbeiyu:** Maofisa wetu, na baba na mama hamjambo?.Mengi yamesemwa ambayo nilikuwa nimejitayarisha kusema, lakini yameshasemwa. Lakini nitajaribu tu kuguzia kidogo. Hata tukirudia, officer msione vibaya kwa sababu tunaumwa. Mimi nitagusia kidogo hii mbuga yetu, wengine wamesema mtu akiuliwa, sijui alipwe shilingi ngapi.

**<u>Mali zetu tunataka zibakie katika mikono yetu. Mfano, uchimbaji wa madini uwe mikononi mwetu, bandari yetu iwe mikononi mwetu, na wanyama pia wawe mikononi mwetu, zote ni rasilmali yetu.</u>**

Kitu kikingine nataka kusema, naomba Katiba mpya iondoe mambo mengine ya zamani na mengine yakaribishwe. Kwa mfano, hii c

hii dini yetu nimeona kwamba hii ufungaji wa ndoa katika kwa DC uondolewe. Nitaongea tu. Ufungaji wa ndoa kwa DC uondole kwa nini unaenda kufunga ndoa kwa DC na hali ma-kanisa yako? Kwa sababu ya kusema hivyo, msichana, labda mimi nimekataa na yule kijana, na kumbe mumepedana na munaenda kisiri siri mnafunga ndoa yenu huko. Lakini mimi, sita-kuwa nina upendo. Mi mzazi, lazima nitakuwa na chuki na yule mama.

Pili, tena nitaingilia Katiba itusaidie kwa hao ndugu zetu pia waislamu. Kuna kitu kingine ambacho kina- tuudhi, ni kama hic nilichosema, sisi wazazi. Utaona msichana wa ki islamu anapatana na mvulana wa ki kristu, tayari amesha msilimisha. Mzazi wake tayari wamesha fungishwa mikaa, wazazi hawako, hiyo kweli hatutapendezewa. Ndiposa ni kasema tunaomba Katiba mambo waondoe na mengine ya-wachwe. Utafungisha mtoto wa mtu mikaa, wazazi wake hawako, umemsilimisha, umemfungia mikaa, Sitakuwa na raha naye hata kidogo. Na wale watoto mnao-zaa, hawatakuwa na imani yoyote. Mambo kama hayo naomba Katiba Ni lazima kama ni ndoa, kama ni mikaa, wazazi wote wawe wako.

Na hii nchi yetu, kutoka hapa Mbololo mpaka Voi, ni nchi nzuri sana ya mazao, lakini kitu kimoja tu tumekosa. Katiba mpya, muomba ni maji. Ambapo maji hayako bali. Tuna maji hapa Mzima Springs. Tuna maji hapa mto wa Tsavo, mimi mwenyewe nisha ni-kayashika na mkono wangu maji ya Tsavo na yako tu karibu. Kwa nini tusiletewe hapa? Katiba mpya bebeni huo uzito mtule maji hapa, na sisi tutakuwa kama watu wa Taveta. Mchanga wetu sisi ni mzuri sana, lakini tumekosa maji. Tunamuomba, tunaomb mpya.

Zaidi, mimi naunga mkono majimbo. Kwa sababu, majimbo ya-kiingia watu wengine sisi tulio nyanyaswa mpka tukawa wemba tutaremsha vitambi.

**Interjection:** Laughter

Tutateremsha vitambi. Maanake tukisema kule kunyanyaswa mpaka wengine tumekonda, mimi binafsi nilipewa kiwanja changu nyang'ang'anywa. Na niliponyang'anywa na huyo mtu, mimi nika-muuliza, mimi ma-karatasi yangu haya, tumepata na wenzangu na ndio tumekata miba ilipokuwako. Hii yako ulipata wapi? Ananiambia mimi nilipata juu mbinguni

**Interjection**: Laughter

Pili, mambo haya ya pombe hata mwenzangu amesema, na hata mimi nasisitiza. Kweli tulipiga makofi kwamba pombe iondole tuliopopiga makofi pombe imeondolewa, kidogo tumekaa tumeona pombe nyingine imekuja yaitwa miti ni dawa. Nimeuliza wa jamani, hii yaitwa miti ni dawa yatibu ugonjwa gani? Sijaambiwa na yeyote, ikiwa ni pombe ifunguliwe pombe. Hata sisi pia t Tuna watoto ambao wamezalia nje wanataka kufanya vipombe vyao pia wajipatie riziki sio ati wengine wanakwenda kutubebea po hapa wanakuja kuuzia hapa kwetu, wanakuja kuuza hapa kwetu wajipatie riziki halafu wanaigeuza ni dawa, inatibu ugonjwa gani?

**Interjection:** People clapping

Mimi ni mtu ambaye naishi Voi lakini hapa ni kwetu nimezaliwa hapa. Na lakini jana nilikuja kule , nikakuta watu wamejaa nikasema watanikuta huku. Na hivi nilikuwa nataka niteremke. Mimi naishi Voi. Nikasema siteremki maanake hapa ni kwetu, nitalala lakini nitoe yale ambayo yananikera. Ahsanteni

**Interjection:** Clapping

**Com Zein:** Ahsante sana. Jiandikishe pale. Naftali Kiteto.

**Naftali Kiteto:** Hamjambo nyote? Jina langu ni Naftali Kiteto. Nimeshukuru kwa yote tumesikia ya Katiba. Nimeyapata vizuri lakini nina langu moja nataka kusema. Wake ambao wameachana na bwana, kufuatana na sheria za kimila, hasa wataita, huyu mama na bwana yake, pengine watoto wako. Na sisi kama mimi tumefikia miaka sabini. Sasa kama hao wanawachana na yule mwanamke, hukuenda kumwokota. Mlikutana, mkaoana wao kwa wao wawili halafu tena wakatuunganisha wazazi kwa wazazi, tukapatana, tukamaliza mali kabisa. Sasa neno la kushangaza ni hili, neno la kushangaa, tunataka Katiba yetu ifuatilie kile kimila chetu kama ikiwezekana. Yaani ,kama uliolewa na ukatolewa mali na pengine umekosoana na bwanako, lazima urudi kwa wazazi, wazazi kwa wazazi watafute nani mwenye makosa. Sasa, wewe na bwanako mnawachna na pengine Mungu amemjalia mmefika watu wa miaka arobaine na tano, mmepata watoto. Sasa wewe hutaki kwenda kwa wazazi hutaki mapenzi halafu sasa Mungu amempa riziki, inataka mme na mke washirikiane ndio watoto wawe watu wazuri. Lakini wewe huendi kwenu. Una-tangatanga, wale vijana wanaharibika. Sasa tunataka, kama ikiwezekana, Katiba ifuate haya mambo. Kama huyo ni mmeo, mkafanya harusi, ukatolewa mahari halafu mmekosana na yule bwana, rudi kwenu. Pale, wazazi kwa wazazi wakutane wamalize mambo yote. Sio kutangatanga. Kwenu huendi, unakaa hapo hapo, unaharibu majina ya upande wa mumeo. Na saa zingine tunaona katika ile kijiji kunaweza kuwa vita. Wewe unaharibu majina. Pale umeolewa na yale majina yako hayakusemwa unasema hivi, na ile na hili. Kwa hivyo, kwa yangu mafupi, naomba hii Katiba, ikiwa mtoto ameolewa na wamekosana arudi kwa wazazi.

**Com. Zein:** Tumeshakuelewa. Tumeandikisha hiyo

**Naftali Kiteto**: Mshaandikisha? Sasa yangu ni hivyo

**Com. Zein:** Tumeshaandikisha. Ahsante sana mzee. Jones Kiriga?

**Jones Kiriga:** Commissioners ambao mko hapa, ningelipenda kuchukua fursa hii ili nami pia nitoe mapendekezo yangu hasa kuhusu mambo ya Katiba. Kuna jambo hapa mimi nafikiria tumeacha kulizungumzia. Kuna hizi natural resources. Nafikiri tumeliongea kidogo lakini bado hatujalifafanua ni vipi tunaweza kufaidi natural resources. Mimi nafikiri, jambo ambalo

ningelisema ni kwamba kwa saa hizi, twa-fahamu kwamba vijana, ndio utu wa jamii. Na ili kukuza hawa vijana, lazima tuwatafutie njia ya kuwa-patia motisha. Hapa tunajua kwamba serikali yetu tukufu hupata misaada kutoka nje mara kwa mara. Ningelipendekeza Katiba iwe ambaye inaweza kulinda hasa vijana endapo pesa zitakuja za msaada wa aina fulani. Kama vile tunapata aid kutoka hizi non-governmental organisations ziletwe katika kila jimbo ama katika kila mkoa ambao watu watagawiwa kiasi fulani ama kiwango fulani na hawa vijana tuweze kuwatumia waende mahali kama porini waende wakajitafutie namna yao ya kuishi. Nafikiri hiyo ndio njia tunaweza kusaidia hawa vijana wetu.

Jambo lingine, tuseme tuna hii mambo tunayoita lease. Hii lease naona kwamba imetatiza sana kwa sababu hii lease utakuta lease iko ya miaka tisaini na tisa kuchukua land. Hii kutu imetatiza watu wengi kwa sababu miaka tisaini na tisa katika hawa wazee wote tuko hapa, sidhani kuna mtu amefikisha miaka tisaini na tisa. Kwa hivyo, hiyo miaka ni mingi sana. Kwa hivyo, ningelipendekeza Katiba yetu irudishe miaka kuanzia miaka ya arubaine na tano mpaka hamsini ili wakati hawa vijana wanapokuwa wataweza at least kula yale matunda ya ile ardhi ama lile shamba lao badala ya ile miaka tisaini na tisa.

Jambo lingine, kuna mambo ya maji. Hapa Kenya kusema kweli, hapa sehemu za Taita, ukisikia watu wanasema maji, hapa sisi ndio tunapatia watu wa Mombasa maji. Maji yote yanayotumiwa Mombasa hutoka sehemu za Taita. Tuko na ile mzima, tuko na hii sehemu nyingine nyingi. Maji yote hayo ni mazuri sana. Na maji hayo yanaweza kuhifadhiwa kwa njia nyingine. Lakini, jambo linalo shangaza ni kwamba, maji haya yanatoka yanaenda Mombasa. Watu wanayatumia Mombasa sana. Sisi wenye kifaa ama wenye maji hayo ambayo ni rasilmali zetu hapa Taita, hakuna kitu tunapata. Tungeliomba, wale watu wanatumia maji huko, kwa sababu nao pia wanalipa yale maji, wakiyatumia, huwa kuna kitu wanalipa. Na sisi maji hii Mombasa Municipality iwe inalipa Taita Taveta kiwango fulani kulingana na rasilmali zetu hapa. Wawe kuna ushuru wanatupatia. Kwa hivyo, hiyo ingelikuwa kwa Katiba yetu, ingelikuwa inaweza kusaidia sana.

Jambo lingine ni hizi vitu vinaitwa Title Deed. Hiyo nafikiri ndio kidogo, imetatiza. Maana mimi jambo la kushangaza ni kwamba, mimi kidogo niko na shamba pale Voi, niko na ka-plot. Nilikuwa nime jaribu kujenga jenga, ni-kaja nika-nyang' anywa. Lakini ndugu yangu Mkikuyu alikuwa kando na mimi. Yeye alikuja na title deed, yake na akajenga. Na mimi miaka yote hiyo nimeishi hapo nimejaribu kutafuta title deed sijapata. Yeye hutumia Katiba gani kupata hiyo title deed? Kwa sababu yeye tayari ako na title deed, na yeye anajenga mimi sina title deed. Yeye alipata namna gani ile title deed? Na sote tuko katika area moja. Kwani hii Katiba iko na watu fulani wawa-favour, na watu wengine haiwa-saidii? Kwa hivyo katika ile Katiba, ningeliomba mjaribu kuangalia hicho kitu.

Jambo lingine kama hapa saa hizi tuna hii tunaita KWS na hiyo college yake Manyani. Nafikiri sehemu hii iko sehemu ya Mbololo na ni wazi kwamba, hii ingelikuwa watu wa kufaidi zaidi ni watu wa kutoka Mbololo. Tungeliomba Katiba ambayo ina ajiri watu kuenda huko, iwe ina- favour kwa mfano watu kutoka Mbololo, wapewe a third. Theluthi moja katika wale watu wanao ajiriwa katika hii KWS especially hii ya hapa Manyani. Na theluthi mbili iwe ni ya wale watu kutoka sehemu zingine. At least hapo inaweza kuondoa umaskini kwa eneo fulani kwa sababu vijana wengi saa hii ndio wanatatizika. Otherwise

na-shukuru sana . Na kwa jumla, naunga mkono wa majimbo.

**Com. Zein:** Ahsante sana. Tuko na wazee hapa nasikia wanataka kwenda, wanaenda mbali. Robert Majala? Ahsante

**Robert Majala:** Ahsante. Ninachoamini, ni wazi wenzetu wote mlio hapa, fimbo ya mnyonge hulipwa na Mungu. Na tumepata nafasi ya kuzungumza mambo kama haya, Mungu ayabariki.

Langu ni KWS, huwa inasitikisha mpaka sasa. Maoni yangu, naweza kudhibitisha yamesemwa sana, na nitasema hayo hayo kuhusu KWS na Voi township. Kwanza, hiyo Katiba, haya yalizungumzwa parliament na mtu aitwae Masheghu wa Mwachofi kuhusu KWS. Pesa zinapopatikana hapa, zilipwe County Council yetu ya Taita ama hata Municipality yetu ya Mombasa. Mpaka wa leo kitu kama hicho hakijafanyika.

Voi township, Katiba ya KANU inasema mwananchi wa Kenya anaweza kuishi mahali popote. Mimi kama mmbololo naweza kuishi Kiambu? Voi yetu imechukuliwa mpaka sasa na kwa vile ilivyochukuliwa, hali yetu tulivyo hatuna shilingi za kuweza kupigania. Tunaomba kama ni haki kamili na Katiba ya Kanu kama inavyosema, mwananchi ana uwezo wa kuishi mahali popote na sisi tupewe nafasi kama yawezekana kisheria, Kiambu tunaweza kuishi akina Mwamburi? Thank you.

**Com. Zein:** Thank you.

**Robert:** Mimi ninalosema ni wazi kwamba na ninaamini kifungo cha Mungu ni kwamba, fimbo ya mnyonge hulipwa na Mungu. Haya yalizungumzwa parliament mpaka ikasababisha mtu aliitwa Argwino Kodhek amweka Joma Kenyatta above the law. Kumpa mwanadamu madaraka ya kimungu. Mimi ni mmoja umri wangu ni seventy five years of age na nimeishi nje kwa muda mrefu. Lakini mtu kupewa jina kama mungu apigiwe magoti yanaonekana sasa. Kama ufisandi wakati wa Colonial Government, DC akiwa mahali anazungumza, anazungumza na action inafanyika. Leo tunasikitika tuna viwaja vyetu hapa kama ranches na DC alitufanyia mkutano mdogo akituelemisha tutafanyiwa na tutaitwa mkutano kabla ya January thelathini na moja. Leo tunakwenda, April inakwisha mpaka sasa hakuna kitu kilichofanyika. Wananchi, sasa kama Kanu Government ni hii ya kila mtu ana uhuru wa kusema, ni nini ufisadi usitumike katika nchi yetu kama hii? Walio na haki ni wale walio na shilingi. Sisi ambao hatuna pesa, hatuna haki ya kuishi na mali zetu. Tumelipa mali zetu group ranching. Hii ni kama company yetu. Tumelipa ng'ombe zetu hapa, we are group ranching mpaka leo tulivyohaidiwa na DC halija-fanyika. Hivi kweli tuta amini kwamba tutapata haki zetu? Bara bara Kanu Government manifesto, sisi ndome yetu inatengenizwa mpaka hapa, na barabra yetu inaharibika ni mabonde mpaka kesho kutwa! Watu wengine, kama mmoja ni mimi nimefikia kwenda kufa, nitakufa bila kupata haki yangu. Sijui kama ninayo-yasema yalisemwa, na naamini kwamba yote yalizungumzwa lakini ninawakumbusha kwamba Mwaghaza Mwachofi alizungumza parliament na akaitwa na Njonjo maana ni facts alisema ya KWS hii iko Taita hii. Kwa nini County Council ya Taita haipati chochote kuhusiana na KWS au Voi municipality? Ni moja nakumbusha, ikiwa Katiba ni ya wote waliopo Kenya, wapewe haki zao. Mimi namaliza kwa kusema, fimbo ya mnyonge, hulipwa na Mungu.

**Com. Zein:** Ahsante sana mzee wetu. Tuko na Christopher Kayana

**Christopher Kayana:** Wanatume na wa-mbololo, kabla sija-anza kuzungumza yale niliyonayo ni kwamba ningewa fahamisha kwamba leo hatukuja kugeuza Katiba au kurekebisha Katiba kwa sababu hatujui. Tumekuja kutunga Katiba. Kwa sababu utakigeuza vipi kitu hukijui, hujakiona na wa-kigeuza vipi? Kwa hivyo, tumekuja kutunga Katiba ya kutufaa sisi. Katiba iliyokuwa imetungwa mwaka wa tisa mia sitini na tatu iligeuzwa kwa manufaa ya waliokuwa na mamlaka na iliwa-faidi kwa sababu tukiangalia wakati tunateremka chini Katiba ilikuwa inasema Kenya au maongozi ya kiserikali yakitungwa na wananchi kwa faida ya wananchi wenyewe. Kwa kimombo wanasema "Government of the people, by the people, for the people". It never happened. Haikufanyika hivyo. Ilikuwa ni mimi nikiwa mkubwa, serikali ni yangu. Nyinyi mwala majuto.

Juu ya mali ya asili. Kwa nini tupembelezane bwana? Kwa nini? Mali ya asili nilipewa na mwenyezi Mungu. Wewe kama haukupata, kaa huko huko maana alichokufanya mwenyezi Mungu akakupa huko, anakijua. Kwa hivyo, mali ya asili, walio katika mali hizo, waondoke. Katiba iwe mali ya asili itavunwa na mwenyeji wa sehemu ile.

Juu ya mambo ya biashara ndogo, ndogo mwenzangu mmoja alizungumza. Lakini vyaudhi kwa sababu hapa tunajidai tumesoma dini. Lakini hatuja-soma dini tumejipaka mafuta kama wale walaghai wafarisayo. Kitabu cha Mungu hiki alichosoma mwenzangu hapa, kumbukumbu la torati aya ya thelathini na mbili, mstari wa kwanza mpaka wa tisa wasema, Mwenyezi Mungu akaona vyema kumugawia kila mtu na kwake. Leo Taita ni yetu. Nasitikika nikidhania Taita, maana ya enda nikiona. Vipi kioski cha kuuza tomato ama kiosk cha kuuza peremende mtaita hawezi kupata Voi. Mimi nikisema, nimeishi Nyeri miaka mingi. Sijaona mtaita, mjaluo, mkamba na kioski wala meza kama hii. Leo Voi ni kwa kila mtu. Kwa hivyo huko ni kila mtu na kwao kufuatana na kitabu, huku ni Kenya ya kila mtu. Jambo hili lasikitisha. Kwa hivyo tunasema, Katiba iheshimu kumbukumbu la torati na yule aliye huko aheshimu. Wewe utakwenda soma bwana. Hata katika wa-Islamu, hiyo kumbukumbu ipo. Kitu kilichoko, haya yote tuta yamaliza tukiwa na serikali ya majimbo. Hiyo ndiyo serikali itaweza kumaliza ufisadi, itaweza kumaliza uhalifu, uporaji na wakati tunasema hivyo, hivi sasa mtakuwa na kazi na mtachukua jukumu kwamba viwanja vyote vilivyo-peanwa kutoka themanini na tatu kufikia jana. Muende mseme vya Voi vyote vifutwe tupeane upya. Kwa sababu wafanya-kazi wa wizara ya ardhi wanajipa viwaja ishirini na tano, thelathini na wewe kwenu bwana, Kisumu nikija kweli nitapata kiwanja? Kunao unaweza kuwataja, lakini sitaki kuwataja maana itakuwa ni dhuru.

Na jambo la muhimu ni kwamba, Katiba ya kwanza ilikuwa inapeana elimu ya bure, madawa ya bure. Leo hivyo vitu vinapeanwa bure? Ni kitu gani kimetokea hapa katikati? Ni kwa sababu dawa ikipeanwa bure, yule aliyekuwa na tamaa ya kupora hata pora.

**Com. Zein:** Kwa hivyo pendekezo lako ni gani?

**Christopher Kayana:** Mimi napendekeza elimu ya bure irudishwe, na madawa ya bure yarudishwe. Kama ni kodi tulipe maana huyo aliyekuja alipopewa Vice President, akageuza mambo yote hayo ikawa at ni cost sharing. I am cost sharing with who? Mimi ni mwenyeji. Hospitali ni yangu. Mimi ni mgonjwa, whom I am cost sharing with?

**Com. Zein:** Tumekuwelewa na tumeandika chini.

**Christopher Kayana:** Jambo lililo la mwisho ni kwamba mashamba ya Taveta, Jipe, Ziwani, Mwatate must be given back to Wataita and Wataveta, kwa sababu marehemu mheshimiwa Mwanyumba, alikuwa amechukuwa mkopo kutoka ulaya. Na akalipia mashamba hayo ili serikali ikilipa mkopo ule, wataita na wataveta wagawiwe mashamba hayo. Yamechukuliwa kwa sababu Katiba ikageuzwa ili ifae mtu fulani, watoto wake waridhike.

**Com. Zein:** Sema, Jipe, Ziwani na gani?

**Christopher Kayana:** Jipe, Ziwani, Taveta, na Mwatate. Angalia gazeti la tarehe nne December sitini na nne, linakwambia hiyo ndio ilinunua hili shamba

I**nterjection**: Laughter.

**Christopher Kayana:** Kitu kilichoko ni kwamba mambo ya ardhi, mambo ya ardhi katika Katiba yetu tunayoitaka ni kwamba mambo ya ardhi ya kila Mkenya iangaliwe ni wazee waliochaguliwa na watu wa sehemu ile wala isiwe ni mambo ya land.

Juu ya Nationa Park. Mimi na shangaa kweli mwenzangu amesema ukweli, title deed ya National Park iko ulaya kwa Queen. Lakini, kutoka hapa Relini mpaka Mdanda rock, kulikuwa ni Game Reserve ya wataita na aliekuwa akiichunga alikuwa anaitwa Mohamed Gem, alikuwa ushelisheli sijui nini. Lakini Queen babake alipokufa mwaka wa hamsini na mbili, akapewa ati ni kupanguza machozi. Sasa, mpka leo yualia? Yualia babake mpaka leo?

**Interjection:** People clapping and laughing.

**Christopher Kayana:** Twataka hiyi Game Reserve irudishiwe Wambololo. Toka hapa mpaka Dololo. Dololo kulikuwa na watu. Jambo ambalo linafuata ni kwamba mambo ya pension yamezungumzwa, na siwezi kurudia. Ni kwamba tunataka bibi, bwana akifa, akila pension pengine wameshikwa na yule mwalimu mkakamavu, baada ya miaka miwili mama kama atakufa mtoto wa kwanza aendelee kupata pension ili wajimudu. Kwa sababu hatujui siku za mtu ni ngapi.

Halafu nikimalizia ni kwamba tunajigaramisha wanyewe kwa sababu ya wivu na utovu wa nidhamu. Ikiwa mtu amehukumiwa

hakuua. Amefanya kosa fulani, pengine kuua na kuiba ndio makosa yanayo chukiza sana lakini makosa mengine yako mtu hufungwa. Mtu huyu ikiwa ni fundi wa kujenga, kwa nini asiuzwe serikali ikatafuta contract, ikatumia wale maabusu wakaenda wakanjenga. Bara bara hiyo imejengwa ya wachina hii kutoka Mtito Andei mpaka Miazeni imejengwa na wafungwa kutoka China. Si serikali ya China imepata pesa? Imekuja kuzichukua hapa. Kwa hivyo tunasema, wafungwa wetu wale wenye ujuzi, watumiwe ili kuvuna pesa. Kwa hayo machache, ahsanteni.

**Com. Zein:** Ahsante sana mzee wangu. Jiandikishe.

**Joseph Mwawasi:** Wananchi watukufu, nilisema asubuhi kwamba, kama tukisikilizana nita washukuru sana. Nilisema asubuhi kwamba, itakapokuwa inakaribia jioni, tutashauriana ambapo mambo haya ya Katiba ni mashauriano. Bado tunaona orodha ya watu ambao wamejitayarisha kutoa maoni ni kubwa. Na sasa ni saa kumi inakaribia na nusu na tunapata maombi kutoka kwenu, kwamba kuna watu ambao tunatakiwa tuwaombe radhi wengi wetu tuwape kipao mbele wazungumze kutokana na hali walizonazo. Wazee wawili wamepewa ruhusa wakazungumza kwa sababu mmeona hali zao. Lakini tumepata ombi pia kutoka watu wanaotoka Ngolia location. Haya tunayoyazungumza haya ya mbuga za wanyama na wanyama kuwafanyia wenzetu unyama wanasema wanahofia wao wakiondoka hapa wamechelewa, mnajua habari za ndovu si mimi kuwaelezea nyinyi. Sasa sijui mta-tushauri tufanye vipi? Maanake mimi ningetoa wazo hili kwamba kuna mtu ana mswada wake anataka kutoa bila kuzungumza aruhusiwe kufanya hivyo. Na tulisema hivyo asubuhi. Wale wenye mswada ambao wanataka kutoa bila kuzungumza watoe. Na kama mtaniruhusu, nitwapa fursa hawa co-ordinator wetu mshirikishi amehakikisha kwamba wametoka Ngolia location. Mheshimiwa, commissioner aendelee na wao, na mtu akiwa na haja za aina hiyo pia azungumze na mshirikishi atuweleze, sijui kama mna-kubali hayo?

**Response:** Tumekubali

**Com. Zein:** Ahsateni. Oliver Mwatee

**Oliver mwatee:** Honourable Commissioners, mimi naitwa Oliver Mwatee, mimi pia ni Member wa kamati katika eneo la bunge la Voi. Mimi sitakuwa na mengi ya kusema kwa sababu jana Voi, nilikuwa tayari nishatoa maoni mengine pale. Lakini kuna mengine machache ambayo yalikuwa yamebaki ambayo niliyotaka niyamalizie sasa. Mimi nilitaka ni zungumzie juu ya professionalism. Ujuzi wa kazi. Honourable Commissioners, utakuta kwamba kuna watu ambao wamesomea kazi kadha wa kadha. Kama kwa mfano tukizungumzia juu ya upande wa madawa na upande wa Agriculture. Utakuta kwamba kuna hizi maduka ambazo zina-uza madawa ya wanyama na mimea ya kupanda. Wale watu ambao wanafungua hizi Agrovets wengine wao hawana ujuzi wa Agriculture ama wa livestock. Lakini kwa sababu ambazo wale ambao wanatoa hizo license wanajua, unakuta kwamba mtu ambaye hana ujuzi wa Agriculture ama livestock amefungua Agrovet.

**Com. Zein:** Unapendekeza nini pale?

**Oliver Mwatee:** Kwa hivyo mimi napendekeza kwamba wale ambao wataruhusiwa kufungua haya maduka ambayo yana-tuuzia madawa ya mimea na begu za kupanda, wawe ni watu ambao wamesomea Agriculture na pia ambao wana ujuzi wa livestock.

**Com. Zein:** Next point.

**Oliver Mwatee:** My second point, tukiingia upande wa hospitali, matibabu. Unakuta kwamba katika health centre nyingi, unakuta kwamba zinakuwa run ama incharge wa hiyo health centre ni nurse. Anaweza ku-diagonise dawa namna gani? Yeye si Clinical Officer. Kwa hivyo tunaomba kwamba, yule ambaye atakuwa incharge wa health centre ama dispensary awe ni kutoka Clinical Officer na kwenda juu. Nurses hawaja-fundishwa ku-diagonise. Kwa hivyo utakuta kwamba anaweza kupatia mgonjwa the wrong medicine.

**Com. Zein:** Tumeelewa hiyo. Next?

**Oliver Mwatee:** Next, hizi pesa ambazo watu wanakatwa za National Insurance Fund. Unakuta kwamba kwa mwaka mtu anakatwa pesa nyingi sana. Lakini hajakuwa mgonjwa, ama family hawajakuwa wagonjwa. Na hizo pesa huwa hazirudishiwi watu. Tunaomba katika Katiba hii kwamba, kama mtu anakatwa pesa ya National Insurance Hospital Fund na hajakuwa mgonjwa na hajazitumia, arudishiwe pesa zake.

Haya, kufutwa kazi kutoka katika ofisi za umma. Mimi napendekeza hivi, mtu yeyote ambaye amefanya kazi zaidi ya maika kumi, kama anataka kuwacha aruhusiwe na alipwe benefit zake. Mtu yeyote ambaye amefanya kazi zaidi ya miaka kumi, akifanya kosa asifutwe bila kupewa chochote. Labda liwe ni kosa kubwa ambalo haliwezi kumruhusu kupata chochote, lakini si vizuri mtu amefanya kazi zaidi ya miaka kumi halafu anafutwa bila benefit, zozote. Hiyo pia iandikwe kwa Katiba kwamba kama hajafanya kosa kubwa zaidi lakini inaonekana kuwa hafai kufanya kazi tena katika idara hiyo, afutwe in public interest na apewe benefit zake.

**Com. Zein:** La mwisho?

**Oliver Matwee:** Mwisho nilikuwa nataka kuzungumzia habari ya wanyama.

**Com. Zein:** Ni sawa, haraka

**Oliver Mwatwee:** Zamani kama ni National Cake, hawa wanyama ambao wako porini wamekuwa wengi sana. Kama Nyati, wakati wa National Celebration kila division ama kila district achinjwe mmoja watu washerehekee. Hayo ndio mapendekezo

yangu.

**Com. Zein:** Okey, Ahsante ni sawa sawa basi maliza sasa. Uliongea jana na tena saa hizi unaongea, jaribu kumaliza. Kuna wengine ambao hawajapata nafasi ya kuongea.

**Oliver Mwatee:** Okey, ahsante sana nitaachia hapo

**Com. Zein:** Mwasi Mwanyumba

**Mwasi Mwanyumba:** Bwana Commissioner na wananchi nafikiri mengi nilikuwa nimetayarisha yamesemwa na wale waliotangulia kusema. Kwa hivyo yangu itakuwa pengine kupitia haraka haraka. Jina langu naitwa Mwasi Mwanyumba.

Kwanza, habari ya utangulizi wa Katiba umetajwa na mmoja aliyesema hapa. Lazima Katiba hii iwe na utangulizi. Kusema inatuelekeza vipi ili kufikia upeo wa amani. Inatuelekeza vipi ile kufikia upeo wa ufanisi, prosperity, inatuelekeza vipi ili tufikie upeo wa umoja wa kitaifa. Kwa hivyo, mambo kama hayo na mengine yatakayo-fikiriwa, yawe ndio mwongozo, torch ya kuelekeza Kenya inaenda wapi. Habari ya Katiba yenyewe. Uwezo wa Katiba yenyewe. Uwezo wa Katiba ni kitu cha muhimu ambacho kimetumia pesa nyingi za wananchi nani wakati mrefu wa wananchi sasa hivi kutengeneza Katiba. Kwa hivyo, hakuna haki watu mia mbili na ishirini Nairobi kugeuza kazi ya watu wote hawa wa Kenya, milioni thelathini ilindwe. Na mawazo yetu tuliyofikiria upande ule ni kwamba ikiwa kuna vipengele rahisi rahisi ambavyo mnaeza mkarekebisha kwa manufaa ya nchi, basi vitangazwe hadharani kupitia vyombo vya habari. Tanataka kupindua vipengele hivi, hivi, kwa sababu hii na hii. Wananchi waijadili mashabani wa-kilima, wakienda mtoni wakichunga ng'ombe wao, wakizungumza juu ya kipengele hicho halafu kutakuwa na njia ya kufanya kusikia maoni wananchi wanasema je.

**Com. Zein:** Sawa sawa, tumeelewa hiyo

**Mwasi Mwanyumba:** Ikiwa ni kipengele kizito, basi hiki kijadiliwe na kifanyiwe National Referundum zipigiwe kura ili kulinda Katiba yetu isije ikachezewa na watu wawili watatu kwa manufaa yao.

Habari ya urayia, nafikiri hii imekuwa ni hali ambayo inataka utalaam. Na Kenya ikiwa moja ya nchi zilizoko ulimwengu huu hatuwezi tukasema twataka citizenship ya Kenya iwe hivi hivi na tukapitana na wengine tano. Kwa sababu hata wa Kenya wataenda nchi zingine. Kwa hivyo tumeona wale ma-Commissioners watakao-angalia mambo ya citizenship walinganishe sawa na nchi zingine za kidunia.

Habari ya usalama tumesema ikiwa kuna haja ya kutangaza hali kama ni hali ya hatari, isiwe jukumu la mtu mmoja. Wacha Rais atangaze akishirikiana na parliament. Asitoke asubuhi nyumbani kwake aka-declare emergency. Liwe ni jambo ambalo

litajadiliwa katika bunge, ndio liweze kutangazwa.

Habari ya vyama vya kisiasa, political parties nafikiri saa hii ingawa ni vizuri lakini vimekuwa vingine kama vya kienda wazimu. Forty four sijui forty five sasa. Nafikiri vingine hata havina manufaa. Wacha, mimi nafikiria katika maoni yetu tulifikiria vitatu au vinne vinaweza kuwa vyama vizuri. Na hivi vyama, nafikiria watu waunde vyama vyao waviendesha na wavi-finance wenyewe. Itakuwa si sawa sana kutumia National finance kuendelesha vyama kila mahali. Hizo pesa wananchi wanahitaji kutengenezewa bara bara, sio kuendesha vyama kile na kile. Kwa hivyo financing ya political parties iwe ni wenyewe. Na vyama tumesema viwe minimum vitatu. Visiwe kama ilivyo sasa.

Habari ya type of Government ambayo inatakikana na wananchi wa Kenya wengi wamesema majimbo, hata mimi nasema majimbo. Tunasema majimbo lakini hayo majimbo lazima kitu ambacho cha muhimu sana kwanza ni wananchi wageuze nia zao. Kwa sababu leo mkinichagua niwe mkubwa wa jimbo hapa hata mimi nita-angalia kwangu mimi nilipotoka kutoka ile sehemu nyingine pale. Kwa hivyo kidogo, kitu kinachotakikana ni nia za wa Kenya zigeuke, waone Kenya kama kitu kimoja. Lakini kwa mapendekezo ni kwamba tunataka feferal government ambayo itakuwa na powers zigawanywe. Wengine wamesema mambo kama usalama na nini iwe katika national. Halafu hizi zingine, bara bara, mashule, ma-dispensary, tunaweza kuyaendesha wananchi hapa katika jimbo letu.

Halafu, habari ya bunge lenyewe, za legislature vile tunafikiria tunasema pia hii ni lazima iwe na mwenzake, to counter balance the powers. Kwa sababu hili moja tumeliona tumekaa nalo na limetuletea matatizo.

**Com. Zein:** Hizo zote umeandika katika hiyo memorandum yako mzee. Pick the most important. Tutajisomea hapa tu.

**Mwasi Mwanyumba:** Halafu lingine ambalo tulikuwa tume-discuss pia ni kwamba hii parliament ipewe uwezo wa ku-vet wale ambao wanao takikana kufanya kazi ofisi katika za umma wazungumzwe, wajadiriwe wa onekane wanafaa waingizwe kazi. Kama hawafai watoke waende nyumbani.

**Com. Zein:** Okey la mwisho sasa?

**Mwasi Mwanyumba:** La mwisho ni habari ya mashamba na property. Hizi tunataka habari ya state land, whatever iondoke sasa. Na zaidi ya yote, hatuna haja na office ya land commissioner. Hiyo ofisi iwe abolished. Imeumiza wanachi. Iondolewe kabisa. Mashamba, ardhi yote ya Taita wacha iwe controlled by the Taita chini ya county council, local government. Halafu mali yote inayotoka pale, ije kwa wananchi wa pale halafu tuangalie ni sehemu gani tutapeleka share katika National Treasury. Hiyo tumesema hivyo.

Habari ya Culture, nafikiri ni important, hakuna mtu ametaja hiyo. Hapa nimesikiliza hakuna mtu aliyetaja culture. Tumeonelea

kwamba kuna umuhimu either kamati hii ndogo au Commissioners ndio wachukue the best cultures all over the country, halafu siwe harmonised.

**Com. Zein:** Mzee wangu sasa dakika tano zimeisha na ninakwambia hivi, tutajisomea hizo makaratasi zote. Tafadhali tuwapatie wengine nafasi nao.

**Mwasi Mwanyumba:** Nimemaliza. La mwisho

**Com. Zein:** La Mwisho basi.

**Mwasi Mwanyumba:** La mwisho ni hizi ambazo hazi-kutajwa na constitutional offices. Ziko kadha wa kadha. Mimi nafikiria moja ambayo haiko na nafikiri ni ya muhimu ni hii ya ombudoman. Ninapendekeza kwamba kuwe na ofisi ambayo mwananchi akikanyangwa sana anaweza kukimbilia. Kwa sababu sasa ukikanyangwa na hawa admistrators ukienda kwa DO ni the same line. Kwa hivyo tunataka hicho kitu kiwe hapo.

**Com. Zein:** Ahsante sana Mzee. Peana hiyo karatasi, memorandum hapo. Douglas Mbela, Na tafadhali usinisomee hicho kiji karatasi hapa. Nitajisomea mimi mwenyewe. Tunaelewana? Kwenda kwa point, briefly maanake kuna watu ambao wanataka kuongea wengine.

**Douglas Mbela:** Ahsante Bwana Commissioner na wenzangu. Kwanza nina haja kukaribisha Commissioners hapa Tausa. Hata nasikia mlikuwa na shughuli nyingine hapa mbele kwa hivyo hapa mjisikie mko nyumbani. Tulikuwa kwa group na tumegawanya kwa mamlaka kwamba kila mtu ataje jambo fulani na nimeomba tu ikiwezekana, mimi nitasema tu haraka haraka yale ambayo ni ya muhimu halafu hao watatu waliobaki waje wamalize vile vipengele ambavyo tulikuwa tumepanga kila mtu tusi-emphasise kila mmoja badala ya kuja kuzungumza zote pamoja.

Jambo la kwanza nataka kusema kwamba Kenya ilikuwa na Katiba yake. Nilisikia kitu kingine hapa kwamba Kenya haikuwa na Katiba. Kenya ilikuwa na Katiba yake kwamba ya kwanza ya uhuru, ile ambayo tunaita ya majimbo. Tuna madaktari katika bunge tuna ma-lawyers ambao wana shughuli nyingi ambazo ….(Tape tripped)

**Com. Zein:** Bwana Mbela, wacha nikuambie hivi, kwenda kwa pendekezo. Twende kwa recommendations. Juu hizo zote hazitaingizwa, hiyo historia ni sawa lakini hatutaiweka kwa Katiba mpya. Kwenda kwa pendekezo.

**Mbela:** Mimi nataka kusema hivyo, nasema hivyo kwa sababu fulani. Kwa sababu kuna jambo limeenea katika nchi. Kama ambao hatukuwa na Katiba. Na nilikuwa nataka ni-emphasize kwa Commissioners hii kwamba kuna Katiba ile yetu ya kwanza ya uhuru ambayo, ndio sisi watu wa hapa tulikuwa tunafikiria iwe chanzo cha Katiba mpya ambayo ita-tengenezwa.

Hiyo iwe foundation ya hii Katiba, isiwe ni ile ambayo tumefanyia amendment. Iwe ni ile Katiba yetu ya uhuru, ndio nataka iwekwe ndio tulikubaliana sisi kwamba ingewekwa kama msingi wa kwanza. Katiba hiyo ni Katiba ya majimbo, ni ya Federal Constitution na ilikuwa na vipengele vya maana. Kwanza, kulikuwa na chamber mbili, Senate na house of representatives ambayo ingefaa irudishwe kama vile ilivyokuwa hapo zamani. Tulikuwa na regional assemblies, ile majimbo ambayo watu wetu wanataka irudishwe. Kulikuwa na serikali za district level ambazo ndio tunataka zirudishwe. Hizo level tatu za serikali tumekuwa na haja nazo zirudishwe. ndio maana nikasema nataka hiyo iwe foundation. Watu wetu wanafikiri wanajua, wanasema iwe hiyo foundation ya Katiba ambayo tunaitengeneza. Ile Katiba iliyo-pigwa pigwa makosa imeturidisha. Sasa hatungeenda huko kama hatungegeuza hii Katiba, tungekuwa sasa tumeendelea mbele. Nataka kusema hapo kuwe on record kwamba nchi nyingi kama Uganda, Tanzania, Zambia hata South Africa ile ambayo ni kubwa na nchi nyingi ambazo zimetunga Constitution kama Nigeria zimetunga Constitution ya majimbo. Nitatumia hilo jibu la majimbo sababu zote ni za majimbo na hizo zimefaa hizo nchi zote sana.

**Com. Zein:** Dakika tano sasa zinaisha mzee wangu.

**Mbela:** Kuna kitu ambacho nilikuwa nataka ku-emphasize sana nani mambo ya sheria za ardhi. Sisi waafrika na mimi nasema kama Mwafrika na kwetu hapa Pwani na hapa kwetu Taita Taveta Waafrika tulikuwa na sheria zetu za Ki-tribe, za kikabila. Na hiyo siku-sema kwamba ni kitu kibaya. Tuli-inherit kutoka kwa Musa, nabii Musa vile alivyoambiwa na Mungu, sheria ya Mungu mwenyewe alitunga akawapa wana wa Israel, twelve tribes na zikagawanywa kule Caanan, na zika-gawanywa zikapewa ardhi yao. Sisi tulikuwa na zetu zilikuwa zinafanana na hiyo.

**Com. Tobiko**: So pendekezo ni gani kwamba tuweke kwa Katiba mpya? Katika katiba turidishiwe ardhi. Mambo ya ardhi ,"Land" yarundishwe tribal. Yarundishiwe tribe. Tuna tribe na community. Tuna tribal, tuna family tunaende kwa clan, halafu tunaenda kwa community halafu tunaenda kwa tribe. Hiyo ndiyo sound foundation ya land ownership in future. Turudi pale pale tulikuwa.. Na nasema hivyo kwa sababu hata katika Katiba ya majimbo ilikuwa imefanya hivyo, imeweka mambo ya ardhi katika regions.

**Mbela:** Kuna jambo lingine la muhumi ambalo nilikuwa nataka niseme lilikuwa ni bunge. Kwamba bunge lingekuwa na Chambers mbili, Senate na House of Representative. Hilo ndilo jambo nilikuwa nataka, kama vile ilivyokuwa pale mbele. Nataka lirudiwe.

Kwa upande huu executive, yani President nataka kuwe na president na Prime Minister. Kuna Constitution nyingi moja ni kama ile ya America na kuna ya India ambayo ni nchi ambayo iko kama sisi ambayo in Chief Minister ama Governor. Wa America ni Governor, wa India ni Chief Minister. Kuwe na ma Chief Ministers ambao watakuwa in-charge of the regions. Halafu hapo chini, ma-DC, Provinicial Commissioners, waondoke kuwe na Civil Secretary. Tusiwe na PC, tuwe na Civil Secretary kama vile Governor.

**Com.Tobiko:** La mwisho maanake tutajisomea hilo karatasi. Si umeandika zote hapo?

**Mbela**: Nimetaja isipokuwa moja ya ma-Chief.

**Com. Zein:** Chukuwa moja la mwisho.

**Mbela:** Moja ambalo sikuwa nataka ni-wache ni la ma-Chief. Ma-Chief walikuwa ni wetu hata wakoloni walipokuja walitukuta na ma-Chief na wakawa chukuwa wakawafanya heads ya zile location ambazo zilikuwa ndio centres za administration. Ma-chief walikuwa wana report directly kwa DC. Sasa tunataka ma-Chief, kama vile walikuwa wakichaguliwa zamani, hata sasa warudi kama zamani, wachaguliwe, wazee kati ya wazee wenzake, wazee wenye wisdom. The wise the wise, men of the area.

**Com. Tobiko:** Okey.

**Mbela:** Wawe elected as Chief, Assistant Chief, na watu wake wale wawe elected.

**Com. Tobiko:** Ahsante sana mzee wangu. Peana karatasi pale. Tutachukuwa hiyo karatasi, hiyo memorandum yako tutachukuwa. Christopher Mwakau? Mzee wangu nenda kwa ufupi maanake bado tuko na list kubwa sana.

**Christopher Mwakau:** Yangu ni machache. Kwa upande wa majimbo, hiyo ni maoni ya kwanza, tunataka majimbo.

La pili ni vyama, vyama viwe viwili tu. Yaani Upper House na Lower House.

La tatu, ni Local Government. Nataka Chairman wa County Council achaguliwe na watu wote. Hapana achaguliwe na Cabinet. Achaguliwe na wananchi. Utawala wa mali ya asili, utegemee mahali ile mali asili iko na watu wa pale. Nafikiri mnaelewa.

La tatu, mashamba, maamuzi yake yawe yakiamuliwa na wale ambao wanahusika na mahali pale.
Mwisho, Rais apewe mamlaka lakini apimiwe hiyo

**Com. Tobiko:** Aongezewe ama apunguziwe?

**Mwakau:** Apunguziwe.

**Com. Tobiko:** Ahsante sana. Jiandikishe pale. Edward Mangole.

**Edward Mangole:** Commissioners langu ambalo ningetaka kusisitiza ni moja tu. Na inahusu hii wildlife. Sehemu yetu kubwa kama mlivyo-sikia, sixty five per cent imechukuliwa na wildlife. Wildlife hii inatunyanyasa kila siku. Tungetaka kama kweli inavyosemekana, pesa nyingi zinaletwa na mambo ya wild-life, sisi wenyeji wa hapa ziwe ni zetu kama seventy five per cent. Sababu yake, wanaoumia ni sisi kwa kuharibiwa mimea yetu, hata watoto wetu kuuwawa. Lakini hakuna chochote tunachopata na kama kuna pesa zinazoingia, kwa serikali, hivo ni kweli, hakuna Mmbololo hapa ama Mtaita hapa anazifaidi. Kwa nini tuwe nayo, na sisi tuliilinda jadi? Hilo jambo liangaliwe. Senti ambazo zinaingia kutokana na wildlife, seventy five per cent iende kwa Wataita ama kwa watu hawa wa pwani kwa jumla.

Na sehemu nyingine ni hii wire chain link wameeka hapa ya moto ambayo inazuia wanyama. Tunaona wazi kwamba hiyo si kuzuia wanyama wa pori, ni kuzuia ngo'mbe wetu wasiingie hapo. Maanake, mnyama wa pori tunawapa kila siku, faini twa-pigwa ngo'mbe akiruka akiingia pale. Je, wanyama wao wakija hapa kama atakuwa anaingia hapa na kule watu wetu wanafukuzwa na bunduki, wakiingia kwetu hapa, wanyama wao tuwafukuze na mishale. Ikubaliwe hivyo nafikiri kwa hayo machache, ningeachia hapo.

**Com. Tobiko:** Ahsante sana.

**Interjection:** People clapping.

**Com. Tobiko:** Reverend Shake?

**Interjection:** Ameenda

**Com. Tobiko:** Stephen Kifuso

**Stephen Kifuso:** Commissioners na wananchi hamjambo? Mapendekezo yangu ni kama ya- fuatavyo. Kwanza, napendelea serikali ya majimbo.

Pili, napendelea Ofisi ya Chief na Assistant Chief ziachiwe VDC, Village Development Committee kwa sababu hao ma Chief wananyanyasa watu, hata mpaka serikali ikidharauliwa, inadharauliwa kwa sababu ya hao ma-Chief. Mara nyingi hata wanachukua kuku wa watu.

**Com. Tobiko:** Hiyo tunaelewa mzee. Ahsante

**Interjection:** Laughter

**Kifuso:** Halafu point nyingine ya tatu ni kwamba President apungiziwe madaraka yake. Napendekeza pia ile mikono mitatu ya serikali iwe independent na hapo President hata-pata nafasi ya kuweza kunyanyasa watu. Point nyingine ni kwamba, Rais achaguliwe kwa vipindi viwili tu. Hata kama amekuwa mzuri, vipindi viwili vikiisha, basi aondolewe.

Ingine ambayo napendekeza ni kwamba, jinsi wengine walivyosema kwamba sehemu kubwa yetu sisi imeingia katika national park. Iweze kuwekwa mikononi mwetu ili tuweze kutumia hiyo sehemu jinsi tunavyopenda. Kuna wananchi wengi ambao hawana land ambao ingalipasa ipunguzwe ipewe wananchi.

Ningalipendekeza pia mishahara ya watu wakubwa ipunguzwe na iwekwe kamati ambayo inaweza kuchunguza hiyo mishahara. Kuna watu ambao wanapewa elfu nne, hapa chini kuna watu ambao wanapewa milioni moja. Tunaomba hiyo mishahara chini na mtu mkubwa. Ili tusiwe na gap kubwa.

Ningelipendekeza pia tuwe na Prime Minister. Pia ningelipendekeza kuwa kuna watu ambao wamechukua land kubwa na kuna wengine ambao hawajapata kitu na labda wana nusu hata nusu, ya acre, hawana mahali pa kujenga. Basi wale ambao wana land kubwa iwe kamati au watu ambao wanaweza kuangalia kwamba wapunguziwe, hiyo land igawanywe kulingana na jinsi population ilivyo. Na zaidi kama mtu anaweza kuwa na land kubwa, basi iwe acre ishirini. Yangu ni hayo tu.

**Com. Tobiko:** Ahsante sana mzee wangu. Ahsante kabisa. Na twende kwa Ezekiel Mboe.

**Interjection:** Ameenda.

**Com. Tobiko:** Fatuma Naindoki:

**Fatuma Naindoki:** Mimi naitwa Fatuma Naindoki. Mimi napendekeza kwa mambo ya waislamu. Napendekeza katika shule za primary ziwe na walimu wa kiislamu. Sababu tunaona katika mashule hakuna walimu wa kislamu na watoto wengi hawaelewi mambo ya kiislamu. Unakuta mtu huyu mwislamu lakini anaimba nyimbo za kikristo. Hata ukimuuliza sura ya kwanza katika Quran, inasemaje, yeye hajui. Mimi napendekeza hiyo majimbo katika Katiba ituletee kila shule mwalimu wakislamu.

Na mengine nataka kuyasema haya mambo ya kuzalisha wanawake. Naona kuna wanaume wanazalisha wanawake. Sasa nikependelea tufanyiwe wanawake badala ya wanaume. Kwa sababu kuna wanaume wanawazalisha wanawake. Haya ndio mapendekezo yangu.

**Com. Tobiko:** Ahsante. Umemaliza? Ahsante. Jiandikishe pale. Magdalina Adele, Margaret Samba.

**Margaret Samba:** Mimi nasema sijui Kiswahili sana. (Taita dialect)

**Translator:** Yeye anasema hivi, kwa sababu wao walikuwa na vikundi vya akina mama, basi vikundi vya akina mama wanakuja tutoe pesa shilingi mia moja, moja, katika nchi yao ya Mbololo. Basi wakatoa pesa zao. Basi walipo-endelea na kikundi hakuna siku wamepata matunda juu ya kikundi hicho. Na pesa zao zimepotea Mbololo nzima. Kwa hivyo, wao ni akina mama wakubwa hata hawajapewa ardhi ili walime, basi wakaambiwa kuwa watapewa shamba walime, basi wakanunuliwa ng'ombe, ng'ombe wakapotea, shamba ikapotea na pesa zikapotea, hata hawakupata faida yeyote. Maoni yake ni kama, wakiwa wanachaguliwa watu, wachaguliwe watu watakao watetea akina mama wakubwa. Hivyo ndivyo mapendekezo yake kulingana na vile walivyo katika vikundi vyao. Kundi cha pili, ilikuwa ni plan. Basi walipo-kaa na plan, wakaambiwa watoe shilingi mia moja kila mmoja. Basi wakakaa, kidogo wakaambiwa basi nyinyi kina mama wakubwa, hamuwezi kupata chochote. Basi hata vitu vya Plan International vilipo- kuja hawakupata kitu. Mpaka leo hivi wako katika nyumba za nyasi. Wananchi wanachaguana wao kwa wao. Kwa hivyo nimependekeza kuchaguliwa watu katika nchi yetu, waendelee kuchagua watu kwa kwel, pesa zetu zisipotee na watu wakubwa, hayo ndiyo yangu.

**Interjection:** Clapping.

**Com. Tobiko:** Ngao Thomas. Hayuko? Johnson Mwakio? John Mganga? Danson Igomba?

**Danson Igomba:** Commissioners, mimi ni Danson Igombo na ninawakilisha vijiji vitatu. Ijapo mengi yamesemwa, ningependa nisisitize tu machache.

La kwanza ni kwamba tuna sisitiza tuwe na majimbo. Na baada ya kuwa na majimbo, nafikiri itakuwa vyema kama kila jimbo litatengeneza Katiba yao ambayo itasisitiza juu ya uongozaji au juu ya uongozi katika kila jimbo.

Jambo lingine ambalo ningesisitiza ni kwamba tunazo rasilmali kadha wa kadha katika hasa wilaya yetu . Tungeomba kama ingewezekana, Katiba hiyo, jambo moja wapo liwe ni kwamba rasilmali yetu iwe mikononi mwa wenyeji.

Jambo lingine ambalo tumeona limendelea kuzungumzwa sijui juu ya wasichana wanapata mimba, juu ya haki ya ardhi, juu ya akina mama kuridhishwa,na kadhalika tunaona kwamba kila kabila nafikiri liko na mila na utamaduni wao. Kwa hivyo, ningesisitiza ya kwamba katika Katiba hii mpya mila na utamaduni zitambuliwe na Katiba. Kwa hivyo kama wataita mila inasema wanawake waridhishwe mali, basi wafuate kulingana na mila yao.

Jambo la tatu ambalo ningezungumzia ni kuhusiana na title deed. Tumeambiwa ya kwamba kuna Game Park, Tsavo na

kadhalika. Kwamba wao walipatiwa title deed. Lakini tukiangalia sisi wataita, title deed kupata ni shida. Kwa hivyo jambo ambalo mimi ningefurahia ni kwamba mambo ya title deed yaondolewe na yanapo ondolewa sasa tutauliza ya kwamba, sasa tutafanya namna gani? Kuna kamati za local ama local community. Ikiwa kuna kamati za wazee, basi wahusike katika kuangalia mambo ya mipaka.

Jambo la nne ni kuhusiana nguvu za President ama Rais. Tumetengeneza memorandum, kwa hivyo hatutazungumzia mengi. Lakini moja ambalo nitaongea ni kwamba, ako na maamraka juu ya kuteuwa. Tunasikia ameteua Tume, ameteua ma-councillors, ameteua wabunge na kadhalika. Kwa hivyo, hiyo iondolewe.Nguru zingine za kuondolewa tumeandika pale.

Jambo lingine ni Chiefs na Assistant Chiefs. Hao wateuliwe na wananchi wenyewe. Halafu kuhusiana na basic rights, sitaongea juu ya basic rights nyingi, lakini nitaongea juu ya mbili tu. Ya kwanza ni transport and communication ama usafiri na mawasiliano. Nafikiri tutakumbaliana hapa, hawa wananchi tumekuja hapa, kuanzia Voi mpaka Ndome. Ikiwa umeingia gari, utakuta kuwa ni shilingi hamsini. Uwe umeshukia Ikinga hamsini,

**Com. Tobiko:** Pendekezo ni gani?

**Igomba:** Pendekezo, ningependelea ya kwamba, hali kama hiyo, wananchi wenyewe wahusishwe ili kwamba watoe mawaidha yao ama kama ni kukataa hali fulani, basi wao wako na right ya transport and communication. Pendekezo la rights pia katika elimu, iwe ya lazima especially primary level. Iwe ya lazima na ya bure. Lakini katika hiyo bure, ningependa kusisitiza kwamba lazima kuwe na mwongozo. Iwe ni ya lazima na ya bure na iwe na mwongozo. Ninapo-sema hivo ni kwamba…….

**Com. Tobiko:** La mwisho, pendekezo la mwisho, umeandika? Umesema kuwa kuna memorandum. Pea wengine nafasi ambao hawana memorandum.

**Igombo:** Okey. Ahsante.

**Com. Tobiko:** Rodgers Mwanyika, Neal Mwawazi? Michael Ndeleko? Nelson Mambo? Raphael Kitegwa?

**Raphael Kitegwa:** Ahsanteni sana kwa kufika hapa. Mimi pendekezo langu, kama mzee mmoja wa kijiji alisema hapa, pendekezo langu ni hawa wazee wa vijiji wawe na vitambulisho vya serikali. Maanake anaweza kutoka akaenda akaumia, asijurikane ni nani.

Pendekezo langu la pili. Napendekeza kwamba serikali irudie kusimamia bei zote za bidhaa. Maanake hao watu wa ma-wholesale wanatunyanyasa. Ukienda kununua kitu leo unakutua tena bei kesho ukija, sio ile. Na wewe mwenye kuuzua

moja moja huna chochote unapata. Hilo ni pendekezo.

La tatu, naunga mkono mambo yale ambayo tulikuwa tumeyaandika yote na yaunga mkono. Ma-Chief wawe wakichaguliwa na wananchi. Tena ma-chief wawe wakifanya kazi nzuri. Na katika location, chief yeyote akikutwa 'mpangala' inaendelea, afutwe kazi.

Langu la mwisho ni turekebishe hii Katiba, tumekaa nayo sana.

**Com. Tobiko:** Ahsante sana. Jaindikishe pale. Ibrahim Mjomba? Arnold Shagala? Nelson Mwakio? Tony Mwafiswa,? Mathew Muada? Leah Juma? Uliongea jana, sio? Unataka kuongeza? Lakini tafadhali kwa ufupi uwache wengine ambao hawakupata nafasi.

**Kitegwa:** Lile moja nilikuwa nimesahau, sisi wataita wa hapa tumelaliwa sana kwa sababu nikifungua radio, unakuta station ya Kikuyu, unakuta Kalenjin, utakuta Kikuria, Mtaita hayuko ndani. Tuwekwe ndani. Pendekezo langu ni hilo.

**Com. Tobiko:** Basi sawa sawa.

**Leah Juma:** Jina langu ni Leah Juma. Box yangu ni arubaine na nane, Voi. Pendekezo langu, nashukuru sana kwa sababu tuko katika nyumba ya Mungu, tena nimefurahi sana. Pendekezo langu, naomba tena twashukuru sana kwa sababu serikali yetu imetukumbuka.. Pendekezo letu, mambo mengi tunazungumza lakini hayafanyiki. Kwa hivyo, tunataka hii Katiba ikiundwa, ikienda, tena pia irudi ndio tujue kama maneno yangu yameungwa mkono, yamekubariwa ama ni vipi? Ndilo pendekezo langu hilo.

Pendekezo la pili naomba yaani kila mahali ambapo ni kwa wananchi wenyewe, yani kila mtu apewe uwezo wa kuweza kuongea kile kitu ambacho anaona kinashida pale. Sio kuongea pande nyingine. Kwa hivyo, nimeona mapendekezo yangu ni hayo.

Kitucha tatu, mimi naomba kwa unyenyekevu, na tena naomba sana kwa uzito. Rais wetu tunampenda sana na Rais wetu tunampenda zaidi. Kwa hivyo wakati atakapo-jiuzulu, arudi hapa kanisa ili tuje tumuunge mkono. Maanake tunasikia tukifungua radio tunasikia kila wakati anashiriki katika kanisa fulani. Kwa hivyo sisi wataita tunaomba aje hapa tumuunge mkono.

Kuna pesa zimetolewa ambapo ni za wanyama kama wameharibu mimea yetu. Na wanyama wameharibu mimea yetu, tumesikia kwa radio pesa zilitolewa. Na hizo pesa hatujapata kujua kwamba hizo pesa tutazipata kivipi. Kuna wamama wengine wazee, kama yule mama alikua anangoa hapa, nyanya yangu. Kwa hivyo, tunataka hizo pesa zirundi kwa wananchi

sije zijulikane, zitangazwe ni watu wangapi mimea yao ililiwa na wanyama, na pia ni watu wangapi walio umizwa na wanyama maaanake ukiwa mtu wa pale pale, unajua ni wangapi. La pili……..

**Com. Tobiko**: La mwisho sasa

**Leah Juma:** La mwisho tunataka wabunge pamoja na ma-councillors, tukichagua tunajua ile kazi tumewatuma watufanyie, wawe wakituambia wamefikia wapi na wameendelea wakafika wapi. Na wakipatiwa tender yeyote ya kufanya kama ni bara bara ama ni kisima, kama kile cha Kiwongo ama ni maji, tujue zile pesa alipatiwa pale ni ngapi na wale amepatia tender ni kina nani. Kwa hivyo, tunataka tuwe tukijua mambo yetu sisi wenyewe wananchi wa pale.

Na la mwisho, nataka kusema juu ya mpaka. Mpaka tunajua tumenyanyaswa sana. Mpaka umerudishwa rudishwa sana sana. Kwa hivyo tunataka mpaka wetu urudi sawa sawa tukijua tuna watoto wetu wamepata mashamba, ambayo tumewazalia nje ya ndoa. Na vijana wetu hawana kazi, tunawataka walime shamba wapate kujimudu sio kuvuta bangi na kunywa 'mpangala'. Hatutaki namna hiyo. Lingine tena….

**Com. Tobiko:** Mama, sasa la mwisho tena?

**Leah Juma:** La mwisho tena, tunataka vile vikundi vya akina mama ama vikundi vyovyote ambavyo ni miradi ambaye iko na certificate, mtu asiwe Chairlady pande hii tena awe Chairlady pande hii. Labda nimeharibu pande ile tena nataka kuingia pande ile. Kwa hivyo tunataka vile vikundi viwe wazi tukijua pesa zitaingia vipi, pesa zitatoka namna gani. Kwa hivyo, tunawaomba, mambo hayo, Katiba hii ya sasa, ituangalilie sana sana maanake tumenyanyaswa, pesa zetu zimeliwa tunapata taabu, vijana wetu wanaendelea kuiba mbuzi wauze wapate 'mpangala'

**Com. Tobiko:** Ahsante Mama. Jiandikishe pale. George Mwajulo? Hayuko, Reverend W Zoe? Donald Mwedevo, hayuko? Satim Mkala, hayupo? Jared Mwandela? Paul Mwakingali? Dalius Mwasi? Raphael Mwalenga? Leah wakupwa? Grace Mkochi? Lepati Mwalenga?

**Leah Juma:** Mimi nimesahau moja. Moja tu. Tu moja na sio mchezo.

**Com. Tobiko:** La miwhso mara ya tatu?

**Leah Juma:** Moja tu. Kuna makanisa, tunataka makanisa haya ya-chunguzwe. Na kuna manabii. Tunataka kama vile ndugu yetu mwingine alisema hapa ati watu wadungwe sidano wakufe. Tunataka makanisa, ikiwa wewe umeokoka na kabisa umesimama kabisa mbele ya mwenyezi Mungu na unaabudu Mungu aliye hai na alikuwa akitenda miujiza, watu wawe wakiletwa makanisani, waombewe na wapone.

**Com. Tobiko:** Sawa sawa. Tumesikia. Ahsante. Robert Mwalenga?

**Robert Mwalenga**: Mimi Robert Mwalenga, ninataka kuongeza tu mawili au matatu juu ya yale yote ambayo mengine yameandikwa iko hapa. Nachagua hivi, kwanza nimeunga mkono mambo ya Katiba mpya. Hii irekebishwe na iwe na provisions kama vile zingine zimetajwa, serikali ya majimbo, iwe na President, iwe na Prime Minister na iwe na zile nyumba, Upper House na Lower House. Hivyo.

Mengine yaliyosemwa zaidi sana sitayarudia isipokuwa, nilipokuwa ni-kindelea kusikiza, nimepata matatu. Kwanza ni kuhusu banks zile ambazo zina-wanufaisha wananchi hapa. Zaidi sana ningeomba hii Katiba mpya iwe na provision juu ya banks. Yaani ziweze kuwa na uniformity. Kwa sababu kuna banks zingine ambazo ziko katika nchi lakini zinasumbua wananchi. Zina charges kubwa kubwa. Kwa mfano kama hii KCB. Hii unakuta watu wanapata pesa kidogo. Wakiweka pesa zao pale, zina charge-wa hata zinaisha kabla ya nini? Kabla mtu hajachukuwa. Kwa mfano kuna bank moja ile Habib bank

**Com. Tobiko:** Tafadhali tuachane na mifano. Nini pendekezo lako?

**Mwangela:** Napendekeza kwamba ziwe na uniformity katika charges. Zingine ziko juu, zingine ziko chini.

Pili nimepata jambo fulani ambapo msemaji mmoja alisema habari ya prison. Ningependekeza kwamba wale wafungwa wengine pengine ambao hawana ujuzi sana, ama pengine wana ujuzi, prisons zingine ziwe na access ya kuwekwa pale along the Great Rivers ili badala wafunguwa pengine kufungwa kwa miaka mingi ama maisha, wanawekwa tu kufagia fagia njia na kufanya fanya nini, wapelekwe katika shamba ama watengeneze shamba along the Great Rivers, kama Tsavo, kama Athi river na zile zingine kubwa, along them. Halafu wawe wa-kilima kama ni miwa, Kenya iwe self sufficient.

Tatu ni kama nilikuwa nimeshindwa na hii wakati mwingine juu ya uchumi wa Africa. Uchumi, tafadhali hapa kwetu, umeenda na watu wengine. Lakini, unakuta sasa wale kama ni Voi pale, watu ambao wana baishara zao ndogo, ndogo wameshindwa kabisa na supermarket ambazo zina watu wale ambao walifanya training mapema. Ningeomba kama kungekuwa na provision katika Katiba ya kuwangalia wale watu, wasifinywe sana na wenye ma-supermarkets.

**Com. Tobiko:** Ahsante sana. Na kuna Pastor Philip Ladi. Mzee jiandikishe pale.

**Philip Ladi**: Mimi kwa majina naitwa Philip Ladi. Kuna mengi ambayo nili andika lakini yametajwa tajwa. Machache nitataja ya Rais. Apunguziwe mamlaka asiwe juu ya sheria. Nita taja parliament…….

**Com. Tobiko:** Endelea kutaja na utoe pendekezo.

**Ladi**: Parliament iwe na nguvu yaku dissolve the parliament. Pendekezo lingine la pili, hospitali ile cost sharing. Sababu wananchi wanalipa kodi na tunataka hii Katiba ambayo tunaiunda sasa, wananchi wasitozwe ile cost sharing ya madawa.

La tatu mbuga la wanyama wa pori katika Taita, limetuzingira kabisa na tunataka area yetu hii ya Taita tufunguliwe, kama sehemu ambazo tunaweza kuzitaja ziko karibu hapa. Irima, ni pahali ambao huwa tunachunga wanyama wetu ambao watazaidia kwa kusomesha watoto na kupata vyakula vya kawaida, matumizi ya kawaida. Sasa nataka Commissioner hii iyangalie na vile tumependekeza ya kwamba tupewe nafasi ya area hiyo ya Irima

Na latano ni ya kilimo cha maji. Ninapendekeza tumezingiriwa na maji. Lake Jipe liko karibu na Tsavo river. Tupewe nafasi hiyo tupate mashamba ya kunyunyuziwa maji.

Pendekezo langu la mwisho, Councillors wachaguliwe wale ambao wanajua lugha ya kiingereza, kiswahili na hesabu. Nafikiria yangu ni hayo, kwa sababu yametajwa sana.

**Com. Tobiko:** Okey, Ahsante sana. Jiandikishe pale. Nani angependelea kuongea na hajasikia jina lake likitajwa hapa? Mje mbele. Hawa wengine wamebaki nyuma wameshaongea ama hawataongea?

**Interjection:** Observers

**Com. Tobiko:** Okey sawa. Mzee tuanze na wewe.

**Alphonse Kisingu:** Commissioners na wananchi kwa jumla na wasalimu sana. Habari gani?

**Audience:** Nzuri.

**Kisingu**: Mimi singekuwa na mengi ya kusema isipokuwa na….

**Com. Tobiko**: Kwa majina

**Alphonse Kisingu:** Kwa majina mimi naitwa Alphonse Kisingu. Mimi sina mengi ya kuongea isipokuwa yale yameniguza nafikiri ndio nitaongea. Nitaongea kwa kuchanga sana lakini nafikiri kuna watu wa-translate. Kwa ufupi mtaongea juu ya maisha kwa ujumla. Kuna kitu kimeniguza sana, kulingana na hii Katiba tunatengenza, tunajaribu kuunga hii Katiba ili itunufaishe, especially wale watu mapato ya chini ama raiya wa kawaida. Kuna mambo inaendelea kama kwa mfano unaweza kupata mtu pengine ana uwezo amefungua kitu kama supermarket hivi ama ako na biashara, na mtu kama huyo unampata

anaendelea kutumia wale watu hawana uwezo ili kujinufaisha yeye mwenyewe.

**Com. Tobiko:** Pendekezo lako ni gani? Unapendekeza nini?

**Kisingu:** Mimi napendekeza kwamba, mtu akiwa ameajiri mtu, iwe na kiwango maalum kulingana na ile kazi anamfanyisha yule mtu. Kwa sababu kuna watu wanajinufaisha kutokana na maskini. Anaandika huyo anafuta, anaandika mwingine anafuta, hamulipi.

**Com. Tobiko:** Sawa

**Kisingu:** Kwa hivyo, mimi napendekeza mambo kama hayo yachunguzwe sana kwa sababu wanazidi kuumiza wengine ili wao waende mbele. Kitu kingine ni kama kwa mfano vitu kama National Park, na kitu kama, mahali magari yana-charge-iwa hizo pesa huwa zinapotea potea tu. Hatujui huwa zinafanya nini. Kwa hivyo, tunaona tunazidi kwenda chini. Hatuendi mbele. Kuna kitu kama hospitali pia, na serikali inasema inaleta madawa, lakini unapata pande hii kumefunguliwa chemist nyingine, inasemekena ni ya kusaidia wananchi. Madawa ya-kija ya serikali, yanageuzwa pande ile, inageuzwa pesa. Sasa unaona mwananchi anazidi kuumia tu pale pale anazungushwa zungushwa. Kwa hivyo, vitu kama hivyo, kungekuwa na watu wakuchunguza vitu vingekuwa kidogo afadhali. Tunapata kwamba kuna wale watu wana mashamba kubwa kubwa. Na tunapata karibu yote ni pori. Na mtu anasema hii ni land yangu. Kama unapata acre kadhaa wa kadha, zingine pande hii na ile unapata zote hizo ni za mtu mmoja, na hazitumii. Na kuna watu wengine hata hawana mahali pa kukaa. Wamepewa na jirani ama mjomba fulani "bwana jenga hapa"

**Com. Tobiko:** Kwa hivyo unataka tufanye namna gani na hayo mashamba?

**Kisingu:** Kwa hivyo watu kama hao nataka wachunguzwe. Ikiwa kama mtu pengine anaweza kuwa ako na watoto wanne na ako na acres and acres na saa zingine hata ni watu wengine wanachunga huko ndani. Yeye hawezi kutusukumia hizi acres. Unajua kama hujatoa pesa, hizo acres zitakuwa zina-lala tu. Kwa hivyo, watu wengine wanaumia na kuna vitu vya kuwasaidia. Na ni watu wanazikatalia. Kwa hivyo, vitu kama hivyo, vichunguzwe sana.

Halafu pendekezo lingine, kuna yule raiya wa kawaida akienda, pengine akikosewa na yule mtu ako ana uwezo, unapata yule raiya hana kile kitu anaweza kufanya kwa sababu yule mkubwa anaweza kuweka wakili, yule mtu hana pesa na hatafanya chochote. Yeye anawachana na yale maneno kwa sababu yeye hana uwezo. Sasa unapata mtu kama yule anaumia, kwa sababu yule mtu ako na pesa, hata anaweza kuandika wakili. Lakini yale mambo yanaelegeza kwamba yule mtu ndiye mkosa kwa sababu yeye hana uwezo. Kwa hivyo unapata yule mtu anakusukumiwa tu na ni kuomba Mungu.

**Com. Tobiko:** Una recommend nini?

**Kisungu:** Kwa hivyo hicho kitu tuna-recommend kwamba ikiwezekana, hata mawakili pia wawe wale wa kuangalia kama mtu ako na pesa na ameandika wakili na yule mtu mwingine hana pesa kuwe na mpangilio kama huo.

**Com. Tobiko:** Sawa sawa

**Kisingu:** Isiwe kwamba huyu mtu kwa vile ako na pesa ana andika wakili halafu…..

**Com. Tobiko:** Ahsante. Tumeelewa ni sawa.

**Kisingu:** Nafikiri yangu si mengi sana. Nitakomea hapo.

**Com. Tobiko:** Ahsante sana. Jiandikishe hapo.

**Timothy Rudi:** Mimi kwa majina naitwa Timothy Rudi. Yangu nilikuwa nimeandika, nitasoma tu kwa haraka haraka.

There should be no minimum education qualifications for councillors kwa sababu hawa huwa wanachaguliwa na wananchi. Kwa hivyo, haina haja kuwa-wekea kiwango cha masomo maanake hata kazi anaenda kufanya ni wananchi wenyew ndio wanaenda kuamuwa kwamba huyu ndiye anatufaa na ana weza kufanya hizo kazi zote.

Chiefs should be elected by the people. Hao pia wa chaguliwe na wananchi, kwa sababu wananchi wenyewe ndio wanaamua hawa wanaweza kutufanyia kazi. Isiwe kama serikali ndio inachagua wale watu.

The Constitutional review should look into matters of salaries of big people. Maanake hapa kuna watu wanapata mishahara, kuna wengine wanapata kama laki moja. Unakuta mwingine anapata elfu mbili, na wanaenda duka moja. Sukari ni ile ile tu, kama ni shilingi arobainne wote wananua pale. Sasa hapo wakiangalia mambo ya mishahara, wajaribu kuweka sawa maanake huyu mtu mdogo ndio anaumia.

Na kuhusu pension, hapa kuna shida maana unakuta mama au bwana amefariki. Ule mama uwa anapewa ile pension kwa miaka mitano halafu inakufa na swali ni kwamba wakati ule bwana angekuwa anakuwa bado anaendelea kuishi angekuwa anapewa zile pesa. Sasa yule mama wakati yule bwana amekufa, yule mama aendelee kupata zile pesa mpaka naye afe.

Tunaajia kazi, hapa tuseme kwa mfano wakati nilikuwa natafuta kazi Mombasa unakuta watu wanaandikwa kule KPA, sisi tunaenda kule hatuna hata njia yoyote lakini tunasikia watu wanatoka nje wanakuja wanapata zile nafasi na sisi tuko pale hatupati zile nafasi. Kwa hivyo yani ni kama kitu iko kama kwetu kama hiyo KPA iko Coast sisi tupewe hizo nafasi kwanza.

Halafu hata kama zimebakia kuangaliwe kama kuna watu wa inje ndio waje wapewe hizo nafasi.

Na hii kuwa kwa mfano kama N.H.I.F., kwa mfano kama zile kodi tunakatwa, tuseme kama watoto hivi, unakuta mtoto akipita 18 years uwa sasa ile kodi iwezi kumsimamia tena na nilikuwa naona kama hiyo age bado iko chini sana maanake mtoto wa 18 years bado ni mtoto mdogo awezi kuwa hata kujisimamia kwa hivyo bado kama wakati anafanya katika mahali fulani kuna kodi zinakatwa kwa watoto aendelee kuwa anaweza kutumia hizo pesa.

**Com Tobiko**: Asante sana mzee. Jiandikishe pale.

**Austin Kabito**: Commissioners na wale wote wako hapo nawasalimu. Majina yangu ni Austin Kabito Mzee, address ni 1800. kuna kitu kimoja mabacho kiko katika Katiba ile ya zamani wote tunasema uhuru wa kuabudu. Tatizo ni kwamba wanaposema uhuru wa kuabudu hawakufafanua kuna uhuru wa kuabudu kati ya watu wangapi ama vikundi vingapi. Kuna ndugu zetu wa Ijumaa ambao lazima pia wapatiwe uhuru wa kuabudu. Kuna wengine ambao ni wa Jumamosi, lazima wapatiwe uhuru wa kuabudu na wengine wa Jumapili lazima wapatiwe uhuru wa Kuabudu. Lakini tatizo ndipo ya kwamba katika hawa wa Jumamosi hata ukiandikwa katika kazi unakuta kwamba siku ya Jumamosi usipokuja unafutwa kazi. shuleni watoto wanapatiwa tution na siku ya Jumamosi ambapo tena imesemekana kwamba kuna uhuru wa kuabudu, na akikosekana akija anatandikwa. Na tena unakuta ya kwamba kama ni watu wanaandikishwa ukikosekana ya kwamba wewe unasma Jumamosi huusiki na uwezi kuja katika shughuli hiyo unafutwa kazi na ambapo hiyo ni kitu iko katika bibilia, ni kitu ya saba hata Koran inakubali. Pendekezo ni kwamba kama kutakuwa na tatizo kati ya mtu ambaye anaye funza Jumamosi ama wa Ijumaa anatatizwa na kuabudu kwake, anakatazwa kuabudu, kuwe na mahakama, mtu anaweza kwenda hata Voi ashitaki kwa nini mimi ninasumbuliwa katika dini na kuna uhuru wa kuabudu.

Halafu tatizo la pili, katika hiyo mzima spring iko wapi, hii ni mali ya asili, kwa nini maji yatoke hapa yaende Mombasa na watu wa hapa wakose maji. Pendekezo langu ni kwamba haya maji yakikosa kwenda huko, tupate maji kwanza sisi ni watu ambao maji yanatoka kwetu na ambapo kama ningelikuwa na mtu wangu wa kuuza ukinunua kwa bei mbaya, nikikuambia usinunue hautanunua tena, sasa hayo maji wasisababishe mpaka tukatoboa ama tukate hiyo mfreji. Kitu inatakikana ni kwamba tupate hiyo maji na tulime nayo.

Haya mambo ya wild life yako katika area yetu na imekula nafasi kubwa hata hatuwezi kufunga wanyama kule, kitu iko ni kwamba hata kama ni kuandikwa tunashangaa watu wanapoandikwa hapo, unapopita unapata watu wameandikwa kutoka zamani wewe ukipita pale ni kama kusumbuliwa tu. Kwa hivyo wale watu wako katika area hii wahusishwe kwenda kuandikwa katika hiyo wild life. Tena hiyo wild life pesa inayotoka ni nyingi ambapo tena hawa watu wa area hii hawafaidiki na hiyo wildlife, ni ya kazi gani katika area yetu kama hakuna kitu tunachopata hapa. Wanyama wanauwa. Juzi tu wameuwa mtu hapa sehemu hii, hatujui ni kitu gani kinaendelea. Wanasema wameweka wire, hiyo wire wameweka ni ya kazi gani. Pendekezo langu ni kwamba ikiwezekana kama kutakuwa kumepatikana mtu wowte ameuliwa ama hao wanyama wamekuja kwetu iwekwe ya

kwamba na sisi kama wanavyo tukataza kuingia kule na wanyama hao wakija huku, basi na sisi tuwakataze hao wanyama. Ikiwezekana tuuwe moja tule wale wanaweza kuliwa.

**Com Tobiko**: Asante sana: Jiandikishe pale.

**Bethwel Mboga**: Mimi kwa majina ninaitwa Bethwel Mboga. Mimi ninapendekeza juu ya hawa wazee wa kijiji ambapo hawa wazee ndio ambao wanafanya kazi zaidi hata kushida hawa ma councilors na ma chifu kwa sababu hao ndio uwa wana-organise hii vitu yote ndio mkutano iweze kufanyika. Lakini unaona hiyo kazi wanaofanya ni kazi ya mfano na tunapendekeza kama hii Katiba yetu inaweza kutukubalia kuwa hawa wazee wawe wakihesabiwa na kitu kidogo hapo ndani yake. Pili, ni juu ya hawa wanyama wa pori, au kwa hii national park. Kusema kweli sehemu ya hapa Mbolola au Tausa division eneo kubwa imeenda na hii national park na tunasikia hiyo national park inalipa pesa nyingi lakini ukiangalia watu wa Tausa division au hivi katika shule kama hizi busury hawa watoto ambao wa area hiyo ambao wanyama wao ndio wanaharibiwa ama watu wao ndio wanauliwa na hawa wanyama huwa hawapati chochote. Tunaomba Katiba hii iwe ikiangalia sehemu ambapo itapakana na hawa wanyama ili na wao wawe wakifaidika.

Tatu ni juu ya hizi …………..(inaudible) kusema kweli serikali imekuwa garama yake imekuwa kubwa lakini saa ingine unaweza kwenda kama ni mgonjwa umepeleka huko. Madawa unapoandikiwa ile kitu iko kwa kitabu mtu anaweza kukuambia enda ununue madawa mahali fulani. Ambapo tunaona sasa hapa mabapo kazi zinafanyika zinafanyika kama kazi ya kibinafsi tunaomba Katiba hii irekebishe kama ni mtu ambaye anaye fanaya kazi zake za private awe private na hizi za government ziwe za government. Nafikiria mambo yangu ni hayo.

**Com Tobiko**: Asante sana. Jiandikishe pale.

**Com Zein**: Nikiweza kuchukua furusa hii kuwashukuru kwa dhati kubwa, Wananchi watukufu kwa kuweza kufika hapa na kutoa maoni yenu ambayo tumeyasikia kumeya-record, na maoni haya yatakuwa ni kati ya maoni yatakayotumika kuchangia kuunda Katiba yetu. Pia ningependa kuwashukuru wanakamati wa Katiba katika sehemu ya uwakilishaji Bungeni ya Voi kkwa kazi nzuri na kubwa walioifanya ili sisi kufikia hapa kuja kuvuna maoni mliotoa. Pia tumeshukuru sana kwa dhati kubwa mshirikishi au coordinator wa Tume ya kurekebisha Katiba Wilfrida kwa kazi bora alioifanya hapa pamoja na sehemu zingine za uwakilishaji Bungeni katika wilaya hii ya Taita Taveta. Pia ningependa kuwashukuru kwa niaba yenu hawa vijana waliokuwa wakifanya kazi pamoja na sisi, maanake wao wanafanya kazi muhimu ya kukusanya haya maoni, tumeya-record ili tusipoteze hata neno moja hapa.
Ningependa kuwashukuru na kuwaambia kwamba pengine mkiwa mnafamiana na watu wengine walio katika sehemu za uwakilishaji Bungeni Taveta na Mwatate kwamba kuna kikao kingine cha makomishona watakuwa huko Taveta. Lakini kikao hiki kesho ni siku ya siku kuu ya wafanyikazi, kwa hivyo hatutakuwa na kikao. Lakini Alhamisi Mungu akipenda tarehe mbili mwezi wa tano tutakuwa Mwakinyungi pande hii nadhani. Kuna njia y amkato hapa, ikiwa kuna watu wa sehemu za hapa

ambao hawakupata furusa wanaweza kutumia hii njia ya mkato tutakutania hapa Mwakinyungi. Sasa kama tulipoanza leo asubui tumalize jioni halafu Ijumaa Mungu akipenda tutakuwa Mwatate, Kenyatta High School, tutakuwa tumemaliza kazi ya Mwatate. Sasa hatuna la ziada isipokuwa kumpa furusa hii Mwadime atufungie kazi hii kama tunavyofanya kwa mila na desturi za tume hii ya kurekebisha Katiba kwa kufanya maombi.

**Mwadime**: Wananchi tunawashukuru sana. Nafikiri tungesimama sote halafu tumalize na neema maana yote yalikuwa kama vile hatukuwa tumetarajia. Ama sivyo. Kwa hivyo tusema neema.

Meeting ended at 5.45 p.m.

**&&&&&&&&&&&&&&&&&&&**